ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 25 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha Tarehe 18 Mei, 2017 Mhe. Tatu Mohammed Ussi aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuwasomea majibu hayo kwenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi alitaka kujua ni vikundi vingapi vya Wajasiriamali kati ya vikundi 115 vilvyopewa mikopo vimeanza kurudisha mikopo hiyo na wajasiriamali wangapi waliorejesha mikopo kati ya wajasiriaamali 222 waliopewa mikopo katika mwaka wa fedha 2015/2016 na majibu ya wizara ni kama ifuatavyo:-

Kwa kawaida marejesho ya mikopo hufanyika mwezi mmoja baada ya mkopo kutolewa.

Aidha, kwa mikopo inayohusika na kilimo na ufugaji marejesho yake yanafanyika miezi sita tokea tarehe ya kutolewa. Hivyo, kwa vikundi 115 vilivyopatiwa mikopo vimeaanza kurejesha mikopo yao. Hadi kufikia mwezi April, 2017 mikopo iliyotolewa ina thamani ya Shs. 345,000,000/- kati ya fedha hizo jumla ya Shs. 307,400,000/- ikiwa ni sawa ya asilimia thamanini na tisa (89%) ya mkopo uliotolwa tayari zimesharejeshwa. Aidha, vikundi 13 tayari vimekamilisha marejesho ya mikopo yao. Majina ya vikundi hivyo yameorodheshwa hapa chini.

S/No.	Jina	Pahala Kilipo
1.	Maendeleo Co - op	Vitongoji, Wilaya ya Chake Chake
2.	Mkataa Umoja Co-op	Kinyikani, Wilaya ya Wete
3.	Kibwekiti Co-op	Kambini, Wilaya ya Wete
4.	Kulegalega Si kuanguka	Micheweni, Wilaya ya Micheweni
5.	Safari Njema	Nungwi, Wilaya ya Kaskazini "A"
6.	Tunabahatisha Co-op	Muungoni, Wilaya ya Kusini
7.	Masinyaha B Group	Paje. Wilaya ya Kusini
8.	Tunajiamini	Unguja Ukuu, Wilaya ya Kati
9.	Mvumilivu hula Mbivu	Machui, wilaya ya Kati
10.	Furaha Foro Group	Masingini, Wilaya ya Magharibi "A"
11.	Wakakamavu B Group	Kihinani, Wilaya ya Magharibi "A"
12.	Faraja	Fuoni, Wilaya ya Magharibi "B"
13.	Tuko Imara Co-op	Mkele, Wilaya ya Mjini

Jumla ya wajasiriamali wadogo wadogo 43 kati ya wajasiriamali mmoja mmoja 222 waliopewa mikopo katika mwaka wa fedha 2015/2016 wameweza

kurejesha mikopo yao yenye thamani ya Shs. 44,607,000/-, ambazo sawa na asilimia ishirini na tano (25%) ya mkopo wote wenye thamani ya Shs. 178,428,000/=.

Maelezo ya ziada ni kwamba Mfuko unatoa muda wa miaka 2 mpaka 3 kwa wakopaji kurejesha mikopo yao. Aidha, mikopo hiyo imewanufaisha wajasiriamali wote wadogo wadogo wanaojishughulisha na biashara ndogo ndogo, viwanda vya kusindika matunda, utengenezaji wa sabuni, kilimo cha matunda na mbogamboga na kazi za mikono.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni sana kwa kunisikiliza.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 42

Kufungwa kwa Miundombinu ya Kamera za Usalama (*CCTV*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba nirekebishe kidogo. Kamera zinayozungumzwa hapa sizo zinazoshughulikiwa na *ROM Solution*, kwa sababu zile ni *wireless*. Kamera zinazozungumwa hapa ni Kamera za *ZTE*, zilizoanzia Malindi mpaka Mlandege. kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika naomba nijibiwe swali langu nambari 42.

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya jitihada za makusudi kuwaletea maendeleo wananchi wake na kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao unazingatiwa kwa kufunga kamera za usalama (*CCTV*) katika maeneo mengi ya mjini.

(a) Je, ni kweli miundombinu hiyo ya kamera imeanza kuharibika kabla ya kutumika

(b) Je, sehemu iliyokatwa waya imeingiza hasara ya kiasi gani.

(c) Je, mkandarasi tayari amemaliza kazi na kuikabidhi serikalini

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika kwa idhini yako naomba uniruhusu nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ni imani yangu kwamba majibu ambayo nimeyaandaa yatatosheleza swali hilo ambalo alitaka lijibiwe.

Mhe. Naibu Spika, serikali katika jitihada zake za kupambana na vitendo vya uhalifu na kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebuni mradi wa kuweka kamera za ulinzi kwa lengo la kufuatilia mienendo na matokeo ya kiuhalifu ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi kwa hatua ya awali. Mradi huu utaendelezwa pia katika mikoa yote ya Zanzibar (Unguja na Pemba).

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeunda timu ya wataalamu ya kufuatilia na kutoa taarifa na ushauri kuhusiana na mwenendo wa mradi. Kupitia kamati hii ofisi yetu hupata taarifa zote kuhusiana na maendeleo ya shughuli za mradi. Ofisi yetu kwa sasa haijapokea taarifa yoyote kuhusiana na kuharibika kwa miundombinu au kukatwa *wire* zinazohusiana na Mradi wa Kamera (*CCTV*).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa majibu haya ni ya pamoja, naomba nimwambie Mheshimiwa mradi wa kamera unaotekelezwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ mradi huu bado haujakamilika na shughuli za kuweka miundombinu zinaendelea. Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, kwa vile suala hili linapelekwa kwa Kanuni za Baraza la Wawaklishi ndani ya siku 45 swali lile liwe limefika katika ofisi husika, waziri kwa nini hakupata muda kuunda hiyo kamati yake ndani ya muda wa zile siku ambazo zimewekwa kwa ajili ya kupata majibu sahihi ya suala hili.

Pili, Mhe. Waziri kuacha miundombinu hii ambayo inazungumzwa hapa ya *ZTE* kukatwa *wire*. Je yuko radhi kuona pesa za serikali hata kama za msaada zinapotea kutokana na kutofuatilia kwake, na mkataba wake ni lini watakamilisha mkataba ili wakabidhi katika serikali yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Kwanza yeye mwenyewe amekiri wakati wa kuuliza swali kwamba hakuzungumzia mradi unaosimamiwa kwa fedha za serikali, yaani ule ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais kupitia Kampuni ya *ROM Solution*, yeye amezungumzia mradi ambao unatekelezwa na Kampuni ya *ZTE* ya China ambayo fedha zake ni za msaada sio za mkopo. Lakini Kampuni ya *ZTE* inaendelea na kuweka miundombinu ya mradi ule na bado mradi ule haujakabidhiwa kwetu. kwa hivyo, kama haujakabidhiwa kwetu bado jukumu la kusimamia miundombinu na kugundua jambo lolote lile litakuwa ni la Kampuni ya *ZTE* mpaka pale Kampuni ya *ZTE* itakapoikabidhi rasmi serikali mradi ule. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri ulinzi ni muhimu katika nchi, lakini tumeona mradi huu wa ufungaji kamera unafanyika hapa Unguja. Je, ni lini miji ya Pemba nayo itanufaika na mradi huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Mheshimiwa katika jibu la msingi nilipokuwa nikielezea nilisema kwamba suala la ulinzi katika nchi yetu ni jambo moja ambalo ni muhimu sana na ndio maana nikasema kwamba, mradi huu ambao unatekelezwa ni programu ambayo inalenga katika kuimarisha ulinzi katika visiwa vyetu kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi za serikali ni kuona kwamba ulinzi unaimarishwa maeneo yote ya visiwa vya Unguja na Pemba. Ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa wizara inayohusika. Kwanza niwapongeze mawaziri wote waliojibu swali mama na swali la nyongeza la Mhe. Abdalla Maulid Diwani, nimemfahamu vizuri sana Mhe. Waziri alipoeleza kwamba, fedha za mradi huu ni za msaada. Lakini hata hivyo, fedha hizi kama ni za msaada nafikiri taratibu za kumtafuta mkandarasi zinakuwa ni vile vile, kwamba serikali inapewa pesa za msaada na baadae kumtafuta mkandarasi ambaye anaweza kuendelea na mradi ule.

Swali langu Mhe. Naibu Spika, liko hapa.

(a) Katika utaratibu mzima wa kuingia mikataba mikubwa kama hii serikali huwa inaweka fungu la *guarantee*, sasa kwa sababu kuna viashiria vya uharibifu inawezekana sio sahihi lakini inaweza ikatokea. Je, ni muda gani wa *guarantee* umewekwa katika mradi huu baada ya kukamilika.

(b) Ni kiasi gani cha fedha (*retention money*) iliyotengwa katika mkataba huu wa *CCTV Camera* ili kulinda muda wa *guarantee* pale ambapo itatokezea uharibifu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ya nyongeza ambayo ameyajibu kuhusu mradi mzima na mwelekeo wa serikali katika kuimarisha ulinzi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Hongera sana Mhe. Naibu Waziri. *(Makofi)*

Swali lake Mhe. Rashid Makame naomba kulijibu kama ifuatavyo:

Katika miradi hii miwili ule ambao unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ule ambao unagharamiwa na Kampuni ya *ZTE* kama msaada. Mradi ambao unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar una *guarantee* katika kipindi chote cha miaka mitano na kila kinachotekelezwa kwenye mradi huu kina *full insurance* kwa ajili ya kutekeleza iwapo itatokezea changamoto yoyote ile katika mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa lakini kwenye mradi huu wa *ZTE* kama nilivyosema katika swali nililojbu la nyongeza la Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwamba msaada huu ulipokuja umekuja na msaada wa vifaa na sio fedha taslim. Fedha taslim wanazo wao wenyewe na hawajaikabidhi serikali. Kwa hiyo, hakungekuwa na haja ya sisi kumtafuta mkandarasi na bahati nzuri mkandarasi ni wao wenyewe na kama ni wao wenyewe kwa kadiri ninavyoelewa kampuni hizi ambazo zinafanya kazi hasa katika teknolojia ya kisasa zinakuwa na taratibu zao za kuweza kuweka *guarantee* na kwa sababu hawa pia ni wazalishaji wa vile vifaa kwa hiyo kila kitu ni cha kwao wao wenyewe. Kujua ni kiasi gani ambacho kimewekwa katika mradi huu kwa ajili ya kutekeleza jambo linapokuwa

limetokea la bahati mbaya, siwezi kukwambia lakini wenyewe makisio na gharama ambazo walituletea kwa mujibu wa vifaa ambavyo tumevipokea walitwambia kwamba mradi huu vifaa vyote pamoja na kazi zote zitagharimu jumla ya dola shilingi milioni 3.5. Ahsante sana.

Nam. 4

Udhalilishaji wa Watoto kwa Watoto

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Miongoni mwa kikwazo kikubwa kinachorudisha nyuma maendeleo ya jamii ni suala zima la ongezeko kubwa la kesi za unyanyasaji na ubakaji wa watoto unaofanywa na watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na nane (18).

(a) Je, serikali kupitia wizara yako imejipanga vipi kuhakikisha kwamba idadi ya kesi za unyanyasaji na ubakaji wa watoto kwa watoto wenzao inapungua hasa ukizingatia kuwa Sheria ya Mtoto inazuia mtoto kupelekwa rumande au Chuo cha Mafunzo.

(b) Je, hatuoni kuwapeleka watoto wanaokinzana na sheria katika kituo cha kurekebisha tabia cha *Tanzania Youth Icon Centre (TAI)* lengo kuu huwa halifikiwi ipasavyo. Kwani wanapofika kule baada ya kurekebishwa kisaikolojia huwa wanaangalia Televisheni na kuchezea kompyuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kuongezeka kwa matendo ya unyayasaji na ubakaji wa watoto kwa kiasi kikubwa kunachangiwa na mmong'onyoko wa maadili unaoikumba jamii yetu. Ili kupambana na tatizo hilo, serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali ambazo zimekua zikisaidia sana katika kupunguza idadi ya kesi za unyanyasaji na ubakaji wa watoto. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kutunga Sheria ya Mtoto Nambari 6 ya mwaka 2011. Sheria hii pamoja na mambo mengine inamlinda

mtoto kutokana na matendo mbali mbali ikiwemo matendo ya udhalilishaji.

Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia inaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya kujiepusha na matendo ya udhalilishaji wa watoto, kuwakumbusha wazazi na walezi kufuatilia nyendo za watoto wao na hatua nyengine zinazolenga kukabiliana na vitendo hivi. Hatua hizi zimesaidia sana katika kupunguza matendo ya udhalilishaji.

(b) Mhe. Naibu Spika, Kituo cha kurekebisha tabia cha Tanzania *Youth Icon Centre* (*TAI*) kina majukumu mbalimbali yanayolenga kuwarekebisha tabia watoto wanaokinzana na Sheria. Ili kufikia lengo hilo wafanyakazi wa kituo hiki hulazimika kubaini sababu zilizopelekea mtoto kukinzana na Sheria, mazingira anayoishi mtoto, malezi ya mtoto na kadhalika. Aidha wafanyakazi wa kituo hiki hutumia mbinu mabli mbali za kitaalamu ili kuwafanya watoto waliokinzana na Sheria kuwa watoto wema na kuwajenga kisaikolojia ili wasirejee makosa hayo. Mhe. Naibu Spika, Kutokana na kazi nzuri inayofanywa na kituo hichi, ni dhahiri kwamba Kituo cha kurekebisha tabia cha Tanzania *Youth Icon Centre* kimesaidia sana katika kurekebisha tabia za watoto na kuchezea Komputa na kutizama *TV* ni sehemu ya njia zinazotumika katika kuwajenga kisaikolojia watoto hao. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka kumuuliza swala la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri je, kuna wataalamu wowote waliomea masuala ya kisaikolojia ya kuweza kurekebisha watoto waliofanyiwa makosa ya ubakaji na udhalilishaji na je, wataalamu hao wamepatia chuo gani.

(b) Sheria inaonesha inazingatia zaidi mtoto aliekinzana na sheria. Je, sheria hiyo inamsaidia vipi mtoto aliathirika kisaikoloji na vitendo vya ubakaji na udhalilishaji aliofanyiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe.

Mwakilishi Mwanaidi Kassim Mussa Mwakilishi kupitia Viti vya Wanawake swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Spika, kuhusu wataalamu ambao waliobobea katika masuala haya wataalamu hawa wapo kwa maana ya kwamba huwa wanapata mafunzo kupitia Vyuo mbali mbali. Kwa hivyo, sina uhakika Mhe. Naibu Spika, kwamba ni vyuo gani hivyo. Lakini nimwambie tu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kupitia Viti vya Wanawake kwamba nitakujuilisha kwa njia ya maandishi kujua wataalamu hao wanasoma kupitia vyuo gani.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala la kwamba namna gani sheria hii inasaidia wale watoto ambao wanabakwa. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Sheria ya Watoto nambari 6 ya mwaka 2011 ni Sheria ambayo nzuri sana, sheria ambayo imesheheni kila kitu sheria ambayo inalinda watoto kwa namna yoyote ile. Kwa hivyo, nimwambie kwamba Sheria hii ya Watoto inalinda na ukiangalia vifungu mbali mbali vya sheria ile utaona mtoto huyo analindwa katika mazingira mbali mbali yakiwemo mazingira ya kupatiwa masuala ya elimu yakiwemo mazingira ya kutofanyiwa vitendo viovu na kadhalika.

Kwa hivyo, niwaambie tu Waheshimiwa Wawakilishi tuwe na tabia ile ya kuzisoma hizi sheria kwa sababu unaposoma hii sheria ya mtoto tutapata mambo mengi zaidi na tutakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tunapigania haki za watoto ili kuepuka huo unyanyasaji. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu tuna vita vikubwa hasa vita vya nyanyasaji au ubakaji kwa watoto wetu. Lakini kwa bahati mbaya bado Mahakama zetu maamuzi yake yamebanwa na sheria kwa mfano Mhe. Naibu Spika, Mahmaka ya Mkoa imewekewa muda wa kutoa adhabu kwa miaka saba ushahidi umepatikana lakini hazidi miaka saba.

(a) Je, kwa kuzingatia hili wizara ina mpango gani wa makusudi ili kunusuru watoto wetu wasiendelee kupotezewa maisha yao juu ya kuletwa msaada wa Sheria katika Baraza hili ubadilishwe ili Mahakama ya Mkoa ambazo zinaanzia kesi zetu iwe na uwezo wa

kuanzia miaka hamsini mpaka mia moja ili kulikomesha kabisa tatizo hili lisiendelee katika nchi yetu.

(b) Tumeshuhudia katika kesi mbali mbali ushahidi huwa unapotezewa muda au haupatikani kabisa kutokana na jamii kutoelewa au kutokwenda kutoa ushahidi kwa tendo fulani. Je, Wizara inahamasisha vipi na inatoa somo gani la makusudi ili jamii ielewe kwamba tendo hili baya likatolewe ushahidi ili lipate hukumu ili jamii ielewe kwamba iko katika mazingira salama kwa watoto wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, suala la Mahakama ya Mkoa hutoa kifungu ambacho kisichozidi miaka saba na kama ulivyosema kwamba unahisi ni vyema kuliangalia suala hili. Sasa nimwambie tu Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kwamba sheria mbali mbali ambazo tunaona kwamba hazikidhi haja basi huwa tunazifanyia marekebisho na kwa kuwa na wewe umetoa pendekezo na pendekezo ambalo umelitoa *in direct* sio *direct* kwamba ni vyema hizi sheria ambazo tunahisi kwamba hazitoi fursa ya haki kwa walengwa ni vyema tukazifanyia marekebisho.

Sasa niseme kwamba wazo lako tumelichukuwa kwamba tutaliangalia na kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria iko kwetu iko chini ya Wizara yetu basi wataalamu wale watakaa wataangalia na kama itaonekana ipo haja ya kufanya hivi basi tutafanya hivi bila ya kusita.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali langu la nyongeza:-

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yako mazuri uliyotupa hapa na umeitaja Sheria ya Watoto namba 6 ina haki ya kumlinda mtoto. Lakini sheria hii hii namba 6 kifungu cha 47 inaonekana inamlinda zaidi yule mtoto aliyekinzana na tabia. Lakini hapo hapo kwa mujibu wa maelezo yako ya majibu yako (b) kuna kituo cha *TAI*, kituo hichi kinalenga kurekebisha tabia za watoto wanaokinzana na tabia swali langu liko hapa:-

Je, wizara yako ina taratibu gani nyengine za kufanya kuona wale watoto waliofanyiwa udhalilishaji na wale watoto waliokinzana na tabia ukiachia mbali fidia, kuna utaratibu gani ambao mmeuweka na wao kuanzishiwa kituo ili ile saikolijia waipate katika kile kituo. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe minong'ono imezidi yaani mtu hata akiwa anazungumza hasikilikani kutokana na minong'ono naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukae vizuri ili tuweze kusikiliza. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa tunapokiangalia kifungu cha 46 ambacho amekitaja Mhe. Mwanaasha Khamis Juma utaona kwamba kimeelekeza zaidi kwa wale watoto ambao waliofanya lile tendo kwa maana kwamba wanaweza wakalipa *compensation* au watoto hawa wanaweza wakapelekwa kuitumikia jamii na kadhalika.

Lakini unapokiangalia zaidi unaona kwamba wale ambao wanafanyiwa lile tendo saa nyengine baada ya kupata *compensation* basi unaona kwamba hakuna kinachoendelea. Lakini niseme kwamba ni vyema, ni wazo zuri ambalo tutalichukuwa kuona kwamba wale ambao wanafanyiwa vitendo hivi nao pia wanapata darasa. Kwa maana ya kwamba ni vyema kuwachukuwa pamoja na kwamba tayari wameshapewa fidia ni vyema kuwachukuwa kuwaandalia mazingira mazuri angalau kuwapa athari ya lile tendo ambalo alilofanyiwa na siku nyengine asiweze kurejea tena na sio kumuacha hivi hivi tu.

Kwa hivyo, wazo lako Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ni zuri na tutalichukuwa kuhakikisha kwamba watoto wote ambao wanafanyiwa matendo haya baada kutolewa zile hukumu, kwa hivyo, tusimwache tu hivi hivi na yeye ni vyema tukaa nae tukaweza kumliwaza, tukaweza kumfundisha namna gani pengine kuepukana na mazingira hatarishi ili masuala haya yasiweze kumpata tena. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 107

Taratibu za Mafao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*)

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar *ZSSF* ambao hivi karibuni sheria yake ilifanyiwa marekebisho ili kuimarisha ndio kimbilio la wafanyakazi wengi wa Zanzibar baada ya kustaafu ambapo hutegemea kupata kitu kitachowasaidia kuendeleza maisha yao.

(a) Je, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *ZSSF* una wanachama wangapi kutoka Makampuni binafsi na Mashirika.

(b) Je, Kampuni na Mashirika yanawasilisha michango ya wafanyakazi kila mwezi kwa mujibu wa mishahara halisi ya wafanyakazi wao.

(c) Je, *ZSSF* ina mpango wa kuhakikisha kwamba waajiri wote wanawasilisha michango yao kwa wakati na kutoa adhabu kwa waajiri ambao hawawasilishi michango ya wafanyakazi ikizingatiwa michango hiyo ni haki ya mfanyakazi husika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 107 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mfuko wa *ZSSF* una jumla ya Wanachama waajiri 1386 na waajiriwa 44,801 waajiriwa kutoka Kampuni binafsi na Mashirika. Kati yao, Kampuni binafsi ni 1,352 wakiwa na waajiriwa 41,214 na Mashirika ni 24 yakiwa na waajiriwa 2,804.

(b) Kwa kiasi kikubwa Kampuni binafsi na Mashirika yanawasilisha michango ya wafanyakazi kila mwezi. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya Taasisi huchelewesha michango hiyo na baadhi ya nyakati pia kudanganya kima halisi cha mshahara wa wafanyakazi wao.

(c) *ZSSF* imekuwa ikichukua hatua za kutoa adhabu kwa waajiri wasiowasilisha michango yao kwa wakati au kwa ukamilifu. Kwa taarifa za

karibuni Mfuko umetoa adhabu kwa Kampuni Binafsi 64 ambazo zimekiuka taratibu na kukusanya TZS 8, 393,737 ikiwa ni malipo ya adhabu hiyo pekee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali dogo la nyuongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba bado kuna baadhi ya Makampuni ambayo yanajaribu kudanganya uhalisia wa mishahara ya wafanyakazi wao. Je, wizara kwa kushirikiana na mfuko wetu wa *ZSSF* imejipanga vipi ili kuona kwamba michango hiyo ya mishahara inachangiwa kwa mujibu wa uhalisia wa mishahara na sio inaoandikwa kwenye fomu za waajiri ambazo anaziwasilisha *ZSSF*. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu mama ni kwamba yako mashirika ambayo yanafanya udanganyifu na moja ya kazi kubwa inayofanywa na Mfuko wa Uhifadhi ya Jamii ni kufuatilia na kuhakiki na katika ufatiliaji huo karibu Makampuni binafsi 95 yamekutwa na udanganyifu wa aina moja au nyengine. Lakini wale wasiowasilisha kuna madai ya karibu milioni mia sita na thalathini na sita wasiodai kwa ujumla wake.

Sasa hatua zinazofanywa ni pamoja kwanza ni kutoa taaluma lakini la pili kutoa adhabu na katika kutoa adhabu yapo makampuni karibu 12 katika mwezi wa Januari mpaka Machi mwaka 2017 yalipelekwa Mahakamani. Sita kati yao yalikiri na kukubali kulipa pamoja na adhabu na kuodosha kesi ile Mahakamani na sita tunaendelea nao katika hatua mbali mbali za kimahakama. Kwa hivyo, hatua hizi zinachukuliwa na *ZSSF* itaendelea kufatilia na kila atakaekutwa na kosa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kuniona na mimi nikapata kuuliza swala dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa majibu yake mazuri. Lakini kwa vile tunafahamu kwamba *ZSSF* ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kwa kila mfanyakazi ana uhuru au ana fursa ya kujiunga kwenye mfuko huu. Lakini tukiangalia kwenye haya Makampuni binafsi hususan Mahoteli kuna hawa waajiri ambao wanawa-*force* vibarua wao yaani wafanyakazi wao ambao bado hawajawapatia hata ile mikataba ya uajiri kuwa-*force* kujiunga kwenye mfuko

huu wa *ZSSF* ili mafao yao baada ya kuwafukuza wafanyakazi hawa yaingie kwenye Makampuni yao.

(a) Je, kama wizara ina utaaratibu gani wa kuwafatilia hawa wafanyakazi wa kamapuni haya ambayo wanawadhalilisha wananchi wetu katika kupata mafao yao haya.

(b) Ni hatua gani ambazo zinakuwa zinatekelezwa pale *ZSSF* kwa hawa waajiriwa au hawa vibarua ambao tayari ile mifuko yao imeshakuwepo kule na wanapokwenda kudai wakaambiwa ni lazima kwamba wakatwe asilimia ya kile kiwango chao cha mapato ambacho kiko pale kwenye ule mfuko wa *ZSSF*. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hidaya Ali Makame kama ifuatavyo:

Kwanza kwa mujibu wa sheria za kazi watu wote wanatakiwa wawe na mikataba ya kazi na mara baada ya kuwa na mikataba ya kazi hutakiwa wawasajili wafanyakazi hao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na wakiwasajili pale na baada ya marekebisho ya sheria tuliyoifanya hivi karibuni muajiri anapaswa amchangie mfanyakazi wake asilimia 13 ya mshahara na asilimia 7 inatoka kwenye mshahara wa mfanyakazi mwenyewe.

Kwa hivyo, inakuwa asilimia 20 ya mshahara unaingia kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kwa sababu huu ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa maana ya *Pension Fund* fedha zile haziwezi kutoka hawezi kuzipata muajiri wala muajiriwa kwa sababu ile ni haki ya muajiriwa. Lakini haiwezi kuipata muajiriwa huyo mpaka yatokee mambo mawili ama afikie hatua ya uzeeni kwa maana ya kustaafu, au apate ajali Mwenyezi Mungu apishe mbali kwa watu wetu kwa maana apate sasa ulemavu utakaomsababisha kwamba asiweze kuendelea na kazi, lakini fedha ile inabaki kuwa ni haki ya mfanyakazi mpaka pale atakapozeeka. Lakini akifariki mfanyakazi huyo basi mafao yale yanakwenda kwa warithi wake. Kwa hivyo, hakuna namna ya muajiri baada ya kutoa mchango *ZSSF* akapata mafao ya mfanyakazi huyo.

Nam. 28

Zawadi ya Mshindi wa Pili wa Timu ya Wanawake Zanzibar Kupewa Mshindi wa 3

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza:-

Kwa kuwa tumeshuhudia fainali ya mechi ya mpira wa miguu kwa wanawake hapo Uwanja wa Amani, na ambapo mshindi wa pili katika shindano lile hakupewa zawadi yoyote na matokeo yake mshindi wa tatu ndio aliyepewa zawadi.

(a) Je, ni utaratibu gani uliotumika hata ikapelekea mshindi wa pili asipewe zawadi na kupewa mshindi wa tatu.

(b) Je, kitendo kile hakitopelekea kuwavunja moyo vijana wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 28 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, mechi ambayo imeshuhudiwa na Waheshimiwa Wawakilishi, haikuwa ya mwisho bali mechi ya kukamilisha ratiba ya ligi ya wanawake.

Timu zilizocheza siku hiyo ni *Women Fighter*, ambayo ilijizolea alama 15 na *Bungi Sisters* ilijipatia alama 12 ambayo ilikamilisha ratiba ya mwisho wakiwa na alama 9. Hali hiyo baada ya mchezo wa siku hiyo *Bungi Sisters* ilikuwa ni mshindi wa 3 na ikapelekeka mshindi wa kwanza na wa 2 ndio waliopewa zawadi.

(b) Mhe. Naibu Spika, haki imetendeka na hakuna kitendo chochote kilichofanyika kuwavunja moyo vijana wetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nyengine ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida tumezowea kuona zile timu za mwisho ambazo zinacheza tunaona ndio zinacheza *final* ambapo mshindi wa siku ile wa kwanza ndio anakuwa mshindi wa kwanza na yule aliyecheza naye ndio anakuwa mshindi wa pili. Kutokana

na maelezo ya Mhe. Naibu Waziri napenda nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Je, ni vigezo na utaratibu gani uliotumika hata timu ya Bungi ambayo ilicheza siku ile ya mwisho *Bungi Sisters* kuwa mshindi wa tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwantatu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika swali mama kwamba ile ilikuwa ni kukamilisha ratiba ya awamu ya mwanzo. Lakini kwa kuwa hata tukiona katika mifano ya timu zetu za Majimbo, tunapofikia robo *final* tulikuwa tunaalika viongozi ambao wanakwenda pale na kupewa motisha.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, utaratibu uliotumika pale, kuna vigezo ambavyo vilifuata kwamba ile timu tayari ilishajulikana mshindi wa tatu na mshindi wa mwanzo na wa pili. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali nichukuwe fursa hii kuipongeza pia Club ya Yanga kwa kuwa bingwa wa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini vile vile niwaombee kwa Mwenyezi Mungu Simba na wao wapate nafasi ya kushiriki Tanzania katika mashindano ya *TFA*. Lakini la mwisho nimpongeze sana Rais wa *FIFA* bwana Gianni Infantino kwa kuipongeza pia *Club* ya Yanga kwa kuwa bingwa Tanzania. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar tumefanikiwa kuwa wanachama wa Shirika la Mpira wa Miguu Africa na kwa kuwa Zanzibar, na kwa kuwa Zanzibar tuna timu za wanawake ikiwemo *Women Fighter*, *Bungi Sisters* na nyengine na kwa kuwa timu hizi zinaunda timu ya taifa ya Zanzibar, *Zanzibar Queen* ambayo itashiriki katika mashindano mbali mbali yanayoandaliwa na Shirika la Mpira wa Miguu Afrika. Na kwa kuwa timu zetu za taifa huwa zinawakilisha nchi yetu katika mashindano hayo na bado timu zetu hazina udhamini katika mashindano mbali mbali ya kimataifa.

Je, wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo *ZFA* yenyewe ina mkakati gani kuhakikisha timu hii ya *Zanzibar Queen* inapata udhamini na kushiriki vyema katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali Al-Jazira wa Jimbo la Kikwajuni, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli nakiri kwamba kuna timu yetu ya taifa ya *Zanzibar Queen*, lakini kwa upande wa wizara ikishirikiana *BMTZ* na *ZFA* tayari kwa upande wa wizara sasa hivi tumeshawaita wafadhili mbali mbali, wakiwemo watu wa mahoteli ili waisaidie au wazisaidie timu zetu hizi za taifa ili tuone kwamba zinafanya vizuri kama timu za mataifa megine zinavyofanya vizuri. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali moja dogo tu lenye kifungu (a) na (b).

(a) Tumezowea kwa kipindi kirefu sana kwamba washindi au mabingwa wa madaraja tofauti kutokupata zawadi zenye hadhi na kujenga matumaini ya ushindani katika mashindano ya mpira wa miguu Zanzibar. Sababu kubwa wizara inatoa majibu ya kwamba hawana udhamini ndio sababu inayopelekea hiyo. Lakini tumeshuhudia ligi nyingi ambazo hazina utaratibu.

Kwa mfano, ligi za majimbo na za chama zimekuwa zina motisha zaidi wa zawadi tofauti na zile ligi ambazo ziko katika utaratibu wa kiserikali na kisheria. Je, Mhe. Waziri nataka niulize, kwa kuwa ligi ya daraja la pili ngazi ya taifa imemaliza juzi tu na ndugu zetu *Villa United* kuwa mabingwa wa ligi hiyo. Nataka uniambie mabingwa hao walipewa zawadi gani.

(b) Wizara yako imejipanga vipi na inategemea kutoa zawadi gani kwa sababu ligi iko ukingoni kwa timu ambayo itachukua ubingwa wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote nimpongeze tena Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa kuwapatia Waheshimiwa Wawakilishi majibu sahihi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nimjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, zawadi huwa zinapangwa wakati ligi inapoanzishwa, ikiwa zawadi ya kikombe, ikiwa ni zawadi ya fedha taslim na zawadi nyengine zote hupangwa kwa mujibu wa daraja zake. Mshindi wa kwanza atapatiwa hiki, mshindi wa pili atapatiwa hiki na mshindi wa tatu atapatiwa hiki. Kwa hivyo, kwa maswali yake yote mawili aliyoyauliza, daraja la kwanza na daraja la pili ambao wameshamaliza ligi na ambao watamaliza ligi, *ZFA* inawapangia zawadi kwa mujibu wa daraja zao.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba tulipokuwa tunatoka huko ufadhili ulikuwa ni mgumu kweli, lakini tunakokwenda hivi sasa ufadhili ni mzuri, kwa hivyo watapata zile zawadi kwa mujibu wa taratibu zile zilizowekwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 116

Upandaji wa Miti ya Asili Katika Mji wa Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zenye miti ambayo huonekana/hutumika kama nembo ya Taifa. Miti hiyo ni Mkarafuu na Mnazi huonekana ndani ya Miji tofauti na kwa nchi za wenzetu ambapo miti iliyo na hadhi kama hii hupandwa katika miji ili kuonesha uasili na uzalendo wao pamoja na kuwa kivutio kwa wenyeji na wageni.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa miti hiyo kuipanda ndani ya mjini.

(b) Ni lini Serikali itatangaza na kuanza rasmi kupanda miti hiyo mjini.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuweka utaratibu maalum wa kumlazimisha kila mwenye nyumba mjini kupanda miti hiyo katika eneo lake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 116 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuayavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Ni kweli kuwa kuna baadhi ya nchi zimeifanya baadhi ya miti yao kuwa ni nembo ya Taifa au kuuita Miti ya Taifa. Mfano wa nchi hizo ni Malaysia ambapo mti wa Mdamdam kuwa ni mti wa taifa hilo. Wenyeji wa huko huita *NARA* na unalindwa kwa hadhi zote. Aidha katika nchi za Arabuni

Mitende imepewa hadhi ya Kitaifa na huonekana sehemu nyingi hata kweye mitaa ya barabara "*avenues*" za miji yao.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tunayo miti mingi ambayo ina hadhi ya kimataifa na kitaifa ambayo ingeweza kuwa nembo kwa taifa hili. Mbali ya mikarafuu na minazi, miti ambayo ina hadhi ya kitaifa na kimataifa ni pamoja na Mtakawa ambao kwa mji wa Zanzibar upo mmoja katika bustani ya Forodhani. Kwa bahati mbaya minazi na mikarafuu ni zao la taifa hapa visiwani lakini bado haijapewa hadhi ya kuwa nembo ya Taifa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Wazo la Mhe. Mwakilishi ni zuri na wizara inaahidi kwamba italifanyia kazi. Hata hivyo, naomba nifahamishe kuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishajiisha upandaji wa minazi na mikarafuu kila mwaka. Suala la upandwaji wa miti mijini linaonekana kukua miongoni mwa wanajamii na wamekuwa wakipanda miti ya aina mbali mbali hasa ya kivuli.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza upandaji miti mijini hasa minazi na mikarafuu, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaandaa mpango maalumu wa kupanda minazi na mikarafuu katika maeneo ya mijini. Mpango huu unakusudiwa kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge na Madiwani washiriki na kutoa michango yao ili kufanikisha upandaji wa miti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mpango huu unaojulikana kwa jina la Pamba Visiwa (*beatify the islands*) unakusudiwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Madiwani kusaidia yafuatayo.

- Kila Mbunge na Mwakilishi kuchangia nazi za kitamli 1500 na mikarafuu 500 kwa jimbo lake.
- Kila Mbunge na Mwakilishi wachangie udongo wa kuoteshea miche ya minazi 1,500 na mikarafuu 300 ya jimbo lake.

Kila Mbunge na Mwakilishi wachangie vifuko vya kujaza udongo wa kuoteshea miche ya minazi 1,500 na mikarafuu 500 ya jimbo lake.

Mhe. Naibu Spika, miche hii itakapokuwa tayari, kila Mheshimiwa atakabidhiwa miche yake akawagawie wananchi wake waipande. Kwa kufanya hivyo wazo la Mheshimiwa Mwakilishi la kutaka wananchi walazimishwe kupanda miti hii litakuwa lina pahala pazuri pa kuanzia, hasa katika maeneo ya mijini kama alivyopendekeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wazo hili ni jema tunaomba Wahehshimwa Wawakilishi walipe msukumo na watusaidie katika ushajiishaji, ili msimu wa mwakani miche ifurike vitaluli na ipandwe mijini na vijijini. Serikali haioni haja ya kuweka utaratibu maalumu wa kumlazimisha kila mwenye nyumba kupanda miti hiyo katika eneo lake, kwani kumlazimisha kila mtu apande miti hiyo nyumbani kwake linahusiana na masuala ya kisheria. Hata hivyo namuahidi Mhe. Mjumbe kuwa suala hili tutalitafutia ushauri wa kisheria, ili tuone ni wapi tunaweza kulielekeza na kukidhi malengo yaliyokusudiwa ama kwa kupitia Serikali Kuu au Serikali zetu za Wilaya katika ugatuzi kwa kutumia Kanuni za Manispaa na Halmshauri husika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza nimsifu Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya kitaalam aliyotujibu. Lakini pia niongeze kwamba ameona umuhimu wa mtakawa ambao umehifadhiwa katika bustani ya Forodhani. Sasa nimuambie Mhe. Waziri;

(a) Je, mikarafuu na minazi haoni umuhimu katika ma-*garden* yetu yalioko mjini akaipanda kwa utaalamu ili ikaonekana kwamba miti hii ni muhimu au ni miti ya asili katika kisiwa chetu.

(b) Nimwambie Mhe. Waziri kwamba mkarafuu inaonekana kwamba uzaliwa wake mkubwa ni Kisiwa cha Pemba. Je, upande wa Zanzibar amechukua hatua gani katika kuzalisha mkarafuu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Kwanza nikubali kwamba kwa bahati mbaya hatujaifanya mikarafuu kwamba tunaweza tukaiotesha kila pahali. Hivi karibuni kama mlishuhudia nilikwenda hospitali ya Mkoani tukapanda mkarafuu na tukapanda na mnazi, ili kuwaonesha wananchi kwamba kuna umuhimu wa mti huu ambao ni mti wa taifa, angalau kila pahala tunapoweza kuupanda basi tuupande. Sasa kwa sababu sheria zetu za Serikali za Mitaa bado hatujaweka utaratibu wa kusema aina gani za bustani ziwekwe kwenye bustani zetu. Basi hili jambo tutalifikisha

katika serikali tutalijadili kwa pamoja, ili tuone kweli tunaweza tukaweka mkarafuu katika bustani.

Ila kwa mazingira Mhe. Naibu Spika, inawezekana kabisa ukasababisha kivuli kikubwa sana pembeni ya barabara kwa sababu ni mti mkubwa. Kwa mfano ukienda kama Ugiriki wao wamechagua Michungwa, wana michungwa midogo midogo ukienda barabarani utaikuta na mgeni yeyote anaruhusiwa kuchuma na kula na kila nchi ina utaratibu kama huu wanafanya. Kwa hivyo, nasema ni vizuri suala lako ulililoleta ni suala la kulifanyia utafiti. Je, ni aina gani katika miti yetu mizuri tuliyonayo inafaa kuwa katika bustani ili ipendeze kama ni nembo ya taifa.

(b) Ni kweli kwamba Zanzibar mikarafuu ni michache ukilinganisha na Pemba, nafikiri kuna mikarafuu kama laki 700,000 tu, na serikali hivi sasa imeagiza kwamba tufanye utafiti, ili kuona ni maeneo gani ambayo tunaweza tukaotesha mikarafuu kwa wingi Unguja, ili tuwe na mikarafuu mingi kama vile tulivyokuwa nayo Pemba. Kazi hiyo imeanza, na hasa upande wa Kaskazini Unguja, tumeona kuna ardhi nzuri ambayo inaweza ikaoteshwa mikarafuu na ikawa mikubwa. Kwa hivyo, ndio maana ukaona hata katika hotuba yangu utaona kuna idadi ya miche ambayo tumeiongeza Zanzibar sasa ili iweze kuanza kazi ya kuotesha mikarafuu.

Lakini kuna jambo moja nataka niliseme vile vile kwamba tumejitahidi kuotesha mikarafuu, lakini ukataji wa mikarafuu nao umekuwa mkubwa, ukataji wa minazi vile vile nao umekuwa mkubwa. Kwa hivyo, nasema upande mmoja wa serikali tunajitahidi kuotesha miche na watu binafsi kufanya, lakini wakati huo huo wananchi wanaikata miti hii kwa kasi kubwa sana, na hili ni zao letu la taifa. Tunakumbuka tulikuwa tukisafirisha mbata zamani, sasa hivi hatuthubutu kusafirisha mbata kwa sababu nazi hazipo tena. Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi kwa kweli viongozi wote tulisimamie suala la kukatwa miti na hasa mikarafuu na minazi.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Je, wizara yako ina utaratibu gani wa kuwapa wananchi minazi bure ili wapande kurejesha hadhi ya minazi ile ambayo imekatwa, kama vile ambavyo mnavyotoa mikarafuu bure.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa swali zuri sana. Ni kweli kabisa Serikali huwa tunatoa mikarafuu bure kwa sababu ya kutaka kulifanya zao lirudi katika hali yake ya zamani, ushauri wako tunauchukua ni maamuzi ya Serikali tutapeleka Serikalini tuone kama tunaweza kutoa na miche ya minazi bure vile vile. Ahsante sana.

Mhe. Ahmada Yahaya Abdullwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kumuuliza suala la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri nakufahamu kama umesafiri Dunia nzima na suala la miti katika nchi zilizoendelea linapewa kipaumbele na barabarani kuna miti maalum ambayo inatia *shadow* ili barabara zetu ziweze kuwa na maisha marefu.

Je, kuna mpango gani hasa mjini kupanda miti ya dharura na ya muda mrefu kusudi iweze kupatikana kivuli kwa faida ya binaadamu na hata wengine wanaotembea kwa miguu, miji kama Mexico, Marekani, Uingereza, Ujerumani mpango huu umefaulu sana na hata unatoa tahadhari kwa magari inapotokea ajali kwenda kugusa majumba ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nakubaliana nae kabisa kamba miti inaleta taswira nzuri sana na ni faraja, tuna timu ya wataalam sasa kama 34 ma-*scientist* wanafanya semina hapa Zanzibar juu ya kuangalia namna gani tunaweza kuboresha kilimo chetu. Jambo moja lililowavutia ni kuona Zanzibar kwa sehemu kubwa sana ni kijani, kwa hivyo ujani katika nchi yoyote ile ni sehemu ya kivutio kikubwa sana. Na ndio maana kilio changu kikubwa ni kwamba tunaweza kuchukua juhudi kama Serikali kupanga utaratibu lakini kama hatupati mashirikiano kwa wananchi na kwa baadhi ya viongozi kazi yetu hiyo itakuwa ni ya bure. Mimi nasema tutashauriana na Serikali katika ugatuzi huu tuone ni maeneo gani tunaweza kuyatenga hasa tukapanda miti ya kutosha na tukayatunza vizuri. Hili ni jambo muhimu sana na nakubaliana nalo kabisa tutalifanyia kazi na ndio kazi tunayoifanya katika misitu yetu ya sasa hivi ya hifadhi.

Ukenda pale Kizimbani katika msitu mpya ule tulionao pale Jozani ambao una chanzo kikubwa cha maji tumeifanya sasa ni msitu wa kitalii. Vile vile waliofika pale miti walioiona pale na aina ya miti tuliyonayo ni mingi kuliko sehemu nyingi sana duniani lakini kumbe wenyewe hatujaiendeleza. Tumeanza sasa hivi tumefugua ile *park* pale naomba Waheshimiwa mkipata nafasi

mkatembelee kwanza ukikaa pale unaiona Unguja yote nzima kwenye ile kamera tuliyoweka pale. Naomba mkatembelee mkaone kazi tunayoifanya, lakini tunaomba ushirikiano sana na wananchi na Serikali zetu za mitaa tunazoziunda hizi nafikiri wazo lako ni zuri tutalipeleka ili tuweze kulifanyia kazi.

Nam. 123

Utaratibu wa Vikao vya Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi hufanya vikao vyake kwa ajili ya kutoa hati kwa wamiliki wapya wa maeneo ya Unguja na Pemba.

(a) Je, Bodi hufanya vikao vingapi kwa kila mwezi.

(b) Je, Bodi imeandaa utaratibu gani wa kufanyika vikao kwa upande wa Pemba ili kuwezesha Bodi kufika kwenye eneo pale inapohitajika kufanya hivyo kabla ya kutoa hati.

(c) Je, Wizara ina mpango wowote wa kuipatia Bodi ya Uhaulishaji Ardhi kiwanja cha kujenga Ofisi mpya kilicho karibu na Nyuki Brigedi ambapo inasemekana kwamba Wizara ilikuwa na kiwanja eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 123 lenye vipengele (a), (b), na (c) kama ifuatavyo**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili ni vyema nikatoa maelezo mafupi kuhusiana na Bodi ya uhaulishaji ili Wajumbe waweze kufahamu mamlaka ya chombo hichi kwa mujibu wa Sheria. Bodi ya uhaulishaji ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhaulishaji No. 8 ya Mwaka 1994 ambapo kazi yake kuu ni kujadili na kuthibitisha maombi ya uhaulishaji. Aidha kwa mujibu Sheria ya Haki ya Matumizi ya Ardhi No. 12 ya Mwaka 1992 ni Waziri wa Ardhi ndie mwenye mamlaka pekee ya kutoa Hati za Ardhi. Hivyo ifahamike kuwa Bodi ya Uhaulishaji haina mamlaka ya kutoa hati na kazi yake

ni kuthibitisha uhaulishaji wa ardhi na inatoa cheti cha kuidhinisha uhaulishaji pale maombi la uhaulishaji yanapokubaliwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa kifungu No. 11(1) cha Sheria ya uhaulishaji, Bodi inalazimika kufanya vikao angalau mara moja kwa mwezi. Bali kwa sasa Bodi hufanya vikao kila baada ya siku saba ambapo kwa mwezi hufanya vikao vinne.

(b) Bodi ya uhaulishaji hufanya vikao kwa Unguja na Pemba ambapo kwa upande wa Pemba, Bodi imejipangia kufanya vikao kila baada ya miezi mitatu.

(c) Hakuna mpango wowote kwa Wizara kuipatia Bodi ya Uhaulishaji eneo liliopo karibu na Nyuki Brigedikwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Bodi. Aidha kumbukumbu zetu hazioneshi kwamba Wizara inamiliki kiwanja katika eneo la Nyuki *Brigade*.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ka kunipa ruhusa ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kabla ya kutoa hati kwa Waziri kama mlivyosema kwamba bodi hii huwa inatoa cheti ambacho hicho cheti chenyewe ndio kinampa muongozo yule Waziri kutoa ile hati, na kwa kuwa bodi ya uhaulishaji wa ardhi kama ulivyosema inafanya vikao vinne kwa kila mwezi na imekiri kwamba kuna wajumbe watano na watumishi ambao hatukuwaangalia ni wangapi na wajumbe wao wa *secretary*, lakini mimi suali langu nilitaka kujua.

a) Je, hii bodi ya uhaulishaji wa ardhi pamoja na hao watumishi watakaokuwa nao hiyo siku ya kikao hulipwa shilingi ngapi kama *seating allowance*.

b) Je, Bodi ya uhaulishaji wa ardhi huingiza shilingi ngapi kwa mwezi ili wakaweza kufanya vikao vinne na wakalipana maposho na fedha nyengine iliyobakia ikaweza kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Nianze na (b) kiasi gani inaingia inategemea na maombi na yale yaliyokuwa yamekubaliwa kwa sababu bodi hii ina-*charge* kwa asilimia kutokana na kile kitu chenyewe. Sasa inategemea vitu ambavyo vimekubaliwa katika kuhaulishwa ndio inategemea na hicho kiwango ambacho kinapatikana, kwa hivyo hakuna *fix amount* kwamba kiasi fulani kinaingia kwa mwezi inategemea wingi wa maombi.

Lakini la pili ambalo ni (a) kwamba kiasi gani wanalipwa kama *seating allowance* sikumbuki vizuri labda Mhe. Waziri anaweza kunisaidia.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naomba niendeleze kulijibu swali la Mhe.Omar baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niendelee kujibu kama ifuatavyo:

Kwanza naomba nifahamishe kwamba kile cheti kinachotolewa na bodi ya uhaulishaji si muongozo au *factors* inayotumika ya kwamba ukipata cheti kile ndio unapata hati hapana. Unaweza kupata uhaulishaji lakini bado kama kuna *factors* nyengne ambazo hujaweza kuzitimiza au vitu ambavyo hukuweza kuvifikia basi pia unaweza usipate hati ya umiliki wa ardhi. Kwa hivyo uhaulishaji ni *transfer* ambayo inafanywa kwa mmiliki na mpewaji, kama mnunuzi na muuzaji.

Lakini la pili suali la posho kikawaida bodi ya uendeshaji wanapanga kwa idhini ya Mhe. Waziri, wanajipangia posho na posho zina- *range* kwa sababu kikawaida posho zinatoka kwenda laki tatu mpaka laki tatu na nusu ambazo katika hili watendaji wanakuwa mara nyingi *secretariet* wanapata 300,000/= mpaka 240,000/=. Lakini Wajumbe wanakuwa wanapata laki 350,000/=.

Lakini pia uliuliza suali la mfuko wa Hazina kiasi gani kinakwenda mfuko wa Hazina au fedha ngapi zinakwenda mfuko wa Hazina, kwa mujibu wa bodi ya uhaulishaji ilipoanzishwa ni bodi ambayo inajitegemea na bodi ambayo inatakiwa ikusanye na itumie wenyewe, kwa hivyo tokea imeanzishwa bodi hakuna hata pesa iliyopelekwa kwenye mfuko wa Hazina kwa sababu sheria yenyewe imewaruhusu kutumia hiyo posho na wana kibali maalum kwamba pesa wanazokusanya wazitumie kwa mahitaji yao.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifutavyo:

Wizara ya Ardhi ndio yenye mamlaka ya mashamba yote ya Serikali ya Unguja na Pemba.

Je, ni sababu gani zilizopelekea mashamba ya Serikali yaliyoko Pemba yakawa yako chini ya Wizara ya Kilimo, lakini mashamba ya aina hiyo hiyo yalioko Unguja yakawa chini ya Wizara ya Ardhi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifutavyo:

Ni kweli mashamba ya Serikali haya yote yalikuwa yanamilikiwa na Kamisheni ya Ardhi wakati huo lakini baada ya utaratibu wa Serikali ambao ulifanya mabadiliko, basi mabadiliko yale ya Serikali na kwa Pemba mashamba mengi yale yalikuwa ni mashamba ya karafuu katika zile heka tatu, kwa hivyo Serikali ikafanya maamuzi, mashamba yale ya Pemba wakapewa Wizara ya Kilimo na yawe chini ya msimamizi wa Wizara ya Kilimo, lakini mashamba yote yaliyokuwepo Unguja yakaendelea kubaki chini ya Kamisheni ya Ardhi na mpaka sasa Kamisheni ya Ardhi bado wanaendelea kuyaendeleza ni maamuzi ya Serikali ambayo hayana utata.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Naibu Spika, najua binaadamu umepitikiwa nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali lenye (a) na (b) la nyongeza.

a) Ningependa kujua *statistics* zao ni Wazanzibari wangapi hadi sasa ambao wamepatiwa hati miliki na wangapi Wazanzibari hawana hati miliki ya nyumba zao na viwanja vyao ndani ya Unguja na Pemba.

b) Ni hati ngapi hadi hivi sasa zimeganda kwa Mhe. Waziri ambazo hazijawekwa saini.

Mhe. Naibu Spika:: Hilo sio suala la msingi Mheshimiwa, swali la msingi linahusiana na bodi ya uhaulishaji wa ardhi, halihusiani na suala hilo utaliuliza kwa wakati mwengine Mheshimiwa.

Nam. 1

Gari za Serikali Kutembea Baada ya Saa za Kazi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema ilikuwa ikipiga marufuku kutumia gari za Serikali na za Mashirika ya Umma kutembea baada ya wakati wa kazi isipokuwa kwa dharura maalum na ilikua ikitumia gari ya aina pekee

ya kabila moja kama Landrover kwa viongozi wetu na mtu mwengine yeyote haruhusiwi kutumia gari aina ile. Aidha, gari hizo zilikuwa na vituo vyake vya mafuta ili kupunguza na kudhibiti wizi wa mali za Serikali.

(a) Je, Serikali imeona utaratibu wa kudhibiti gari za Serikali kutumika baada ya saa za kazi hauna maana tena.
(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia gari za Serikali za aina moja na ikawa gari hizo kwa matumizi ya Serikali tu.
(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na vituo vyengine vya mafuta ili kuondoa matatizo yanayojitokeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 1 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, uamuzi wa Serikali wa kuweka utaratibu wa kudhibiti matumizi ya magari za Serikali na Mashirika ya Umma kutumika baada ya saa za kazi ni jambo lililowekwa kisheria kama ilivyoelekezwa katika sheria nambari 13 ya mwaka 2004 *Government Motor Vehicles Act*, kifungu cha 25. Utaratibu huo bado unaendelea kutumika kupitia Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakuu wa Taasisi za Umma ambao wamekabidhiwa dhamana ya kuzitunza na kuzilinda mali za Serikali katika Taasisi zao. Hata hivyo, sheria hiyo imetoa ruhusa kwa baadhi ya watendaji wa Serikali kutumia vyombo hivyo kwa utaratibu maalum.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli Serikali katika miaka ya nyuma ilikua ikitumia gari za aina moja, hii ilitokana na mfumo wa manunuzi uliokuwepo wakati huo ambapo manunuzi yote ikiwemo magari yalikua yakifanywa kupitia Bodi ya Manunuzi ya Kitaifa *"Central Tender Board".* Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi ilipitisha sheria ya manunuzi "*procurement act"* iliyotoa mamlaka kwa Wizara na Taasisi za Umma kufanya manunuzi kupitia Tenda bodi za Taasisi zao kwa kufuata sheria za manunuzi.

(c) Mhe. Naibu Spika**,** kuhusu kuweka vituo vyengine vya mafuta kwa huduma za mafuta ya gari za Serikali ni kwamba, hapo zamani ni kweli ununuzi wa mafuta ulikuwa unafanywa kupitia Bohari Kuu ya Serikali. Aidha, katika juhudi ya Serikali ya kubana matumizi, iliamuliwa kuwa fedha za ununuzi wa mafuta ziwe zikilipwa kupitia

katika mishahara ya wahusika, ambapo kwa kiasi kikubwa zoezi hili limepunguza matumizi makubwa ya mafuta.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nimuongeze swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratbu ni kwamba kila baada ya miaka Mhe. Rais anafanya mabadiliko ya viongozi na pengine kuna viongozi wengine hizi taratibu hawazijui.

a) Je, umewakumbusha hawa Makatibu Wakuu kwamba suala la kutumia gari ya Serikali baada ya saa za kazi kwamba kuna sheria yake.

b) Ni adhabu gani anayopata dereva aliyekuwa anaendesha gari za Serikali bila ya kibali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Hii ni kazi ina wajibu wa Makatibu wakuu wote na wahusika wa taasisi kuzifuatilia na kuzitekeleza sheria zetu tulizoziweka hapa, kwa hivyo nina imani kubwa sana iwapo Katibu Mkuu yeyote atashindwa kutekeleza sheria hii basi mamlaka husika zitawachukulia hatua.

Kuhusu ni adhabu gani wanazopewa hizi adhabu kama ulivyosema kwanza tuna utaratbu wetu mtu hupewa onyo na baadae tukaangalia kama atarejea basi kuna hatua tunamchukulia.

Nam. 37

Upandaji na Uwiano wa Nauli za Gari
Baina ya Unguja na Pemba

Mhe. Shaibu Said Ali - Aliuliza:

Kumekuwa na masikitiko katika jamii kutokana na kupandishwa kwa nauli za usafiri wa gari ndani ya visiwa vya Zanzibar na kutokuwepo uwiano wa nauli hizo baina ya Unguja na Pemba ambapo nauli kwa kilomita 7 za usafiri katika

kisiwa cha Pemba ni sh. 700/= wakati nauli ya umbali kama huo au zaidi kwa upande wa Unguja ni sh. 300/= hadi 400/=.

(a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba kupanda bei hizo kwa Kisiwa kimoja kunaleta malalamiko makubwa kwa jamii ya kisiwa hicho.

(b) Ni lini Wizara itarekebisha bei hizi ili zilingane na kisiwa chengine.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Upangaji wa Nauli za gari za abiria katika visiwa vya Unguja na Pemba unaratibiwa na Bodi ya Usafiri barabarani kama ulivyoelezwa katika kifungu cha 80 cha sheria nambari 7 ya mwka 2003 na utaratibu wake umefafanuliwa katika kanuni ya 101 ya gari za biashara.

(a) Hivyo kwa mujibu wa utaratibu huo kumtoza nauli abiria kinyume na nauli iliyotangazwa na mamlaka husika ni kosa na mkosaji atatozwa faini yenye thamani sawa na Dola 10 za Marekani kwa mujibu wa kifungu 101(6).

(b) Bei ziliopo zimewekwa kwa kufuata taratibu husika kwa visiwa vyote viwili hivyo tayari zisharekebishwa.

Mhe. Shaibu Said Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu ubovu wa barabara ulioko Tomondo mpaka Kwarara ni sawa sawa na ubovu wa barabara iliyoko Pujini, gari linatoka Kijitoupele mpaka Darajani la Daina ni kama linalotoka Ndagoni mpaka Chake Chake.

(a) Je, kuna sababu gani za kimsingi zilizopelekea bodi yake kupandisha bei ya nauli kwa Kisiwa cha Pemba.

(b) Je, wizara yako iko tayari kufuatilia suala hilo na kuona uhalisia wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Shaib Said Ali swalilake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kiutaratibu bei huwa zinapangwa kwa utaratibu maalum, wale *operater* wa sehemu husika huleta maombi yao kupitia Bodi ya Usafiri Barabarani na baadae Bodi ya Usafiri Barabarani iwapo itaridhika kwamba ile bei iongezwe basi huengezwa. Lakini napenda kumuarifu kwamba bei hizi zilizokuwepo hivi sasa zina muda mrefu hazijaengezwa na kwamba tumekubaliana katika makubaliana kwamba bei zisiingezwe mpaka pale bei ya mafuta itakapofika bei isiyopungua Tanzania Shs. 2,370/-. Kwa hivyo niko tayari kulifuatilia hili, na yule yoyote kama nilivyosema mwanzo iwapo atakiuka taratibu zetu hizi basi tunampeleka polisi na baadae kutozwa faini ile iliyoitaja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, nami kwanza niungane na muuliza swali mama juu ya nauli kubwa kwa Kisiwa cha Pemba. Kwa kuwa swali kama hili nililiuliza mwaka jana kuhusu barabara yetu inayotoka Wete – Konde na Wete – Micheweni juu ya upandishaji wa nauli kubwa kwa abiria wanaoteremka njiani.

Kutoka Wete mpaka kama Finya wanatozwa shilingi 1,000 wakati ni kilomita 8 tu, hali kadhalika kutoka Wete mpaka Kinyasini kama kilo mita 5 na kidogo tu wanatozwa shilingi 1,000 je, ni lini Bodi ya Usafiri wa barabarani kwa kutumia kifungu hicho hicho cha 80 cha Sheria Nam.7 ya mwaka 2003 kitaweza kuondoa tatizo hili, ili wananchi waondokane na kadhia hiyo. Je, bei hii iliyopo kwa sasa imepangwa na nani hata wakaweza kuzitumia wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sna Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mgogoni swali lake la lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Katika kujibu swali mama na vile vile, katika kumjibu Mhe. Shaib nimeelezea kwamba katika Bodi yetu nataka kumfahamisha tu kuna wajumbe wawili ambao wanatokana na wenye daladala au gari za kuchukulia abiria mmoja kutoka Pemba na mmoja kutoka Unguja. Sasa katika ile Bodi wao ndio wanatakiwa walete malalamiko yao kama kuna ongezeko la bei au vipi, lakini hata hivyo kuhusu swali lako kwamba wale abiria wanaoshuka kati kutozwa bei ya kwenda kule hili nitalichukuwa na kulifanyia kazi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu yake alitwambia kwamba kuna sheria ambayo ipo imewekwa kwa mujibu wa utaratibu kuhusu maswala ya nauli naomba kumuuliza ni gari ngapi zilizokeuka sheria hizi na wameweza kulizipisha fidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mwakilishi Nafasi za Wanawake kwamba:

Kiutaratibu kosa linapofanyika linapelekwa polisi na polisi baadae linapelekwa mahakamani. Kwa hivyo huo ndio utaratibu wa kujua wahusika wangapi ambao wamefikishwa mahakamani na kutozwa faini. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

HOJA YA SERIKALI

Makaridio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Mussa Foum Mussa atafuatia Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo asubuhi hii ya leo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwapo hapa na tunaendelea na kazi yetu. Pili vile vile nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kutuletea Hotuba hii nzuri na tunaendelea kuijadili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani zangu hizo na mimi nataka nianze kuchangia. Kwanza mimi nitaanza programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, kwanza niipongeze programu hii, kwa sababu ni programu ambayo inawaweka au inaanza kimsingi kuwatengeneza vizuri vijana wetu, tunaoanza kuwapeleka katika kuendelea na masomo, kama inavyojieleza programu hii,

ipo katika ukurasa wa 44 *paragraph* ya 64 naomba ninukuu maelezo yake yanavyosema:

> "Programu hii madhumuni yake kumtayarisha mwanafunzi awe aweze kusoma, kuandika, kuhesabu" pia "programu hii ina madhumuni ya kumtayarisha mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya Elimu ya Msingi kumuwezesha mwanafunzi awe aweze kusoma kuandika na kuhesabu".

Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo hayo kama yaliyojieleza madhumuni yake naendelea kuipongeza hii programu, lakini mimi katika Skuli yangu ya Muambe naendelea kusema kwamba kuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu na hasa hasa katika Skuli yetu hii ya Msingi. Pale tuna wanafunzi 2,640 mahitaji ya walimu yanajionesha kwamba tuwe na walimu 60 lakini tunao walimu 28 ina maana upungufu pale ni walimu 32 huu upungufu mkubwa sana, tuna mikondo mitatu ya wanafunzi, sasa mkondo wa kwanza unaingia 1:15 hadi 3:55 hapa tu nikuonesha kwamba hiyo kumuandaa mtoto aweze kuyafanya au kuyatenda yale yote tuliyoyaeleza hapa mwanzo muda mdogo halafu baadae wanaingia 4:00 mpaka 6:00 na saa 7:00 mpaka 11:55.

Mhe. Naibu Spika, hali sio nzuri, upungufu mkubwa na mimi hapa namuomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri hoja yangu inakuja hivi kwamba. Katika Wilaya yetu ya Mkoani sijui huu ugavi unaendaendaje. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anijibu na naomba kwamba anieleze hasa hasa nnavyotaka, alau Skuli tatu, kwa mfano Skuli ya Kengeja, Skuli ya Kiwani na Skuli ya Mtambile, anielezee ule upungufu je, unalingana na upungufu huu, kwa sababu huu upungufu ni mkubwa upungufu wa walimu 32 ni mkubwa je, huu ugavi nani anayegawa na suala hili tu nimekuwa nikilieleza siku nyingi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa naomba kidogo ukae nimpishe Mhe. Mwenyekiti halafu utaendelea baadae.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti alikalia kiti)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naendelea katika hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti hali ya Skuli ya Muambe kwa walimu hali sio nzuri Skuli ya Msingi upungufu mkubwa sana, na mimi sisemi kwamba hatujui kwamba kuna usumbufu wa walimu tunalijua hilo lakini hoja yangu tunalijua hilo, lakini hoja yangu kwa nini Skuli yetu iwe upungufu mkubwa kulingana na skuli

zilizokuwepo jirani yake, hii ndio hoja yangu alau ile Skuli ya Muambe iwe na usumbufu wa walimu 30 pengine iwe 28, 20 lakini unaweza ukenda skuli nyengine kuna upungufu wa walimu 7 walimu 10 kwa nini skuli hii iwe na upungufu mkubwa je, huyo mgawaji halioni hili. Sasa mimi sitaki niseme kwamba nitapiga buti katika wizara hii kuhusu hili, nnaloliomba kwamba nije nipate majibu mazuri tu yenye kuridhisha hata mkinijibu kwamba Mheshimiwa tunajua ulipita ubinadamu basi mie nitaridhika. Lakini nataka jawabu nitakayojibiwa hapa ilingane je, hili suala ni kwanza je ni kweli, lilitokea kosa katika ukawaji ndio ikatokea hivi mimi nitaridhika.

Mhe. Mwenyekiti vile vile, niseme kwamba Skuli yetu ya Muambe tumepata hasara katika mvua hizi zilizonyesha, tuna tatizo la vyoo, pale vipo vyoo vya zamani na tulikuwa tumejenga choo hakijamalizika lakini kutokana na mvua zilizotokea hali sio nzuri, kwa hivyo unamuomba Mhe. Waziri nahili alifahamu ingawaje Mhe. Naibu Waziri alitembelea pale na akaiona hiyo hali na tunategemea kwamba wizara suala hili itaji-*coment* ili kulitekeleza suala lile kwamba vijana wetu wapate sehemu ya kujihifadhia. Pia, Mhe. Mwenyekiti niipongeze wizara kwamba katika skuli zitakazojengwa za ghorofa na sisi Muambe tutajengewa Skuli moja ya ghorofa. Kwa hivyo naipongeza wizara kwa kuliona hili, na hili limekuja kwa sababu kubwa nao wameiona.

Mhe. Mwenyekiti, Muambe imekuwa kubwa kwa sababu imezaa shehia tatu hivi sasa, lakini skuli tunayoitumia ni Skuli hii hii moja shehia zote. Kwa hivyo tuna vijana wengi wanaohitaji kwenda skuli, hilo kundi lililokuwepo nje ni kubwa zaidi kuliko lililokuwa skuli sasa kwa hivyo wakati muafaka kwa wizara kuiona hii hali na wao wakaona kwamba skuli moja basi ijengwe Muambe ya ghorofa, kwa hivyo naipongeza wizara kwa sababu hii kubwa waliotuona.

Mhe. Mwenyekiti vile vile, niende katika Skuli ya Mtangani shehia ya Mtangani, kule kuna banda lililojengwa nadhani kwa msaada (ADB) banda lile siku za mvua vijana hawawezi kusomea kwa sababu lote linavuja, na Mhe. Naibu Waziri nadhani siku moja alikuja tukaenda shirika na tulienda pamoja na sheha wa kule na banda lile tukaoneshwa sote na hivi karibuni mvua hizi, sheha wa Mtangani kanipigia simu vijana kipindi hichi hawawezi kusoma ndani ya banda hili lote linavujisha. Kwa hivyo, naiomba wizara namuomba Mhe. Waziri na hili suala hili alione ili tufanye *maintenance* katika banda lile ili siku za mvua eee vijana wetu waendelee kujisomea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nadhani Mhe. Waziri kanisikia vizuri sasa niende katika Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuendelea kutoa huduma hii ya mikopo juu ya

wananchi wetu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa mikopo haitolewi na Serikali basi vijana wengi wa kimasikini wangeendelea kubaki nje kwa kushindwa kulipa huduma hii ya kusoma. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, nina masikitiko kidogo masikitiko yangu haya sijui kwamba wizara inayajua au inafanywa na watu wale wale watu wa mikopo sasa hapa Mhe. Waziri atapokuja atueleze, kwamba mikopo inatolewa lakini unapofika ule wakati wa kutoa mikopo kuna kuwa na masharti. Masharti yanajieleza kwamba wale wote ambao kuwa wanataka kwenda kusoma masomo ya *Art* wao hawapati mikopo, wanaopata mikopo ni wale wanao masomo ya sayansi tu. Je, sasa ni kusema hawa vijana wetu waliokuwa wazee wao masikini lakini wanataka kwenda kusoma masomo ya *Art,* wasisome iwe basi kwa sababu hali ni ngumu huko nje.

Watu masikini hawana uwezo wa kusomesha vijana wao sasa tukiweka vikwazo hivi ina maana ni kusema vijana wote wa kimasikini, wale wanaokwenda kusoma masomo ya *Art* watakuwa hawasomi, sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja je, hili suala ni kweli au kuna maelezo maelezo gani hapa ili na sisi tujue kwa sababu mara hii vijana wengi mimi wamenifuata na wakanieleza kwamba tuliomba mikopo lakini tulipokwenda tulipewa maelezo haya na uwezo hatuna je, sasa tufanye nini. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja tueleze hali halisi na mimi naiomba Serikali, Serikali bado ina nia nzuri ya kusomesha vijana wetu wa kusaidia, lakini iendelee na wale vijana ambao kuwa wanataka kusoma ya *Art* na wao waendelee kupata mikopo, kwa sababu tukifanya vizingiti kama hivyo ni kusema kwamba vijana wetu wengine watakosa kusoma kwa sababu wazee wao ni masikini.

Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo vile vile, niende katika michezo katika skuli zetu kwanza nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa nia yake safi ya kuonesha kwamba anataka skuli zetu zirudishe mambo ya michezo, kwa sababu kipindi kikubwa skuli zetu zilikuwa hazina michezo tukiacha skuli za zamani na hivi sasa nadhani vijana kidogo wameshaonesha vipaji cha kuiendeleza michezo. Lakini vile vile, naiomba wizara zamani ukiacha hii michezo ya riadha, mpira lakini vile vile, tulikuwa na michezo ya kuwajenga vijana wetu katika njia ukakamavu, kwa mfano tulikuwa na michezo ya gwaride, gwaride lilikuwa linajenga heshima, linajenga ukakamavu na vijana walikuwa wana heshima nzuri.

Sisi wengi nadhani humu tumecheza paunia, kulikuwa kuna siku maalum ya paunia katika maskuli yetu. Mhe. Waziri namuomba na hili lifikiriwe ionekane kwamba kuna umuhimu wa hili jambo nalo kulirudisha. Mfano mzuri tuangalieni katika sherehe za Muungano mara hii zilizofanyika Dodoma.

Tumeona kuna baadhi ya skuli wamechaguliwa vijana wamecheza gwaride uwanjani wameingia pala kama kikosi cha *commando*. Tunapendekeza kwamba mara hii kwenye Sherehe za Mapinduzi tuwaone na vijana wetu na wao wanaingia pale Amani kwa msisitizo mzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia habari ya malimbikizo ya walimu, kuna walimu wengi wanadai malimbikizo yao. Nadhani kulikuwa na utaratibu kwamba kuna walimu waliokuwa wanauzoefu wameshasomesha kwa miaka 30, kulikuwa na tunzo zao wanazopewa. Nadhani hili liendelee wanadai.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi sitokuwa na mchango mkubwa, yale mengi ambayo niliyokuwa nimeyaweka nichangie yameshazungumzwa, hakuna haja ya kuyarejea rejea.

Naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 90, asilimia 10 akinijibu wala sina haja hiyo, wala sipendi, kupiga buti. Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis akifuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Suleiman Makame Ali alijitayarishe.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wanzangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa juhudi zao za kuhakikisha elimu nchini inaimarika.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 44 programu ya kwanza Elimu ya Maandalizi na Msingi. Nichukue fursa hii kumpongeza tena Mhe. Waziri lakini vile vile serikali kwa ujumla kwa jitihada zake za kuhakikisha huduma ya elimu zinaimarika kwa kuongeza majengo yaani mashule lakini vile vile kuwaajiri walimu wenye fani tofauti ambayo wanasaidia kuendeleza upatikanaji wa elimu kwa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu kwa program hii nilitaka tu kumuuliza Mhe. Waziri kutokana wale walimu ambao wameshajitolea kwa miaka mingi. Wamejitolea kwa lengo la kusaidia watoto wetu na wengine waliahidiwa wataweza kupatiwa ajira pale ambapo zitatolewa ajira. Tukiangalia nafasi za

ajira tulizonazo tulizozisikia zinatangazwa ni chache. Ningemuomba Mhe. Waziri akija atueleze kuna mpango gani kwa walimu waliojitolea siku nyingi na wana tamaa ya kupata ajira, labda wao watafikiriwa vipi na Wizara.

Mhe. Mwenyekitik, katika programu hii kulizungumziwa suala zima la ufatiliaji. Kabla ya kuzungumza chochote nimpongeze sana Mhe. Waziri, mimi ni shahidi nilimuona akifuatilia baadhi ya skuli kwa kuwahoji walimu jinsi gani wanawahudumia wale watoto na wanavyowachunga na vile vile jinsi gani wanafundisha na kupita madarasani kuangalia mabuku ya wanafunzi kwa lengo la kujiridhisha elimu inayotolewa na walimu wale. Ni jambo la kupongezwa na ni mfano wa kuigwa na wengine. Bila ya ufatiliaji hakuna jambo litakalofanyika. Juzi nilivyochangia nikasema kwamba viongozi wajaribu kufatilia wasikae mezani kusuribi kupokea taarifa. Mhe. Waziri huyu ni mfano wa kuigwa kutokana na kazi zake tunazomuona anazifanya na sote ni mashahidi hata kwenye vyombo vya habari tulimuona.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe aendelee na zoezi lile, itapelekea wale walimu kujua kwamba kuna ufatiliaji unafanyika na kujiweka tayari wakati wote. Nafikiri zile lawama za wazazi kwamba watoto hawapati elimu vizuri walimu hawasomeshi, walimu wataweza kujipanga na elimu itaweza kupatikana vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika programu ya 5 ukurasa wa 59 juu ya suala zima la ukaguzi. Ukaguzi umezungumzwa ndani ya kitabu hiki kwa mapana yake. Nakumbuka mimi zamani nilipokuwa nikisoma kulikuwa kunakuja wakaguzi maskulini na walimu wakati wowote wanakuwa wanajiweka tayari kwa sababu ukaguzi ule unakuwa wakati wowote wanafuatiliwa na hawajui muda gani. Ukaguzi ule ulikuwa unafanyika kwa mwalimu mmoja mmoja wanapita madarasani wanakaa na kuangalia jinsi gani mwalimu anafundisha na kuangalia madaftari ya wananchi. Kiasi cha kwamba wanajua kupima uwezo wa walimu tuliokuwa nao katika maskuli yetu. Sijui hivi sasa ufatiliaji ule au ukaguzi ukoje? Ningemuomba Mhe. Waziri akija anieleze kwamba sasa kuna utaratibu gani wa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimshauri kwamba utaratibu ule ungerudi kwa kurudisha heshima kwa walimu na kufanya majukumu yao vizuri. Utakuta walimu pengine mwalimu yupo nje watoto wamo ndani watoto wanasokotana, pamoja na kuwa na wingi wa wanafunzi katika madarasa, lakini vile vile na utaratibu haupo vizuri kwa walimu wetu. Lakini tukirudisha utaratibu ule wa ukaguzi kukaguliwa walimu pia tutajua nani ana uwezo nani hana tukapunguza wale walimu wazembe na wao pia watapunguza kufanya uzembe wakiwa

kazini ukizingatia wanalipwa mishahara kila mwezi, kwa hivyo wataweza kutekeleza wajibu wao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije programu hiyo hiyo ya 5 ukurasa wa 54 kifungu cha 95, Programu ndogo ya kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Naomba nichukue fursa hii tena kuipongeza sana kwa kuhakikisha elimu Zanzibar inatolewa kwa wote kwa kuzingatia ujumuishi katika elimu kwa kununua vifaa ambavyo vinawawezesha watu wenye ulemavu tofauti kuweza kujifunza. Hili ni jambo la kulipongeza na nithubutu kusema kwamba tulipotoka sipo tulipo sasa. Zamani huduma za watu wenye ulemavu au elimu ilikuwa elimu haizingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu. Sasa serikali imejitahidi kwa kununua vitabu ingawa changamoto haziishi lakini kwa kweli serikali imejitahidi kwa hili na ni lazima niwapongeze.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu hizo kuna maeneo machache yanahitaji Mhe. Waziri anasikilize vizuri na ayazingatie na ayafanyie suluhisho lake. Mwaka 2015/16 Kitengo hichi kilipangiwa bajeti milioni 60 lakini cha kusikitisha kilipatiwa laki nane tu ambayo ni sawa na asilimia moja ya bajeti nzima waliyopangiwa. Hili ni jambo la kusikitisha, laki nane (800,000) kwa kitengo kama hichi haweza kufanya kitu hata kidogo kwa sababu wana mambo mengi. Isitoshe hiyo mwaka 2016/17 walipangiwa bajeti lakini nimejaribu kuangalia katika kitabu hichi sikuona ni asilimia ngapi wamepatiwa. Bajeti hii ya 2017/18 wamepangiwa milioni 40 kutoka milioni 60, kutokana na mahitaji ya watu wenye ulemavu wanahitaji mambo mengi. Wizara inajitahidi kama nilivyosema kunua vifaa mbali mbali mfano *wheelchair*, na vifaa vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, vifaa hivi huwa vinatumika na katika kutumika vifaa hivi huwa vinaharibika na vinapoharibika wanafunzi wanakuwa saa nyengine kifaa kikishaharibika anakuwa haendelei tena na masomo. Panahitaji pesa za kufanyia matengenezo vile vifaa. Lakini isitoshe elimu mjumuisho ina changamoto nyingi ambazo tunakuwa tunazipigia kelele. Ili kuhakikisha changamoto zile zinaondoka ni lazima kuwe na ufatiliaji, patahitajika fedha kwa ajili ya ufatiliaji ili kuona kwamba elimu ile inakidhi haja na inakwenda katika viwango ambavyo vinatakiwa. Kutokana na utoaji wa bejeti wa kiasi kama hichi, sifikirii kwamba tutaweza kufika pahali pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kupitia bajeti hii kwa hichi kiasi ambacho tumekiweka hapa nimuombe sana na kwa vile Waziri wetu ni Waziri msikivu natumai atalikubali ombi letu. Hii bajeti ambayo imepatingiwa kitengo hichi kwa mwaka huu ningeomba sana sana wakapatiwa kama ilivyopangwa

pamoja na udogo wake ili wakaweza kukamilisha yale malengo pamoja na mipango yao kama walivyoipanga.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mengi ya kuzungumza lakini sitopoteza muda kwa vile wanzangu mengi wameshayazungumza niiunge mkono hoja kwa asilimi 100 huku nikitumaini kwamba Mhe. Waziri atauzingatia ushauri wangu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis nafasi za watu wenye ulemavu, sasa nimwite Mhe. Bahati Khamis Kombo akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame na Mhe. Tatu Mohamed Ussi ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuniona asubuhi hii. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kufika hapa katika Baraza letu tukufu na tukaweza kuijadili hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa juhudi zake ambazo anazichukua kutuletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Pemba si muda mrefu tutaanza kuchimba mafuta ili tuweze kunufaika.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpe shukurani za pekee Mhe. Waziri wa Elimu, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zao ambazo wanazozichukua katika kazi zao, naamini kwamba ni kweli Uwawaza tunaweza bila ya kuwezeshwa na ndio maana Mhe. Rais akamteuwa Mhe. Riziki Pemba Juma kuwa Waziri wa Elimu ni ukuta na ukuta usiokatika kirahisi, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, mengi wenzetu wameshayazungumza tukiyalinganisha yote matatizo ni sawa sawa matatizo tuliyonayo ndani ya majimbo, lakini watu wanasema kila anayelia anasema mama yangu hasemi mama yetu. Na mimi naomba nichangie kidogo yale ambayo yamenigusa ndani ya jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa skuli za Maandalizi katika skuli ya Ukutini. Wananchi wa Shehia ya Ukutini walikuwa na tabu sana kwenda Chambani kutokana na mito na maji ya mvua mengi ambayo tuliyokuwa tukiyapata wakati ule bado hatujakuwa na skuli. Kwa juhudi za wananchi wa Shehia ya Ukutini walijitolea wenyewe kujenga chekechea na chekechea ile ilizaa Skuli ya msingi na leo tuna skuli ya Sekondari. Ni jambo la kusikitisha chekechea ile huu ni mwaka wa 17 walimu hawajaajiriwa wanaendelea kujenga

taifa na michango kidogo wanayoitoa wazee. Kama tunavyojua kwamba wazee ni masikini, michango yao pengine inafikia mtu miezi sita bado hajalipia.

Vile vile skuli ile ya msingi iliyopo hivi sasa imezaa chekechea, sasa imekuwa ni ugumu mkubwa mno kwa wale walimu ambao ni waanzilishi wa skuli ile ye chekechea iliyopo Ukutini. Hapa nilitaka kujua Mhe. Waziri hawa walimu ambao ni waanzilishi mwaka huu wa 17 amekuwa akiwafikiria nini. Atakapokuja kufanya majumuisho naomba anieleze juu ya walimu hao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika skuli yangu ya chambani na Ukutini kuna walimu ambao wanasomesha baadhi ya siku wanakwenda Chambani na baadhi ya siku wanakaa ukutini na wengine wanakwenda katika Skuli ya Chwaka imekuwa ni tatizo kubwa mno kuhusiana na ukosefu wa walimu. Humu nimeona katika kitabu chako hichi kuna walimu wa sayansi ambao wataajiriwa 258 hawa hawatoshi. Nikwambie tu Mhe. Waziri ndani ya jimbo langu mimi la Chambani nahitaji karibu walimu 100 wa sayansi na ambao waliokuwa sio wa sayansi kwa ujumla wao wote. Mhe. Waziri walimu hawa 258 naomba utakapokuja utwambie utawagawa vipi katika usuli zetu ili na sisi tuone Chambani walimu wa sayansi tunao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la makaazi ya wanafunzi, yapo mabanda yameshafikiwa kiwango cha kuezekwa na Wizara yako ya elimu. Naomba Wizara ya Elimu ichukue jitihada za makusudi kwenda Chambani kuwaona wananchi walivyofanya juhudi zao mpaka pale walipofikia ili na wao waweze kuezekewa yale mabanda ili wananchi wetu waweze kusoma vizuri. Kuna madarasa wanasoma wanafunzi kuanzia 90 mpaka 110. Hivi sasa ninavyokwambia kuna walimu ambao tayari keshokutwa wanastaafu. Huko nyuma nilileta swali langu katika Baraza hili hili nina ukosefu wa walimu. Nakuomba uiangalie sana Skuli ya Chambani ina matatizo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Skuli ya Ngwachani Bondeni ile skuli ina tatizo la vyoo, wanafunzi hawana vyoo, kipindi hichi cha mvua imepata athari ya mpasuko ile skuli yenyewe. Nakuomba Mhe. Waziri utakapofanya ziara ya kwenda Pemba basi ulitupie macho banda ya skuli liliopo Skuli ya Bondeni. Isitoshe skuli yangu ya maendeleo iliyopo Ngwachani ni Skuli nzuri inatajikana vizuri lakini inavuja, ikinyesha mvua ni tatizo na kuna wanafunzi hivi sasa wanakaa chini ndani ya ukumbi wa mkutano ndimo wanamosomea wanafunzi. Naomba Mhe. Waziri niangaliwe Skuli ya Maendeleo isiwe ukiitizama nje ni ya kifahari lakini ikinyesha mvua wanakimbizana limekuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Wambaa wanafunzi hivi sasa hawana pa kukaa, ni tatizo kubwa sana mabanda hawana walimu wamehemewa hawajui wanafunzi wale wawapeleke wapi. Naiomba Wizara ifanye ziara makusudi iende katika skuli ya Wambaa kuliangalia tatizo hili na kupata ufumbuzi. Pia kuna Skuli ya Amali ambayo ipo Mahuduthi ile Skuli imekuwa ni tatizo, haina vifaa vya kusomeshea, lakini pia wanapotaka kufanya *practical* ni lazima waende katika Skuli ya Fidel-Casro. Imekuwa ni kero kwa sababu ni mbali na pia pale ilipofunguliwa ile skuli kuna viongozi ambao walitoa ahadi ya kupeleka *computer* mpaka hii leo ahadi ile bado haijatekelezwa na walimu wa mafunzo hapana. Namuomba Mhe. Waziri awaangalie kwa kina ili ile skuli iweze kupata hadhi yake ya amali vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tunayo Skuli ya Kengeja, skuli ni kongwe lani ile skuli imekuwa ni chakavu mno. Namuomba Mhe. Waziri iangaliwe angalau kwa kufanyiwa *repair* ili iweze kutukuka na wale wanafunzi walioko pale waone kwamba na wao hawakuachwa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala la ajira Mhe. Mwenyekiti tunao walimu wengi ambao wameshamaliza kusoma na wengine tayari wanaendelea kujenga taifa lakini Mhe. Naibu Waziri hapa aliwahi kutuambia kwamba wale ambao wanajenga taifa Serikali haiwaelewi vizuri kwa malipo, sasa je hivi sasa ajira zinatoka na hawa baadhi yao wamekaa nyumbani watasaidiwaje na wao tayari pale wameshapoteza nguvu zao zaidi ya miaka mitano au sita, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atuelekeze jinsi gani atawasaidia hawa walimu ambao walikuwa wakijenga taifa katika skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa hayo machache nimalizie kwa sababu kadiri utakavyozungumza ni mengi ambayo wenzetu wameshayazungumza na kila atakayesimama hapa ana malalamiko hayo hayo tunaendelea nayo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache ahsante sana nakushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani naunga mkono hotuba hii kwa asilimia sabini, thalathini mpaka nitakapopata majibu yangu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis Kombo wa Jimbo la Chambani kwa mchango wako mzuri sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali akifuatiwa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nami nashukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla sijachangia niipongeze Wizara kwa uongozi wake mahiri, madhubuti kwa kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Zanzibar wanapata elimu iliyo sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba elimu ni moja ya haki ya msingi wa kila mwananchi na ni nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo kutoka kwenye Ilani ya CCM niende kwenye bajeti iliyopita kwenye Mpango wa Utekelezaji wa 2016/2017 walisema hapa kwamba wataajiri wafanyakazi 90,942 walimu 400 wa sayansi, wakutubi 300, watunza maabara 200 na maafisa wa fani mbali mbali 42.

Mhe. Mwenyekiti, walisema kwamba watakamilisha ujenzi wa madarasa 120 ya maandalizi na msingi yaliyoanzishwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitaka nimuulize Mhe. Waziri kwamba Jimbo langu la Ziwani walimu wangapi wa sayansi wamepatikana pale ndani ya kipindi kile 2016/2017 lakini pia vile vile ni madarasa mangapi ambayo kwamba yamejengwa katika jimbo langu la Ziwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hii bajeti mpya walitwambia kwamba kuna majengo ya skuli ya Kwale yamejengwa. Mhe. Mwenyekiti nimwambie Mhe. Waziri na ninadhani Afisa Mdhamini yupo ni shahidi anajua kwamba Skuli ya Kwale bado iliyotengezwa na watu wa Milele ni Skuli ya Birikau, nashukuru watu wa Milele kwa kutengeneza mabanda yale manane yanang'ara na yanavutia na msimamizi wa masuala yale alikuwa Afisa Mdhamini nampongeza sana kwa sababu alihakikisha na yeye walimshirikisha akalisimamia lile mpaka akakabidhiwa na siku alokabidhiwa Afisa Mdhamini alinialika na mimi nikawepo, kwa hivyo namshukuru sana kwenye suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Skuli ya Kwale ambayo kwamba imeandikwa humu haikufanyiwa yale matengenezo Skuli ya Kwale niseme iko hali mbaya kuna mabanda pale vyumba kama vitatu na ofisi ya walimu, ofisi hiyo hiyo ni ya mwalimu mkuu pamoja na walimu wasidizi wa mwalimu mkuu.

Lakini ofisi ile Mhe. Mwenyekiti, au mabanda yale hata mbuzi ukimfunga mule hakai kwasababu yako hali mbaya kuna vyumba vitatu pamoja na ofisi ya walimu *staff* ndio mimi sasa hivi nimejitolea kupitia mfuko wa Jimbo Shs.

9,000,000 nimezipeleka pale na Shs. 500,000 nimetoa mimi ili kuhakikisha wanafunzi wanaokwenda *form I* na *form, II* na *form IV* na *form III* wapate kukaa pale, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ilikuwa ni usumbufu wanafunzi wa *form II, form I* na *form III* na *form IV* hawana pa kukaa.

Kwa hivyo sasa hivi nadhani na Afisa Mdhamini atakuwa hilo suala keshaambiwa taarifa hizo anayo kwamba mabanda yale ya Skuli ya Kwale yalikuwa hayako kwenye matengenezo sasa hivi tayari nimeshayafanyia hivyo, lakini naiomba wizara kwenye bajeti hii wahakikishe yale mabanda mabovu yalokuwepo pale Skuli ya Kwale ambayo ni ya tangu kadimeni maana nikisema kadimeni ni tangu mimi sijazaliwa sijui mwaka wa ngapi sijui waliosoma mababu zetu na mabibi zetu, waweze kuyaondoa pale kama kutakuwa hakuna matayarisho ya ujenzi basi japo kuyaondoa. Kwa sababu ni hatari kwa vijana wetu wanafunzi wetu walioko pale na hakuna asiyejua mtoto ile ni kazi kubwa kwa sababu watoto kama unavyoona hawasikii na lakini jengo lile ni bovu wanapita pale na wanacheza mule. Kwa hivyo nawaomba Wizara wahakikishe kwamba majengo yale wanayaondoa ili kuweka usalama.

Mhe. Mwenyekili, lakini pia vile vile niende kwenye masuala ya vyoo Mhe. Mwenyekiti kwenye hotuba hii imeandikwa kuna vyoo baadhi ya maskuli vimefanyiwa matengenezo na ukarabati.

Mhe. Mwenyekiti, nithubutu kusema kwamba katika masula ya vyoo maskulini mengi hususan maskuli ya shamba ni mtihani kila siku hapa tunapiga kelele kuhusu maswala ya udhalilishaji na ubakaji, leo Mhe. Mwenyekiti, unamkuta mwanafuzi anakwenda chooni vichakani kwenda kujisaidia akifika atafanya nini si atabakwa tuu kule, wabakaji wako wamsubiri. Sasa sisi tutakuwa tunapiga kelele humu ubakaji, ubakaji lakini skuli maskuli mengi hususan maskuli ya shamba vyoo mitihani hawana vyoo na kama vyoo vipo maji hawapati, tunawajengea mazingira magumu wanafunzi kusema la ukweli mtihani mkubwa. Sasa leo mwanafunzi anatoka pale anakwenda vichakani kwenda kujisaidia akifika kule vidume wako wanamsubuiri wanambaka keshokutwa twapiga kelele ubakaji, namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie sana ili ahakikishe kwamba maskulini maji yanapatikana lakini pia vile vile na vyoo pia vinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, jana hapa katika kuchangia waheshimiwa walisema kuhusu walimu wana kazi kubwa ni kweli na mimi nakubali hilo kwa sababu kumtoa mwanafunzi kuanzia *nursery* mpaka akafika *professor* ni kazi kubwa ya kuelimisha lakini Mhe. Mwenyekiti nithubutu kusema kwamba kuna baadhi ya maskuli siasa tu ndiyo inayokwenda mbele. Wanafunzi wakifika pale

wanapigwa siasa mpaka wale walimu wenyewe baadhi ya maskuli mengine na ushahidi huo ninao, iko baadhi ya skuli kama ya Jimbo langu la Ziwani, walimu wakifika wao kazi yao ni kuzungumza siasa maofisini mpaka watakwenda majumbani kwao, wanafunzi kuwa waliokusudia walimu hawaendi kulifanya, maana lengo ni kuwasomesha sio uende pale ukazungumza siasa nani atapewa nani hapewi.

Kwa hivyo nawaomba walimu kwamba siasa waiache nyumbani wakenda kazini wafanye kazi kwa mujibu kama walivyokubali kwa sababu Serikali inahakikisha kwamba wanalipwa mishahara yao, sasa leo kama hawataki kumsomesha ana hiyari kuabudi siasa basi aende akafunguwe tawi lake la chama akae kule awe katibu wa chama, ajulikane huyu ni katibu wa chama. Lakini kule maskulini sio akaabudu siasa wakati wa siasa asubiri akifika huko kwake akazungumze siasa na wenzake, kwa hivyo naomba sana suala hili liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya hapo niende kwenye ukurasa wa 40, ukurasa wa 40 hapa umesema kwamba Programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Elimu Pemba 2016/2017 walisema kwamba wameipatia bilioni 20,766,931,000 lakini mara hii huku kwenye bajeti hii hii wamesema kwamba Wizara ya Elimu Pemba wameitengea Shs. 4,046,861,000. Kwa hivyo hapa kwa nini kuna nini hata ikabidi kwamba mara ile wakapewa kiwango kikubwa mara hii wakapunguziwa kule Pemba na changamoto ni hizo changamoto ziko nyingi hakuna asiyeziona na nimezungumza kuhusu masuala ya vyoo maskuli yote hayana vyoo. Kwa hivyo pesa hii ni kidogo haiwezi kufanya kitu hata ukitizama ghala lile la kuwekea vitabu kule Pemba la Wizara ya Elimu kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, mtihani ukienda mule hujui kitabu cha *chemistry* ni kipi, hujui cha *biology* ukipate wapi wewe unaona balaa tu vitabu vimebebana hujui uvipate wapi alimradi kusema la ukweli mtihani.

Lakini vile vile nilimzungumzia Mhe. Naibu Waziri nikamwambia vipi kuhusu lile ghala la elimu kule Pemba wale wanaokaa mule kwenye ghala wakaa kama kuku yaani hata maji, choo nao pia hawana. Kule skulini hakuna basi mpaka maafisa wanaoshughulikia lile ghala la Wizara ya Elimu Pemba hawana mpaka vile vyoo hawana, watoke waende msikitii wa Ijumaa pale Chanjaani ndio wapate kwenda vyooni mtihani kwa hivyo nawaomba kwamba hili fungu kidogo wawaangalie kwamba mara ile waliwapa pesa nyingi lakini mara hii wanawapunguzia kulikoni na kazi kubwa. Kwa hivyo mimi nawaomba Mhe. Waziri wa Elimu aliangalie hili pamoja na Waziri wa Fedha ili kuwawezesha hawa kwamba Pemba waweze kufanya kazi vizuri kwa uzaidi.

Mheshimiwa, vile vile niende kwenye suala la madawati mimi nikitaka nijue tu kwa sababu tulichanga hapa kuhusu masuala ya madawati na suala la madawati sasa ni tatizo Mhe. Nadir jana alisema hapa kuna wanafunzi bora wapewe mabusati, mimi sisemi wapewe mabusati, lakini nasema hivi kwamba Mhe. Waziri aje anambie yake masuala ya madawati yamefikia hatua gani tunataka tujue. Lile suala la madawati anambie limefikia hatua ipi kwasababu tumechanga madawati na wahisani wako wameshatoa michango yao kwa hivyo mimi naomba nijue suala la madawati limefikia hatua gani.

Lakini pia vile vile niende kwenye suala la Skuli ya Ndagoni Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka hapa niliuliza siku nyingi masula kuhusu suala la Skuli ya Ndagoni kutokana na kwamba ile Skuli ya Ndagoni haijapata hati mpaka leo hii kutokana na mzozo uliokuwepo pale lakini Mhe. Naibu Waziri kuna siku moja nikamuuliza masuala hapa akanambia ataunda kamati na ni kweli kamati ile aliunda niliishuhudia mimi mwenyewe sasa nikitaka nijue ile kamati imefikia hatua gani, ili ile skuli nayo iondokane na ule mzozo na kupata hati yake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la uajiri wa walimu ukurusa wa 41 hapa anasema kuwaajiri wafanyakazi 700 wakiwemo walimu 258.

Mhe. Mwenyekiti, suala la walimu naona hapa wamepungua mara ile walisema walimu 400 mara hii 258 kwa hiyo nataka niulize hawa walimu watakuwa washatosha kwasababu naona changamoto ya walimu kila siku ipo, changamoto la walimu kila siku ipo leo kuna wanafunzi wa *nursery* wale wale walimu wanasomesha madarasa mengine wakasomeshe na *nursery* ninakwenda sehemu skuli nyengine hazina walimu wa kutosha, mwalimu ana kipindi kile kipindi hapati kusomesha vizuri akasomeshe na *nursery* haiwezekani. Kuna vijana pale wanajitolea sasa ile ile pesa anayopata mwalimu ndio anayopewa yule kijana aliyekwenda kujitolea pale mwalimu anatoa pesa yake mfukoni.

Sasa michango hii haiwezi kuondoka na mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani kuna watu washanijia na risiti zafika nne kama tano sita hivi, wananambia Skuli ya Wesha na Skuli nyengine wanadaiwa michango tena kupitia *nursery* nikawaambia ni kweli lazima mdaiwe kwa sababu mwalimu hawezi kusomesha vipindi vyake alivyonavyo akenda kusomesha darasa la kwanza, la pili, la tatu na la nne, halafu akatoka akasomeshe na *nursery* muda huo huo haiwezekani. Kwa hivyo naomba hapa Mheshimiwa suala hili la walimu waliangalie ikiwezekana kama hawawezi kuajiri wale walimu wa kusomesha *nursery* basi wawaongeze hao walimu wanaotaka wenyewe lakini *nursery* iwe na walimu wake sio kwa sababu walimu wale wale walioko pale

itakuwa ni tabu kwamba wale wakasomeshe huku na huku ni mtihani. Vipindi vitakuwa havitoshi na wale wanafunzi walioko kule watakuwa hawapati kufahamu vizuri kwa sababu mwalimu atasomesha kwa kuripua tu ataripua pale siku nyengine atawaambia andikeni hapo hafahamishi chochote, anakimbilia akasomeshe *nursery*. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri na hili nalo aliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi wenzangu wengi washasema na maneno ni hayo hayo lakini naomba Mhe. Waziri hayo niliyowaambia wayafanyie kazi wayachukuwe na wanipe majibu kama nilivyokusudia mimi mwenyewe na nadhani Mhe. Mwenyekiti niunge mkono hoja kwa asilimia thamanini, ishirini nazibakisha Mhe. Waziri aweze kunijibu masuala nilouliza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali wa Jimbo la Ziwani kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Tatu Mohamed Ussi wa Viti Maalumu akifuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya na Mhe. Mohamed Said Dimwa ajitayarishe.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii lakini kabla ya kuchangia kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uhai na uzima nikaweza kusimama hapa ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, mimi michango wangu hautokuwa mkubwa kwa sababu ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati hii ya Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wa Elimu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu lakini pia nisimsahau Afisa Mdhamini kule Pemba wa Wizara hii ya Elimu, kwa juhudi zao wanazochukua katika kusukuma gurudumu hili la maendeleo ya elimu, lakini pia niwapongeze kwa mashirikiano yao waliyotupa tukiwa katika kamati ili tukaweza kufanikisha shughuli zetu za kamati.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja mchango wangu unakuja au ushauri wangu unakuja wakati tulipokuwa tunatembelea kamati tuliona changamoto nyingi katika maskuli lakini miongoni mwa changanmoto hizo ni moja ambayo skuli zetu zina matatizo ya hati miliki, maeneo yale ya maskuli lakini pia uzio katika maskuli.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya tatizo lililojitokeza katika Chuo cha Amali kule Vitongoji kwenye bweni la wanawake ni kwamba wanawake wale kwenye

bweni lao wanakuwa wanapata matatizo kutokana kuingiliwa na vijana ambao wanawafanyia kero. Sasa hili lote Mwenyekiti, linatokana zile skuli hazina uzio sasa naishauri Wizara kuliangalia vizuri au kuliangalia tena na kuweza kutafuta mbinu na namna kuzitafutia hizi skuli zetu au kuzijengea uzio pale hali itakaporuhusu.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nishauri sasa hivi kumekuwa na changamoto nyingi za maeneo yetu ya maskuli kuingiliwa na ujenzi wa majumba, nyumba za makaazi sio skuli zote lakini hata wewe Mwenyekiti, au Naibu Waziri na yeye alikuwa ni shahidi tulivyokwenda Skuli ya Uweleni pale tukaona eneo la skuli panajengwa kibanda cha biashara. Lakini vile vile kuna skuli nyengine ni Skuli ya Ng'ombeni Mhe. Mwenyekiti skuli hii kwa sasa lile eneo la skuli lote wananchi wameshajenga maeneo ya nyumba za makaazi, utakwenda skuli utakutia darasa lipo hapo lakini na nyumba ya makaazi ipo hapo wakati eneo lile zamani ilikuwa nyumba zake ziko mbali sana. Sasa mimi nilikuwa naishauri tu Wizara, japokuwa hawajawa na uwezo wa kujenga uzio lakini ningeiomba Wizara ikashirikiana na Wizara ya Mazingira kuyapima yale maeneo ili kujua yale maeneo ya skuli na kuyakinga katika kujenga nyumba za wananchi, hili nilikuwa nashauri.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kulishauri katika mikopo kwanza napongeza Bodi ya Mikopo jinsi ilivyosimamia urejeshaji wa mikopo kwa wale vijana wetu ambao walikopa na baadaye wakajisahau kulipa ile mikopo naipongeza sana. Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu hapa Mhe. Mussa Foum alizungumzia suala zima la utoaji wa mikopo, Idara hii ya Mikopo inatowa mikopo kwa fani ile ya wale ambayo wamesoma masomo ya sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, sayansi tunaihitaji lakini na masomo ya *Art* pia tunahitaji kwa sababu sayansi tunahitaji wataalamu wa sayansi kwamba madaktari, waendesha ndege lakini kuna na maeneo mengine na wao tunahitaji Mheshimiwa katika fani hii nayo tunahitaji hata wasanii, tunahitaji na wengine sasa ina maana mikopo hii ikitolewa wale tunawafanya kuwa wanyonge wanajisikia kama hili somo la *Art* halina maana. Kwa hivyo mimi naishauri tu Wizara waangalie wanafunzi wa sayansi lakini na wanafunzi wa *Art* na wao waangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuishauri Wizara labda Wizara katika programu zake. Mhe. Mwenyekiti, unajua katika madarasa yetu kuna baadhi ya wanafunzi wana mahitaji maalum. Sasa mimi ningeiomba wizara au kuishauri inapopanga programu zake wale walimu wanaokwenda kusomea ule ualimu na sisi labda wangeingiza na somo la wale watu wenye mahitaji

maalum. Kwa sababu mwalimu ambaye hakusomea somo hilo la watu wenye mahitaji maalum basi inakuwa ni vigumu kwa wale watoto wetu ambao wana mahitaji maalum hususan wale wenye ulemavu wa usikivu, lakini na wale wenye ulemavu wa uono mdogo. Mimi nilikuwa naishauri wizara wapange programu hii ili wale walimu wanaokwenda kusoma basi na wao waingiziwe hili somo ili waweze kufaidika na wao watoto wetu wenye mahitaji maalum. Nashauri tu, kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije katika suala la ajira. Suala la ajira wenzangu pia wameshalisema na wamelisema kwa sababu tunayasikia malalamiko humo majimboni mwetu. Sasa mimi ilikuwa nashauri tu, kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina nafasi za uajiri kwa hivyo naomba na mimi wafikiriwe wale vijana wetu ambao wamejitolea kwa muda mrefu, lakini zaidi napendelea na wanawake waangaliwe kwa jicho la huruma. Wanawake ambao wameshajitolea kwa siku nyingi na wao wapate nafasi za kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mengi yameshazungumzwa na ripoti ya kamati yetu ilizungumza na nikatoa michango yangu kwenye kamati, sina mengi isipokuwa naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Tatu Mohamed Ussi kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil akifuatiwa na Mhe. Mohamed Said Dimwa na Mhe. Hamida Abdalla Issa ajitayarishe.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Mimi nitajikita kwenye hotuba hii ukurasa wa 31 kifungu Nam.46, Huduma ya Urajis wa Elimu. Kwanza kabisa napenda kuipongeza sana wizara kwa jinsi ya Mhe. Waziri anavyosimamia programu zake kwa utulivu na uhakika. Lakini shukurani hizi naelekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar programu hii kuipatia fedha asilimia mia moja. Fedha zilizoombwa ni shilingi 35,250,000 na mpaka mwezi wa Aprili, tayari fedha zote za programu hii zimeshaingizwa. Kwa hivyo, hongera sana SMZ kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenyewe.

Hii inaonesha kwamba wizara ina jukumu la kuwasomesha watu wetu ili wawe wanasayansi. Kwa mnasaba huo mimi nauliza Mhe. Waziri, suala la usomeshaji ni suala la kitaifa kwa watu wetu na tukitaka tusitake mzigo wa kuwasomesha ni wa chombo chetu kitukufu serikali, ana mpango gani kuzisaidia skuli binafsi hata kwa asilimia kiduchu kwa lugha ya kishamba, vifaa vya maabara ili watoto wetu wawe wanasayansi na tuingie kwenye Karne

ya 21 tukiwa na watoto walioelimika na wanaweza wakarusha ndege nchi yoyote.

Mimi nije moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Kitengo hiki Bi Siajabu. Huyu ni mwanamama mahiri na makini kusimamia sheria, narejea tena huyu ni mwanamama makini na hodari wa kusimamia sheria bila ya kubabaika. Kwa hivyo basi, bila ya kusema chochote mimi moja kwa moja kwa haya naipongeza sana Wizara ya Elimu na kwa mnasaba huo naunga mkono asilimia mia moja bajeti hii. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mhe. Hamida Abadlla Issa, Mhe. Zulfa Mmaka Omar nakuona kwa hiyo nakuomba uchangie baada ya Mhe. Hamida kwa vile hayupo nakupa nafasi hiyo na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ajitayarishe.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi ya upendeleo ya kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa pongezi, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kututeulia waziri ambaye yuko makini, anafahamu kazi zake, pia anajali utu na umoja katika kufanya kazi kwake. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kutuletea hili jembe linafanya kazi vizuri na sisi tuseme kwamba, kwa hili yuko vizuri sana.

Pia nimpongeze Naibu Waziri wake kwa kufanya kazi zake vizuri kwa sababu tunafahamu kwamba haya wanayoyafanya wanayafahamu zaidi ndipo wakachaguliwa. Tukitoka hapo mimi nije katika mchango wangu, ingawa mengi yameshachangiwa lakini na mimi kuna mambo kidogo nataka niyaseme.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na watoto wa skuli za maandalizi (*nursery*). Mhe. Mwenyekiti, pale tumekuta kwamba sasa hivi kuna mfumo kwamba watoto wale wanakuwa wanapatiwa vyakula wakati wa *reassess* ili na wao waweze kufanya mambo yao. Lakini niiombe sana serikali kuna kipindi pesa zile zilikuwa zinacheleweshwa kupelekwa katika skuli zile. Kwa hivyo, niiombe sana wizara pesa zile zipelekwe kwa wakati, kwa sababu watoto wale pesa zile zinapocheleweshwa wanakuwa wanakosa vyakula katika skuli zile na wazazi tayari wameshajiachia kwamba watoto wao wakienda skuli wanapata chakula. Kwa hivyo, kukosa chakula kwa watoto wale tunaweza kuwasababishia matatizo ya kisaikolojia kidogo katika ufahamu wao. Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri pesa zile zipelekwe kwa tarehe ambayo imewekwa ili kuondoa usumbufu ambao wanaupata watoto wale kipindi ambacho pesa zile zinakuwa zimekwisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nizungumzie suala la wanafunzi wa darasa la sita. Mhe. Waziri nimwambie kwamba sijui sina ufahamu wa kutosha juu ya wanafunzi wale, lakini suala ambalo nataka niliseme sijui niseme kwamba tulifikiria mara ngapi kukatisha lile darasa la saba. Kwa sababu tunaona kwamba wanafunzi wanakwenda *Form I* wakiwa wadogo sana, unamkuta mtoto mdogo yuko *Form I* kule kwetu anavaa fomu weupe kwa weusi hata ile fomu nyeupe hajui jinsi ya kuitunza. Kwa hivyo, mimi naona pale kidogo kimuangalio wangu hili suala halijatulia. Kwa sababu kwanza hofu yangu watoto wale watamaliza skuli wakiwa wadogo na tunaona kwamba ajira ni ngumu sana kwa vijana wetu. Sasa hofu yangu watoto wale kumaliza skuli mapema wasije kujiingiza katika makundi maovu na serikali ikazidi kupata matatizo. Ila naamini kwa ufahamu wake nitamuomba sana anifahamishe Mheshimiwa vipi suala lile ameangalia hasara na faida? Je, wameangalia mbele maisha ya watoto wale yatakuwaje? Kama wameangalia na faida ziko nyingi sana mmi sina tatizo, ila nilikuwa naomba sana suala lile Mhe. Waziri atueleweshe pengie kuna faida na sisi Wajumbe wa Baraza hili tuweze kuzifahamu.

Mheshimiwa nikitoka hapo niende katika suala la madawati. Mheshimiwa tumechangia pesa za madawati na tunaona michango inaendelea kila siku kuhusu madawati lakini kinachonisikitisha kuna skuli nyingi sana ambazo madawati yale hayapo.

Mheshimiwa sisi tuliambiwa kwamba kuna madawati yatagawiwa katika mikoa, lakini niseme kwamba sijui katika ugawaji ule wa madawati wawakilishi hatukuitwa tukajua au vipi. Nisikitike kwamba kuna skuli moja pale ya Madungu kuna wanafunzi wanasoma kuanzia darasa la kwanza hadi la sita lakini skuli ile wanafunzi ambao wanakaa katika madawati ni kama madarasa matatu tu. Kwa kweli Mhe. Waziri hili ni tatizo, ningemuomba sana wakati wa mgao wa madawati yale basi aangalie zile skuli ambazo hazina kabisa kwanza, zile ambazo wanayo japo kidogo wanaweza kustahamili. Lakini sasa tunaona kwamba mwanafunzi wa darasa la sita anakaa chini, au mwanafunzi wa *Form I* anakaa chini kwa kweli Mheshimiwa ni tatizo sana. Kwa hivyo, nimuombe sana katika ugawaji huu wa madawati waangalie na zile skuli ambazo zina hali ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika skuli hiyo hiyo ya Shamiani lakini sekondari. Mheshimiwa pale pana skuli ambayo kuna kuanzia *Form I* hadi *Form VI*. Mheshimiwa pale pana *boarding* lakini ile *boarding* mimi naweza kusema kwamba vigezo vyake kidogo haviko sawa. Kwa sababu *boarding* yao kwa kweli ni mbaya sana, hili sitaki nilizungumze hapa

nitakwenda kwake yeye na kumueleza changamoto ambazo ziko pale kwa watoto wetu wa kike ambazo wanazipata. Kwa hivyo, nitamfuata nitakaa naye tujue ni jinsi gani tunasaidia wanafunzi wale.

Katika skuli hiyo pia wana uhaba wa walimu, tunajua kwamba mwanafunzi akifikia mpaka *Form VI* ana vikwazo vingi na ana masomo mengi. Pale Mheshimiwa kuna mwalimu mmoja tu wa Kiswahili ambaye mwalimu huyo sasa hivi anakaimu Ualimu Mkuu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri afanye jitihada zake za mbio mbio ili kuweza kupeleka mwalimu pale ku-*cover* ile nafasi ambayo inaleta usumbufu kwa wale wanafunzi wetu. Kwa sababu tunajua kwamba wanafunzi tunawapenda na kila ikiwa walimu wanakuwa wengi katika skuli naamini kwamba kupasi kwake pia kunasaidia. Kwa hiyo, juzi wamefanya mitihani ya *Form VI* lakini na kilio hiki bado wanafunzi wale wanacho.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu. Mhe. Waziri nimuombe sana upande wa mikopo, ingawa kwamba na Wizara ya Fedha naweza kusema kwamba suala hili liko huko, lakini nikuombe sana Mheshimiwa uzidi tena kuchakarika juu ya suala hili, kwa kweli wanafunzi wengi sana wanakosa mikopo. Wanafunzi wanarudi nyuma unakuta mwanafunzi ana nia ya kusoma lakini mkopo ule anaukosa wanapata watu kidogo. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba hasa hili fungu la mikopo wanafunzi lizidishwe kwa sababu nahisi bado ni dogo. Kwa hivyo, kama kungelikuwa kuna nafasi nyegine ya kutoa na kupeleka kwa wanafunzi wetu ili wapate mikopo ningeliomba sana, kwa sababu mikopo ni muhimu kwa wananchi wetu kama tunavyojua hali kwa kweli ni ngumu hasa vijijini na watoto tunakuta kwamba vijijini wana muamko wa kusoma, lakini wanashindwa mikopo wanakosa kwa njia moja ama nyengine.

Kwa hivyo, nimuombe sana yeye ni mwanamama na anafahamu vijana vipi wanajituma, hivyo nimuombe sana hili suala la mikopo uliangalie tena, na hao ambao wamesoma hawakulipa tusibakie tu kusema kwamba jamani njooni, njooni tuwafateni maofisini ikiwezekana tuwafungulie kesi Mahkamani hataki kulipa kwa sababu mdaiwa sugu popote anatajwa. Kwa hivyo nimuombe sana hawa wadaiwa sugu watajwe.

Nikitoka hapo nataka niende katika zile skuli za wachina, tunakuta zile skuli za wachina ni muda mchache tu ambao zimejengwa. Lakini sasa kuna kipindi hata sisi Kamati ya *PAC* tulikwenda katika ukaguzi wa skuli zile na tuliiomba wizara yake itueleze jitihada gani ambazo wamezichukua kwa wale ambao wamejenga zile skuli na mpaka leo sikupata majibu sahihi kwamba ni hatua

gani zimechukuliwa. Kwa hivyo, ningemuomba Mheshimiwa atueleze wale ambao wametumia pesa zetu za serikali vibaya kwa kutujengea majengo ambayo hayafai hasa katika yale mabati, ni adhabu gani hawa watu wamepewa na tunajitahidi vipi kutoa *tender* zetu za ujenzi tukiangalia watu muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa sababu mengi sana yameshachangiwa, lakini niendelee kumpongeza Mhe. Waziri anachapa kazi vizuri na aendelee kuchapa kazi na sisi tuko pamoja na yeye. Naunga mkono wizara hii kwa asilimia mia moja bila ya matatizo yoyote na ninawaomba sana Wajumbe wenzangu wizara hii tuipitishe kwa roho kunjufu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka, sasa kabla sijamwita Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Maalim Haroun Ali Suleiman naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Dimwa atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na yeye ajiandae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa imani yako kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza niende na pongezi za pekee niungane na wenzangu wote walioipongeza wizara hii lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye haiba njema. Nimpongeze vile vile Naibu Waziri kwa kuweza kutujibu masuala yetu kwa ufasaha, lakini timu yote ya Katibu Mkuu mpaka kufikia tarishi walifanya kazi kubwa kuwaunga mkono mawaziri hao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niingie kwenye ukurasa wa 19 moja kwa moja kwenye mapitio ya bajeti ambayo yaliyopita. Hapa tumeelezwa jinsi ya wanafunzi waliopata mikopo mwaka 2016/2017, lakini vile vile tukapewa idadi ya waliyoongezeka lakini vile vile tukapewa idadi halisi iliyopo na sasa imepungua sana. Nataka kusema tu, Bodi ya Mikopo inatakiwa sasa iweze kufanya kazi kubwa sana na ninashangaa sasa kuja kwetu kuomba tena pesa, nilifikiria baada ya kuwezeshwa kwa kiwango kikubwa sasa bodi ile itaweza kujitegemea. Hata hivyo, nataka akija Mhe. Waziri aniambie ni wadaiwa sugu gani, wangapi ambao hawajalipa, lakini na hatua gani ambazo zimefikiwa mpaka leo kuweza kuwapata na kurejesha mikopo ile.

Jengine nataka kujua jitihada zinazofanywa kuongeza fungu hili ni jitihada gani, isipokuwa nataka pia nielezwe kwa undani kabisa juu ya suala zima la uandishi wa vitabu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nimesoma sana kitabu hiki cha Kiswahili cha mwanafunzi na nimejaribu kukidadavua kwa upeo wangu mkubwa sana na ninaomba uniruhusu niweze kutoa baadhi ya makosa kwa sababu baadae *paper* hii yote nataka nimkabidhi mwenyewe Mhe. Waziri ili apitishe kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kusoma kitabu hiki cha darasa la pili kuna sentensi ambazo hazikukamilika, kuna sentensi moja inasema: "Mjomba aliuliza kuwa atakuja lini?". Sasa hii sentensi haikukamilika nilivyoona mimi, usahihi zaidi nasema 'Mjomba aliuliza atakuja lini', na hii *paper* nitaitoa ili basi aweze Mhe. Waziri kuidadavua na yeye vyema. Lakini kubwa nilikuwa nataka kujua tu, vitabu hivi waandishi hawa wana-*bid tender* hizi kwa kiwango gani, wangapi wana-*bid tender* hizi za vitabu vya kuandika hivi, lakini kuna mapitio yoyote au kuna Baraza lolote linapitia vitabu hivi? Naviona, kitabu hiki kimeandikwa na Kampuni ya Nyambari Nyangwine. Namkumbuka sana mwandishi huyu nilikuwanaye kwenye Bunge la Kumi anaandika vitabu vingi, lakini nilichokiona kuwa wanafunzi wengi wanapenda kusoma vitabu vyake kwa sababu anawapa majibu kabisa. Sasa Mhe. Waziri aniambie tu kwa mnasaba na huo nikasema leo nakuja na ile dhana ya wale waandishi wa vitabu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa na waandishi wengi sana na wamejipatia sifa Afrika Mashariki lakini hususan na kwengineko duniani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya waandishi hao waliotunga alikuwa ni Mohammed Said Abdalla ambaye alitunga kitabu cha Bwana Msa aliandika vitabu vingi sana na naiomba nivinukuu kwa ruhusa yako. Kimoja aliandika Mwanashungi Hewala, Kosa la Bwana Msa na vitabu vyengine vingi. Lakini nataka nianze kuvitaja ni vingi sana nimeviorodhesha hapa vitabu takriban 47. Nilikuwa nataka niseme tu waandishi hawa tangu alipokaa mwalimu wangu Mwalimu Haroun Ali Suleiman akaja mwalimu Shekhe Abdalla lakini akamalizia na Mhe. Ali Juma Shamhuna pamoja na Mhe. Riziki wamewaita lini kuweza kujua hivi vitabu na waandishi hawa wamewaita hata siku moja.

Lakini cha kushangaza zaidi vitabu hivi kwa wenzetu Bara vinatuka, kwa wenzetu Kenya vinatumika kwa hapa Zanzibar hakuna kinachotumika hata kimoja sio *officially* na wanajitahidi nadhani wameanza ku- *bid* tenda mbali mbali. Sasa nataka Mheshimiwa aje aniambie hawa ni tatizo gani lilokuwepo ikiwa wenzetu Kenya na Bara wanatumia vitabu hivi hapa Zanzibar kuna nini kwa nini kichukuliwe kitabu kama hichi cha Nyambari na Nyangwine *Publishers* kuliko vile vitabu vyetu kuna tatizo gani, kuna tatizo lolote Mhe. Mwenyekiti, wamefanya nini na hawa waandishi ni wengi sana.

Lakini ukisoma historia ya Zanzibar sasa hivi ndani ya mitandao yetu utakuta historia hiyo imeanza kugeuzwa mbali mbali. Lakini kuna waandishi ambao wameandika vitabu mbali mbali Mhe. Mwenyekiti, kuna waandishi wameandika maisha ya bwana nikisema bwana ni Shekhe Abeid Amani Karume wameandika vitabu vingi sana kitabu chake cha kwanza kiliandikwa na Mdungi Ussi mwaka 1965 kabla ya mimi sijazaliwa. Lakini cha pili kiliandikwa na Ronald Mwanjilisi huyu alikuwa Waziri katika Serikali ya Julius Kambarage Nyerere. Lakini kuna kijarida kidogo sana kiliandikwa cha Chama cha Mapinduzi. Nadhani leo nimekuja nayo nimekuja na *full* nondo hapa na chengime maisha haya haya aliandika Ali Shaaban ukiyaona ndio utaona ndio maisha halisi ya Shekhe Karume nimekuja na nondo Mhe. Waziri hapa nina vingi sana nimekuja navyo hapa na hivi vyote ndivyo vinavyoelezea maisha halisi ya bwana Abeid Amani Karume.

Lakini leo ukienda kwenye mitandao utakuta upotoshaji mkubwa sana umetokea pale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohammed Said Mohammed kidogo samahani. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwakumbushe katika Kanuni ya 61 kifungu (i) "Hatazungumza kwa sauti ya juu Mjumbe aliekuweko humu." Kwa hivyo, nawaomba kanuni hii hii muwe pia mnaitumia kutahadharishana humu ndani ya Baraza.

Kwa sababu mtakapozungumza kwa sauti za juu Mheshimiwa anaetoa mchango wake na Waziri anaesikiliza atakuwa hasikii baadae atakuja kukosa yale majibu ya kumjibu mchangiaji au Mwakilishi anaechangia. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa tuisome hii kanuni ili tuwe na utulivu ndani ya Baraza, ahsanteni. Mheshimiwa endelea. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwanza tukushukuru kwa nia moja ya kutukumbusha kanuni zetu ambazo tumejipangia ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Lakini nikiendelea na mchango wangu nimemalizia pale kwenye vitabu na nitawapa nondo ili waende nazo lakini wanijibu tu hawa waandishi wetu wa Zanzibar wamewaita lini na wako wangapi mimi nawajua. Lakini kwa faida ya wananchi wako wangapi, tuna vitabu ambavyo mimi nimeviorodhesha takribani Mhe. Waziri kiasi cha 47 nimeviorodhesha vitabu hivi na vitabu hivyo vinatumika hapa. Nataka mje mniambie.

Lakini jengine niende kwenye maskuli yetu mbali mbali ambayo nimeona Mhe. Waziri kwenye majaduweli yako umeyataja humu zile skuli ambazo hazikuwezekwa pengine hatukupata pesa za kutosha, lakini nilitaka tufanye mkakati wa kudumu. Niwapongeze sana kwa sababu madawati tulienda vizuri sana, sasa tuelekee kwenye kumaliza mabanda yote. Juzi Jumapili ile iliyokuwa na mvua kubwa sana nilienda kufunga mafunzo ya Skauti Kaskazini "B" kwenye Skuli ya Pwani mchangani niliikuta inavuja vibaya sana. Lakini kuna jiwe la msingi ambalo Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wetu wa Baraza la Mapinduzi aliweka jiwe la msingi kwenye chumba ambacho kitakuwa cha mitihani mwaka 2013 kiko katika hali mbaya hakijawahi na nimekiona lakini bahati nzuri umekitia kwenye jaduweli lako.

Unambie ni mikakati gani unafanya sasa kumaliza madarasa haya ili yale madawati yetu waliochangia Waheshimiwa Wawakilishi na wengine yanaweza kwenda kukaa kwa salama, ikiwa hali ile ya kuvuja sana madawati haya yote yatakuwa kazi bure ya Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman na kamati yake kushajihisha kutupatia madawati sana. Lakini tumpongeze sana Mhe. Mwalimu Ali Suleiman Haroun kwa kazi kubwa mimi nasema kila siku kama nitapewa ruhusa au nakuwa napewa ruhusa ya kutoa digirii ya heshima au daktari ya heshima basi Mwalimu Ali Suleiman Haroun ana haki kupewa udaktari wa heshima. Kazi kubwa sana alifanya kwenye elimu. (*Makofi*)

Lakini niende kwenye elimu hii ya maandalizi nimeona fungu lake dogo sana Mhe. Waziri ambalo mmelipangia na nahisi iko haja sasa tuende kwenye kitabu kikubwa kuangalia fungu SK010101 Elimu ya Maandalizi pesa zilizopangiwa ni thalathini na tano milioni laki nane thamanini elfu na kidogo. Lakini Elimu ya Juu huenda sina uhakika lakini tunaweza tukabadilisha. Nataka Waheshimiwa Wawakilishi tuungane mikono juu ya hili. Kwa sababu hatuwezi kujenga nyumba yetu bila ya kuwa na *foundation* imara. Sasa tujenge kwenye *foundation* imara ili tuweze kunyanyua na juu. Mathalani kwa wenzetu wengi wanafunzi wengi wa elimu ya juu wakishakumaliza wanatakiwa warudi kwenye nchi yao lakini hapa tathmini ndogo tuliyoifanya wengi wanakimbia kwa sababu ya ajira hakuna. Sasa watwambie pamoja na kutangaza ajira hizi Mhe. Waziri wa Elimu tathmini ambayo umeifanya.

Tathmini yenyewe iko hivi ni wanafunzi walimu, nikizungumzwa wanafunzi walimu wale waliomaliza wanataka kuajiriwa wangapi katika shule la msingi lakini na shule za Sekondari ni wangapi. Lakini nije tena Mhe. Waziri wale wanafunzi waliomaliza kidato cha sita wakawa wao wanajitolea. Sasa hawa ningekuomba sana Mhe. Waziri uwape kipaumbe katika kuwaajiri na hatimae kuweza kuwapeleka chuoni kupata elimu hasa ya kufundisha.

Jengine Mhe. Waziri nikupongeze sana katika kumdhamini Mhe. Rais wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumpongeze sana kwa kuanza kubuni mbinu imara ya kurudisha michezo maskulini. Lakini niwapongeze Waheshimiwa wote waliochangia pale niwapongeze Timu ya Negro na Rais wao Mhe. Ali Salum Haji timu ya Taifa na Timu ya Jang'ombe Boys ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa niwapongeze sana. Ile ina maana tutaanza kuibua vipaji mbali mbali. Lakini uanze kutwambia sasa ukija Mhe. Waziri ni tathmini gani umeifanya tunaweza tukarudi vipi kwenye vipaji kuinua vipaji vyetu ni walimu wangapi wa michezo maskulini umewatayarisha ili tuone kweli kama umekuwa na programu hii ya hakika sio kupoteza pesa za wavuja jasho. Watu wengi wamehamasika juu ya lile.

Lakini la mwisho kabisa niende kwenye Mfuko wa Madawati. Mfuko wa Madawati sio huu tuliochangia kulikuwa hapa tulipitisha sheria ya kuwa tiketi zile zilipiwe za Bandarini na *Airport* kuna kasma inatoka inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa madawati. Pesa zile unazipata au huzipati na kama huzipati unalijua au hulijui na kama unalijua utwambie ni kiasi gani ambazo unapata na kama hupati usiogope kukiri kama hujui kitu ili basi tukamate fungu tuone tupate *commitment* ya serikali tujue fedha zile za wanyonge, pesa zile za wavuja jasho na kodi ya wananchi inakwenda wapi tulikuwa tunataka kujua.

La mwisho kabisa niende kwenye Bodi ya Mkopo nijue tu kama mwanzo nilivyokwambia nataka kupata nilifanya tathmini ya wale watu wanaodaiwa na tuone basi ni wangapi wadaiwa sugu na mmechukua hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache niseme niwashukuru sana na nataka majibu hayo lakini leo ajabu kubwa naunga mkono asilimia mia (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kutujaalia asubuhi ya leo kuendelea na shughuli yetu muhimu hapa Barazani na kutujaalia afya njema sote tuliokuwemo humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nishukuru sana mimi nimesimama hapa nina mambo kidogo sana sio mengi kwa kiasi tu baadhi ya mambo nikupelekeni kwenye historia kidogo ili tuelewe.

Lakini nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazoendelea kufanya

katika sekta zetu zote za huduma za jamii za kiuchumi na nyenginezo. Zinafanya kazi nzuri pamoja na Makamu wa Pili wa Rais anasaidiana vizuri na sisi Mawaziri wake tunajitahidi kadiri tunavyoweza pamoja na Manaibu na wengineo.

Lakini pia nichukuwe nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Waziri wetu wa Elimu, Naibu Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wote na Watendaji wote pamoja na walimu na wanafunzi wa skuli zetu za Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu eneo hili katika umri wangu wa miaka 63 sasa hivi nimelifanyia kazi kwa zaidi ya miaka 40. Kwa hivyo, natangaza *interest* wajue mimi ni mwalimu *by profession* na ni sekta ambayo kwa kweli nimeifanyia kazi kuliko sekta nyengine yoyote.

Kwa hivyo, na mimi nina haki ndio maana nimesimama hapa kuchangia kidogo halafu mwisho nitakuwa na maombi kwa Mhe. Waziri na mimi niombe kidogo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi.

Lakini pamoja na hayo yote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi wanaunga mkono hotuba hii pamoja na mimi mwenyewe kwa asilimia mia moja na tunamtakia kheri Mhe. Waziri kwa kweli wanajitahidi kufanyakazi nzuri sana katika wizara ana wasaidizi wazuri, Naibu Waziri wake ni mtu makini, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu bahati nzuri watu hawa wanafahamu sana wote na wao wananifahamu. Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia katika eneo moja twende kwenye historia kidogo. Baadhi ya Wajumbe wamezungumzia suala zima la Sera ya Elimu iangaliwe. Mimi nakubaliana nao kwamba inaweza ikaangaliwa si vibaya kwa sababu sera yetu ya mwazo Wizara ya Elimu ilikuwa 1991 wakati inaandaliwa sera ile ya mwaka 1991 mimi nilikuwa mwalimu Mkuu wa Skuli ya Sekondari ya Haile Selassie nikaenda Wizarani nikapata uteuzi wa kuwa Naibu Mkurugenzi mwaka 1992. Sera ile ikaanza kutumika toka wakati ule hadi mwaka 2006 ikatoka sera nyengine. Ilipotoka sera nyengine mimi tayari nimeshakuwa waziri wa Elimu mwaka 2006 na sera hii uimepitiwa na wahusika mbali mbali washirika mbali mbali wa maendeleo waliangalia na wakatoa mchango.

Sasa limekuja suala la watoto wetu wanaomaliza skuli darasa wa sita ni wadogo. Lazima niseme tuelewe kwanza wale darasa la sita sio kwamba wanamaliza kwa sababu wale watoto wanaendelea na kusoma wanaingia *form*

1 form II form III na kuendelea kadiri inatakavyowezekana uwezo wao wa kusoma humo mbele.

Niipongeze wizara kwa kuanzisha utaratibu, ulikuwepo utaratibu huo lakini umeendelea tena kuna kipindi fulani uliondoka lakini sasa hivi umerudi tena kwa kufanya mitihani darasa la nne na la sita. Lakini kwa nini imekuja hii Sera ya 2,6,4 yaani miaka miwili ya maandalizi ni ya lazima na miaka 6 ya *Primary* ni ya lazima na miaka 4 ya Sekondari ndio sera mpya inavyotuelekeza. Lakini kwa wakati huu tumeweza kufika darasa la sita na watoto wamepelekwa *Form I* kwa nini ilifanyika hivyo.

Lakini tukumbuke huko nyuma historia inasemaje, mimi nimeingia skuli 1961 wengi hawajazaliwa humu ndani nina hakika kama wapo ni wachache sana 1961. Sisi tukamaliza darasa 8 ndio wa mwisho kwa mwaka 1969 baadae likaendelea darasa la 7 ndio mwisho na siku ile tulifanya mtihani 1969 mwezi Oktoba darasa la nane walifanya mtihani huo na darasa la saba wakafanya mtihani huo huo kama mwaka huu uliomalizika walifanya darasa la sita na la saba ndio hao hao waliofanya mtihani.

Kwa hivyo, ni masuala ya kawaida hutokezea na mfumo huu si mpya hapa duniani nchi nyingi kuna nchi sisi tunaita darasa la kwanza, la pili la tatu wengine wanaita *grade I, grade II* lakini wengine wakifikia *grade V* katika baadhi ya nchi duniani wanaingia *grade VI* na pengine grade *VI* ndio mwaka wa mwanzo wa elimu ya sekondari inategemea mfumo wa nchi yenyewe ulivyo. Kwa hivyo, si jambo jipya sasa mfumo huu ndio kwanza umenza kutumika yaani wale darasa la sita wameingia kidato cha kwanza hakuna alierejeshwa nyumbani kwa sababu taratibu haziruhusu. Elimu ya lazima ni miaka 12 lazima tuitimize hiyo.

Sasa nawashauri Waheshimiwa tusije kufanya maamuzi haraka sera ile ilitengenezwa na watu waliobobea Mwenyekiti wake alikuwa Mhe. Dr Mohammedd Gharib Bilal msaidizi wake alikuwepo Mhe. Ali Juma Shamhuna ambaye baadae alikuwa Waziri wa Elimu, alikuwepo wakati ule Mhe. Juma Duni alikuwepo Dr. Bishara Thenian, alikuwepo Dr. Hemed Rashid Hikman, Dr. Said Gharib na maprofesa wengine na ilifanyiwa utafiti dunia nzima karibu walitembea na kwenda kutafuta utafiti juu ya suala je, tunaweza kwenda kwenye mfumo huu na hatimaye likaja pendekezo lile ambalo limeleta *system* ya *Nursery School* miaka 2, *Primary School* miaka 6 na Sekondari miaka 4.

Sasa inawezekana pengine ikatokea matatizo mawili matatu katika utekelezaji na suala la msingi ni kwamba je, walimu wetu wako tayari kwa mfumo huu? Je

wameandaliwa vizuri? Sasa jukumu lilikuwa ni letu wenyewe sote kwa sababu kama mtoto atapitia maandalizi miaka miwili, kama atapitia *primary school* miaka sita vizuri kwa sababu tatizo la kufanya watoto wetu wamalize skuli mapema hili linawasaidia wanapata digirii bado vijana. Leo unaanza digirii ya kwanza umeshakuwa mtu mzima haipendezi kama mimi nimemaliza digirii sasa hivi ya kwanza ndio naingia utamalizika kabla ya wakati wako.

Kwa hivyo, unaingia skuli tumesema una miaka mitatu, tuseme ya *Nursery School* miaka 2 , miaka mitano unaanza darasa la kwanza, miaka sita au miaka saba utasoma itakuwa miaka kumi na tatu, ukifika sekondari miaka minne unapata miaka kumi na saba unakwenda miaka miwili ya kidato cha tano na sita, unafika umri miaka kumi na tisa, ukiingia Chuo Kikuu mpaka ukamaliza miaka mitatu utakuwa na umri wa miaka ishirini na mbili. Sasa tujiulize miaka ishirini na mbili unasoma digirii ya kwanza sawa unakuwa kijana mzuri. Lakini kama utaingia na miaka ishirini na tano umeshakuwa mtu mzima, ukitaka ufike mpaka darasa la saba, la nane miaka ni mingi, imepunguzwa na wataalamu wakati huo wakashauri kwamba bora iwe ni hivyo.

Lakini tunayo haki wakati wowote kuiangalia tena sera yetu kama tukihisi ina hitilafu au ina matatizo. Lakini mimi naona tusije kufanya maamuzi ya haraka tunahitajia kujipa muda kidogo tuendelee na uzuri wenyewe kwamba wale watoto, kwa sababu imejengeka dhana hapa na dhana iliyojengeka wale watoto wale wakishamaliza darasa la sita Mhe. Mwenyekiti, kwamba ndio wamemaliza, hawajamaliza wale bado wanalazimika kuendelea na skuli mpaka darasa la kumi wanafanya mitihani na mitihani imewekwa darasa la nne, darasa la sita, darasa la kumi makusudi kwa lengo la kuwapima kila hatua wanayofika ili waweze kupimwa vizuri. Kwa hivyo, tusiwe na wasiwasi jambo ambalo jipya litachukuwa muda kidogo kueleweka na tusitie mashaka yoyote Mhe. Mwenyekiti.

La pili nataka nizungumze kidogo ambalo limejitokeza hapa vile vile kuhusu marekebisho ya mishahara ya kiutumishi, imezungumzwa baadhi ya walimu wanadai mambo yao hayakwenda vizuri.

Katika kipindi ambacho Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inaongozwa na Dk. Ali Mohammed Shein, imefanya marekebisho ya mishahara mara nne, jambo ambalo halijawahi kufanyika huko nyuma vipindi vinne mfululizo. Mimi ni shahidi nipo kwenye serikali hii *Alhamdulillah* tokea tumeingia mwaka 2010 mpaka leo mwaka 2017 nipo namshukuru Mwenyezi Mungu. Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie

tumalize salama na baadae hapo tunamuomba Mwenyezi Mungu tuendelee In shaa Allah.

Mhe. Mwenyekiti, sasa jambo la msingi ni nini. La msingi kwamba hebu tukumbuke tunakotoka marekebisho ya mishahara yaliyofanywa yote haya kwa miaka mingapi hayajafanyika. Serikali imefanya marekebisho, tumeshiriki vizuri kikamilifu na serikali ikatoa maamuzi ya marekebisho, hata walimu wakapewa maposho maalum kwa ajili ya kutengeneza mazingira mazuri ya walimu. Tumerekebisha kama kuna kasoro mbili au tatu basi mimi natoa wito waheshimiwa msije mka-*hesitate* yaani mkachelea kutuletea, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sisi utumishi tutakuwa tayari kuyapokea marekebisho hayo na tuweze kuyachukulia hatua zinazofaa, tusiwe na mashaka hatutomnyima mtu haki yake.

Kwa walimu kwa mfano, tumeangalia nini. Kuna kipindi tuliangalia walimu wale wa miaka mingi wamesomesha miaka 15, miaka 20 tulihesabu miaka yao na uzoefu wao yaani waliofanyakazi katika sekta ile ya ualimu, ilihesabiwa na kupewa nyongeza zao kwa mujibu wa utaratibu ule. Kilichojitokeza sasa baadae, baada ya walimu wale kuwarekebishia mishahara wa *certificate* wa miaka mingi, wakaonekana wengine wamewapita hata walimu wenye *diploma* yalipofanywa marekebisho. Sasa na hili pia tumeshaliangalia na katika utaratibu huu mpya tumelizingatia na hilo na tume- *accommodate* mambo yote hayo. Kwa hivyo walimu *Alhamdulillah* mambo yao sio mabaya tushukuru na tumpongeze sana Mhe. Rais kwa uamuzi wake huu na tuendelee kumuunga mkono katika juhudi zake mbali mbali za kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, sio walimu tu, maeneo mengi wamefaidika kama masheha na vikosi vyetu kama mlivyozungumza wenyewe humu ndani na maeneo mengine. Lakini pia kuna maamuzi makubwa aliyatoa mazito. Ni kweli ni sera yetu, lakini ilikuwa kwa kipindi fulani tulikuwa tunasema watu waendelee kuchangia elimu, elimu ya msingi katangaza kwamba itakuwa bila ya malipo tunampongeza sana. *(Makofi)*

Vile vile alisema hadharani kwamba elimu ya Sekondari mitihani yote itakuwa inalipiwa na serikali, na hali itakaporuhusu basi hata hiyo elimu ya Sekondari nayo itakuwa mahali pake, itapewa mahali pake kwamba wasome bila ya matatizo. Sasa madamu mwenyewe Mhe. Rais kalisema hili, mimi nina imani kwa sababu ni mtu mkweli muadilifu hana wasiwasi na hilo atalitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie jambo moja ambalo lilielezwa hapa. Kifungu cha kanuni cha 37(3)(1)(2) cha kanuni yetu kinasema hivi; Jambo likishatolewa

ufafanuzi maelezo sio vyema kulirejea rejea tena. Limezungumzwa hapa na mimi nataka nieleze nyumba ile iliyoelezwa na Mheshimiwa wetu mmoja hapa, alitaka kujua nyumba ile ni ya nani, mwenyewe nani, ni ya serikali au ni ya nani. Sasa ni bora tulitolee ufafanuzi leo tulimalize, japokuwa kanuni inakataza Mhe. Mwenyekiti, lisizungumzwe tena, lakini sasa Mhe. Mjumbe kalizungumza na kama hatojibiwa ataona kwamba labda hajaridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hilo suala lina suala unalotaka kulizungumzia lina mahusiano na hii hotuba iliyozungumzwa hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Enhee. Tunakuja Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ni suala la mafunzo ya amali na mafunzo ya amali yamezungumzwa na hiki kituo ni cha mafunzo ya amali, kwa hivyo ni mahala pake hapa kulizungumza na kulitolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa sababu nakumbuka jana alizungumza kuhusiana na

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Halina matatizo Mhe. Mwenyekiti, ni kutoa ufafanuzi, kwa sababu watu waelewe tu mafunzo ya amali yenyewe yako vipi na imekusudiwa nini, ni bora kufahamu kuliko kila siku kuliuliza jambo kama hili na jambo ambalo sio zuri na linaleta mashaka makubwa. Kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo uliache japokuwa linakuhusu au ulitolee maelezo kwa mujibu wa kanuni hiyo. Kwa sababu nakumbuka uliwahi kulijibia na umesema kanuni ya 37 hatuhitaji kurejearejea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Nilisema mapema kanuni inakataza. Madamu kanuni inakataza hofu niliyokuwanayo Mhe. Mwenyekiti, ili tusije tukamsumbua waziri wetu kwa sababu hili jambo limeulizwa. Hofu iliyokuwepo asije akasumbuliwa waziri, mimi sina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Haya endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Naam.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Haya. Kwa sababu ni jambo zuri tulielewe sote kwamba asiulizwe waziri akaja akasumbuliwa. Mimi sitofurahi kuona waziri anasumbuliwa kwa jambo ambalo limeshatolewa maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kunifahamu na naomba nitowe ufafanuzi. Nyumba iliyokuweko Makunduchi Kigaeni mimi ndio Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi. Lakini Mwenyezi Mungu kanijaalia ni waziri hivi sasa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, Nyumba ile ilikuwa inamilikiwa na Shirika la Utalii miaka mingi sana ya kihistoria, baadae nyumba ile ikaanza kuharibika, nikamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye kwa bahati nzuri yupo Barazani, mheshimiwa hebu twende tukaiangalie ile nyumba inaumia, inaharibika na nimepata taarifa kwamba nyumba ile inataka kuuzwa, wanataka kuuziwa watu binafsi au kuna watu wanaiomba nyumba hii, naona bora itumike kwa shughuli za kimaendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Makamu wa Pili akaja akakagua na akawaita watu wa utalii, mbele yetu pale wakaulizwa Je, mnayo nia ya kuitengeneza nyumba hii. Wakasema ndio tutaitengeneza. Basi Mhe. Makamu wa Pili akasema basi nikupeni muda gani, wakaomba miezi mitatu, yeye akawapa miezi sita. Nashukuru sana miezi sita imemalizika nyumba haikutengenezwa ikawa inazidi kuteketea.

Mhe. Mwenyekiti, kuna shirika hii linaanzia na *CAAA* ukiniambia tafsiri yake kwa urefu neno la Kifaransa silijui. Lakini ni shirika hili ambalo lilisaidia ujenzi wa skuli ya Maandalizi Ndijani. Wale wananchi wa Wilaya ya Kati wanaijua skuli ya *Ndijani Nursery School* waliijenga wao. Lakini pia walijenga na ukumbi mkubwa sana wa kisasa kule Ndijani, na mimi wakati huo nilikuwa waziri wa elimu, wakatuomba wakatuambia hebu tutafutieni mahali tuweze kujenga skuli ambayo itawasaidia kuwajenga vijana wetu katika mafunzo ya amali waweze kupata ajira. Basi nikafikiria kwamba tuwapeleke Chwaka, lakini Chwaka nyumba zile ikawa Wizara ya Fedha na Mipango inazihitajia kwa ajili ya Chuo chao cha pale.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba nyengine ni hiyo ya Makunduchi ambayo inaumia. Tuka-*process* ikafika hatua nyumba akenda Makamu wa Pili baadae Mhe. Makamu akatushauri nipeleke zaidi mbele serikalini. Nikiwa kama waziri wa kazi wakati ule na utumishi, mimi nikasema hili litatusaidia kuongeza ajira kwa

vijana wetu wa Kusini kule, kwa sababu ni ukanda wa kiutalii kuna hoteli nyingi kule. Nyumba ile nikapeleka maombi serikalini na hatimaye Wizara ya Fedha ndio ambao wenye mitaji ya umma wakapewa nyumba ile ikarejeshwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha wakaandikiwa barua watukabidhi Wizara ya Kazi, sio Maalim Haroun. Waikabidhi Wizara ya Kazi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za vijana katika mambo ya ajira, hasa katika mambo ya utalii na yanayohusiana nayo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nyumba imepatikana na wakatiliana makubaliano kati ya serikali na wao shirika hili wakatia saini makubaliano. Hivi karibuni kwa sababu tayari mimi sio dhamana tena wa mambo ya kazi. Mimi sasa hivi ni Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini haya mambo ya mafunzo ya amali yana mahali pake ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Tukafanya kikao cha pamoja kati yangu mimi, wizara ilikuwa ina dhamana ya jengo hili na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na waziri mwenyewe nashukuru alihudhuria na watendaji wake wote walikuwepo, pamoja na watu wa mafunzo ya amali, wakaambiwa wafuate taratibu zote.

Mhe. Mwenyekiti, mkataba unasema kwamba nyumba ile ni mali ya serikali endapo wataamua kurejesha. Kwanza hawatoruhusiwa kumpa mtu mwengine yeyote ni mali ya serikali sio ya mtu binafsi wa kumiliki, ni jambo ambalo sote tulikuwa hatuelewani kwamba nyumba ile ni mali ya serikali. Kitakachojengwa pale cha nyongeza chochote watakapoamua kuondoka basi itakuwa ni mali ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hebu tumuombe Mwenyekiti wa Kamati ile ya Ustawi wa Jamii Dk. Mwinyihaji Makame na kamati yake wende wakaikaguwe ile nyumba, ile nyumba ambayo imefungua milango mikubwa sana kimaendeleo. Kwanza katika ujenzi wake zaidi ya ajira 40 zimepatikana, vifaa vya ujenzi vyote vile vimenunuliwa katika maduka ya kule kule, tumewawezesha wananchi wetu kuondoa umaskini vile vile. Watakaosoma pale pamoja na hao ndugu zetu ambao tunalalamika leo hapa kwamba nyumba ile anayo nani na nani. Ndugu zetu watasoma pale pale na watoto wetu, tunatarajia *In shaa Allah* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanaendelea na utaratibu wa kuwaandalia utaratibu wa kufunguliwa rasmi nyumba ile itakapokuwa wakati wake muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nimehisi niliseme hili kwa sababu lisije likarejea tena na kanuni zetu zitatukataza hata kurejea. Limeshatolewa ufafanuzi mara ya

kwanza, mara ya pili na hii ni mara ya tatu. Nakushukuru kwamba umeniruhusu nimelisema hili vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho namuomba Mhe. Waziri na mimi anifikirie mambo mawili. Najua waziri huyu ni msikivu sana, naibu wake ni msikivu zaidi. Kuna sana na zaidi, kwa sababu kwa kazi za haraka haraka anatumwa naibu waziri, zile zinazohitajia *policy* na mambo mengine waziri mwenyewe anasimamia, lakini wote ni watu makini. Chuo kinajengwa kule cha Mafunzo ya Amali Makunduchi Kisonge, sio hiki nilichokizungumza ni chengine ambacho kina msaada wa *African Development Bank*, kilisimama muda mrefu. Nilipata habari huyo *Consultant* huyo huyo ndio yule ambaye alikwamisha ujenzi wa kule Daya ikiwa ni sahihi. Naomba sana tulitatuwe tatizo hili ili kile chuo kile nacho kimalizike, naomba sana. *(Makofi)*

Lakini la pili namuomba waziri hii skuli imekaa miaka mingi, kuna skuli ilikuwa ya Sekondari sasa hivi ya msingi ya Miwaleni. Namuomba sana Mhe. Waziri afanye kila njia, basi skuli hii nayo ipewe kipaumbele katika miaka inayokuja ya bajeti, angalau ikifika miaka ya 2020 skuli ile iwe tayari.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho skuli yetu ya Kibuteni ambayo naomba sana ni ya muda mrefu nayo imekwama, naomba sana ule mkandarasi ambaye sasa hivi nimepata taarifa kwamba mkataba wake umeshakatika, basi apewe mwengine afanyekazi ya ujenzi na sasa hivi kuna ma-canch yamewekwa kule juu yanaharibika na mvua hizi sijui kama yatakuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana naunga mkono tena hoja hii, niwatakie kila la heri. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tumuunge mkono waziri wetu ili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iweze kutekeleza majukumu yake vizuri, kila la heri ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri Maalim Haroun kwa mchango wako na ushauri wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, akifuatiwa na Mhe. Said Soud Said waziri asiyekuwa na wizara maalum. Mwisho kabisa kama muda utatosha nitampa nafasi hii Mhe. Maudline Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha hapa sasa tukiwa na afya njema.

Lakini pia niendelee kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kazi kubwa anayoifanya na juhudi zake katika sekta hii ya kuimarisha elimu. Sote tumekuwa ni mashuhuda kiongozi wetu huyu anapigana hapa na pale kuhakikisha kwamba watoto wetu wote wanakwenda shule, lakini kila Mzanzibari anapata haki ya msingi ya kupata elimu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo pia naomba niwashukuru sana watu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, akiwemo mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, watendaji wake, lakini pamoja na walimu wote wanaosomesha katika skuli zote, kuanzia maandalizi, msingi, sekondari na vyuo, kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari sisi tunapata elimu ya kutosha na tunakuwa katika hali ya usomi wa kawaida. Ninazungumzia hili kwa sababu elimu tunasoma, lakini elimu ni afya, elimu ni michezo, elimu ni kila kitu, bila ya elimu katika maisha haya hakuna kitu ambacho kinaweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kusema kwamba nawapongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi ya makusudi walioichukua. Nasema kwa juhudi ya makusudi waliyoichukua ya kuanzisha madarasa ya *science subject* kwa watoto wa kike. Watoto wa kike wengi walikuwa wanakwenda kwenye masomo ya *art* kwa sababu ya urahisi na unafuu wa kusoma. Lakini wamefanya bidii kubwa, wamefanya maandalizi mazuri na leo watoto wale wamekuwa watoto wa sayansi. Kwa kweli hii ni kazi kubwa wameifanya niwapongeze kwa hilo na *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu walimu wale na wizara hii ndio atawalipa hakuna mwengine wa kuwalipa.

Jengine ambalo naweza kulizungumzia katika sekta hii Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye sehemu ya mikopo. Wanafunzi wetu wengi sasa hivi wanapata mikopo kuliko ile idadi ambayo tulikuwa mwanzo tukiifikiria, lakini maana yake nini mikopo inatolewa mingi. Maana yake watu wamehamasika na kusoma, watoto wote vijana wamekuwa wanajua umuhimu wa elimu tofauti na kile kipindi ambacho elimu mtu anaona ni jambo la kawaida. Lakini sasa hivi kila mtu amehamasika na anajua umuhimu wa elimu kwa hivyo kila mtu anataka mkopo ili aende chuo na asome. Pia wazazi wamehamasika kwa asilimia kubwa, kwa hivyo wamechukua juhudi kubwa ya kuhakikisha kazi hii inafanyika.

Vile vile niende kwenye suala jengine ambalo nataka kuliongelea ni suala la umiliki wa maskuli ambayo tunayo hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya

Elimu na Mafunzo ya Amali, tumekuwa na mkakati maalum sasa hivi wa kuamua kuyapima maskuli yote na kuhakikisha kwamba maskuli yote yanapata hati miliki. Naomba niwashukuru sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba wameanza kutanguliza, kwa sababu ile kazi inahitaji vifaa, inahitaji malipo. Lakini nawashukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba sasa hivi malipo wameshafanya ndani ya wizara yangu, ili kuhakikisha kwamba kazi ile inakamilika kwenye maskuli ya Magharibi A, ambazo tumezianza na zimeshafanyiwa *PG* zimeshapimwa na sasa hivi nyingi zinawekewa *beacon*. Kwa hivyo, suala hili naomba niwatowe wananchi wasiwasi, niwatowe wasi wasi wajumbe wako wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba skuli zote za Unguja na Pemba zitaendelea kupimwa na kupatiwa hati miliki, na tutajitahidi kadiri iwezekanavyo kwamba zoezi hili likamilike kabla ya mwaka 2020, wakati tunakwenda kwenye uchaguzi mkuu wa serikali.

Jengine ambalo nataka kulizungumza Mhe. Mwenyekiti, hapa wizara yangu imejipanga vizuri kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, katika *master plan* ambazo zote zimetengenezwa na sasa hivi katika kutengeneza miji midogo, jambo la kwanza tumeangalia suala zima la maeneo ya skuli, lakini viwanja vya watoto ndani ya maskuli ni vitu muhimu ambavyo vimepewa kipaumbele. Suala hili nalisema kwa sababu sasa hivi ni kazi kubwa ambayo inafanywa huko.

Kwa hivyo, kwa mshirikiano yenu nyinyi kama Waheshimiwa Wawakilishi, tunawaomba sana mshirikiane na watu wetu wakati wa upimaji, lakini na zile *sacrifices* katika maeneo ya maskuli kwa sababu mwengine ni maeneo ya watu, kwa hivyo baada ya kutaka fidia kubwa basi wizara hii inakuwa na kazi, kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina jukumu la kutoa elimu, kuwalea watoto wetu na walimu hawa wanafanyakazi kubwa. Kwa hivyo, tuombe kwamba tushirikiane kwa pamoja katika kuhakikisha kazi hii tunaifanya kwa pamoja na kazi hii ilete matunda mazuri ili watoto wetu na watoto wa majirani zetu, kwa sababu mtoto wa mwenzio ni wako, basi sote tuhakikishe watoto wanasoma katika skuli hizi na katika yale maeneo ambayo yatakuwa yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la michezo ndani ya maskuli. Kusema kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali jamani imefanya kazi kubwa wamepiga hatua kubwa, mpaka idara ya michezo ndani ya wizara ipo, walimu wenye vipaji wapo na wanafanya kazi kubwa. Mimi naomba tu tuendelee kuwapongeza na tuendelee kuwashika mkono kuhakikisha kwamba

hii sekta ndani ya wizara inafanya kazi vizuri, watoto wetu wana vipaji na wana uwezo.

Kusema kweli mimi naomba niseme Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuambia hapa mheshimiwa kwamba ukizunguka, sisi tuliosoma Bara wakati ule tunaambiwa elimu Zanzibar tunaonekana kama mayahe, lakini unapokwenda kwenye vyuo, wanaoongoza kwenye vyuo ni watoto wa Kizanzibari. Katika skuli hizi hizi ambazo za serikali ndio watu walikuwa wakizisoma, skuli za maandalizi hizi zilikuwa Saateni na Kidutani na sasa hivi ziko nyingi. Lakini skuli za misingi hizi hizi ndio tumesoma na sekondari hizi hizi, lakini vipaji vya Wazanzibari vimekuwa vikubwa ndani na nje ya nchi. Naomba niliseme hili kinywa wazi, kwa sababu watu wananisikia Wazanzibari uwezo tunao, elimu tunazo lakini yote yametokana na juhudi za walimu wetu kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa hivyo, mimi niombe tu wizara hii tuendelee kuipongeza, tuendelee kuiunga mkono na tuendelee kuwapa nguvu ili waweze kutunyooshea watoto wetu vizuri ili wawe na maadili mema. Lakini tukija katika hili pia watoto wengi sasa hivi pamoja na pirika zilizokuwepo za utandawazi, tunazungumzia *globalization*, lakini bado walimu wanachukua juhudi ya ku-*control* watoto wetu na kuhakikisha wanawaweka sawa. Lakini sisi wazazi tunapoitwa maskulini wakati mwengine pia tunakuwa wazito wa kwenda, lakini wanatuita kwa sababu ya kutuongoza na yale malezi wanayoyataka wao yawe na watoto wetu na kule nyumbani yaende vile vile. Kwa hivyo, pia nitowe wito kwa wananchi tushirikiane na walimu pale tutakapohitajika ndani ya skuli, kwenye kamati za skuli lakini unapoitwa kujua maendeleo ya watoto, lakini pia kwenda kusikiliza maendeleo ya mtoto wako ni suala la umuhimu sana ndani ya maskuli. Kwa hivyo, tushirikiane nao tuwape *support* ili vipaji tuweze kuvinyanyua vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia, naomba wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu tuunge mkono hoja hii na tuweze kuipitisha bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali vifungu vyote bila ya matatizo, ili watoto wetu waendelee kuwa na mazingira mazuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Salama Aboud Talib. Sasa naomba nimwite Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini kwanza kabisa napenda nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza harakati zake za kuifanya elimu kuwa bure hadi hii leo, vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa pili wa Rais kwa jitihada zake za kusimamia Wizara zote ikiwemo Wizara ya Elimu na mfano hai katika jimbo lake la Mahonda.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kutangaza elimu kuwa bure ni jambo kubwa sana na sio jambo la kulibeza kwani Serikali inapoteza pesa nyingi sana katika hali ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar wasomeshe watoto wao bila ya malipo, hii ilikuwa ni ilani ya Afro Shirazi kabla ya Mapinduzi na baada ya Mapinduzi ikatekelezwa na hadi leo inaendelezwa, kwa hivyo ni jambo kubwa sana la kulipongeza na kumpongeza Rais aliyeko madarakani kwa kulisimamia hili.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nishauri wawakilishi namna ya kuisaidia elimu Zanzibar tuna wajibu mkubwa na tuna wajibu mkubwa kwa sababu zifuatazo, ukweli ni kwamba walimu wetu wanajitahidi sana kusomesha na wazazi nao wanajitahidi sana kusimamia harakati za watoto wetu kusoma. Lakini sisi kama viongozi kama wawakilishi na sisi pia tuna wajibu wa kusaidia elimu ikapata nafasi yake na hili nalizungumza zaidi kwa wawakilishi kutoka kisiwani Pemba kwamba kazi kubwa tunawaachia wazazi tunashindwa sisi kuwasaidia wazazi wakati watoto wanapokabiliwa na mitihani, hapa Unguja nimegundua kwamba Wazazi wanashirikiana na Wawawakilishi na Wabunge kwa nguvu zote na wanapiga kambi vijana na wanawashughulikia vijana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanafanya mitihani yao vizuri. Sasa na sisi tuige mfano huu kule kwetu Pemba Wawakilishi ambao tunaumwa na serikali hii na tuko tayari kuhakikisha kwamba ilani ya chama cha Mapinduzi inatekelezeka.

Kama tunavyojua ilani na sera ya Chama cha Mapinduzi huwa mtu anapoahidi inakwenda kwa muda wa miaka mitano kwa vile sasa ni wajibu wetu sisi katika hii miaka mitano kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapasi kwa wingi zaidi kisiwani Pemba kwa kujitolea wenyewe kuwapigisha kambi na kuhakikisha walimu wanapata motisha walimu wanapata nguvu na hata ikiwezekana kuwasidia. Serikali inasaidia sana hoja hii ndio maana licha kuwa na walimu Wazanzibari tuna walimu kutoka Nigeria, tuna walimu kutoka Ujerumani, tuna walimu kutoka India, tuna walimu kutoka Quba kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari tu wapate elimu huo ushahidi upo. Sasa leo tunabebwa lakini sisi wenyewe tunakuwa hatuko tayari kubebwa ni wajibu wetu sasa sisi kama

wawakilishi kuwasaidia wazee wasiokuwa na uwezo na hususan kama nilivyosema Kisiwani Pemba, kupiga kambi vijana wakati wa mitihani na kutoa nguvu zetu zote ili watoto wetu wapasi mitihani ile.

Wawakilishi sisi ni viongozi tulio na jukumu kubwa na tutakweda kuulizwa na lazima tukubali kwamba elimu ndio kitu pekee katika ulimwengu wa leo na hata hapo zamani, kwa sababu hata Mtume wetu Muhammad (SAW) aliteremshiwa Mwalimu Jibril akaja akamwambia Iqraa maana yake ni kwamba sote tunafahamu kwamba yeye ni kigezo, na hata Qur-ani ilisema *Lakad kunna fii rasulillahi us-watul hasanah*, kigezo chenu nyie ni Muhammad kwa nini? Kwa sababu yeye aliletewa mwalimu sasa kwa nini sisi tusijitayarishe kuwapa motisha walimu ili watoto wetu wakasoma vizuri. Waheshimiwa Wawakilishi tuna jukumu la kuwasaidia wazee wetu, tuna jukumu la kuwasaidia watoto wetu ili wapasi na wasome vizuri.

Mhe. Naibu Spika, walimu wanajitahidi kiasi cha kutosha kusomesha hili jambo linaeleweka wanajitahidi na ndio kama hivyo mwalimu anaweza kutoka skuli hii akenda kusomesha Kiembe Samaki, akatoka Kiembesamaki akenda Darajani mwalimu huyo huyo mmoja kwa nini, kwa sababu ya kuhakikisha taaluma yake anaitoa na jambo la kufurahisha basi mwalimu hapendi kumuona mwanafunzi wake kafeli. Anataka amuone mwanafunzi wake kamsomesha kapasi na hilo jambo tulielewe, na sisi tujifahamu kwamba tulikuwa wanafunzi, hakuna hata mmoja ambae hakusomeshwa humu ndani. Walimu walikuwa na majukumu makubwa kila mmoja kasomeshwa humu ndani, walimu walikuwa na majukumu makubwa ya kutusomesha sisi na sisi leo tuwe na majukumu makubwa ya kusomesha watoto wetu, wala tusichague elimu haina itikadi ya chama, elimu haina dini ya chama, elimu haina chochote. Elimu ni elimu tu ukipata elimu utalitumikia taifa hili.

Waheshimiwa Wawakilishi lazima tuhakikishe kwamba vijana wetu tunawasimamia kuwa wazalendo wa baadae maana neno uzalendo ni jambo kubwa sana. Nchi hii ishasomesha watu wengi sana na kila anayesoma akipata *Degree*, akipata *Master* anakimbia kwa nini amekosa uzalendo lakini tukiwasomesha katika utaratibu mzuri na tukawaelimisha kwamba hii nchi ni nchi yao na wanatakiwa waitumikie kwa nguvu zao mimi naamini wasomi watabakia na wataitumikia Zanzibar ili ifikie malengo yake ya kuwa bora zaidi katika Afrika ya Mashariki na Kati.

Mhe. Mwenyekiti, ningetaka niseme kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amejitahidi sana katika hoja ya kunyanyua michezo ndai ya maskuli yetu ya Unguja na Pemba, sisi kama

wawakilishi tujitahidi sana kumpa nguvu Mhe. Rais ili na sisi tuweze kuonyesha uwezo wetu wa kimichezo katika maskuli kwa kutoa zawadi ndogo ndogo ili kuwapa motisha vijana wetu ili waimarishe michezo kama vile ambavyo tunalitaka taifa hili lifikie hatua hiyo. Tusifanye ubakhiri kuyafanya hayo tusiwe tayari kungojea watu waje watufanyie hayo hakuna watu wa kuyafaya hayo ni sisi wenyewe Wazanzibar kwa watoto wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani nilikuwa nitoe ujumbe huu ili kuwatanabahisha viongozi wawakilishi hawa katika mazingira ya lazima ambayo yanatulazimu sote kwa pamoja, katika kuisaidia Serikali ili kufikisha malengo yake ya sera na ilani ya Chama cha Mapinduzi kama vile walivyokuwa wameahidi wakati walipokuwa wakitafuta ridhaa ya wananchi wa Zanzibar. Sasa sisi kama viongozi lazima tutekeleze ilani hiyo kwa vitendo ili kuwafanya Wazanzibari ambao wametuchagua basi waridhike na miaka mitano hii ya ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na nawaomba Wawakilishi wote tuipitishe bila ya mabuti, tuipitishe tu hii hoja ipite tupate ufafanuzi wa kuendelea mbele.0000. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi sasa naomba Mhe. Waziri Moudline Cyrus Castico ambae ameniambia atachangia kwa dakika tano kabla ya kumpisha Naibu Waziri wa Elimu ili ajibu zile hoja za Wajumbe atakazozijibu. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Waziri wa Uwezehaji, Vijana, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupa nafasi tena ya kuweza kuendelea katika Wizara hii makini ambayo ni muhimu sana katika maisha kwa sababu amesema mshike sana elimu, usimuache aende zako kwa maana ni uzima wako. Napenda nimpongeze sana Mhe. Rais kwa juhudi anazofanya kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma katika mazingira ya kupata elimu bure katika maisha yao, lakini pia ka ajili ya Waziri wetu wa Elimu Mhe. Riziki Juma Pembe kwa kazi zake nzuri pamoja na Wizara yake wanazofanya kwa moyo wa dhati.

Labda ningependa tu kusema kwamba kuhusiana na ushauri wa kituo cha watoto wanaopinzana na sheria, nitake kusema tu kwa kutaka kuwaambia Wawakilishi kwamba Wizara hii na masuala haya yanashughulikiwa sana na Wizara yetu na watu wanaofanya kazi hii hawawezi kufanya kazi hiyo pasipokuwa na elimu ya kutosha, wanakwenda kusoma vyuo vikuu, wanakwenda nchi za nje kusomea masuala haya. Kwa sababu *sychologier*

peke yake kuisomea ili uweze kupasi kumshauri mtu mwengine sio chini ya Degree ya miaka mitatu lakini pia kuna wanasheria wengi ambao ni matunda yetu kutoka shule za *SUZA* Chuo kikuu kilichoko Tunguu na maeneo mengine ambao ndio wanaokuja kuajiriwa katika Wizara yetu. Kwa hivyo wasiwe na wasiwasi kwamba Wizara yetu labda inakaa na watu ambao hawajaenda shule vizuri au hawajasoma vizuri wanasoma na wanajiandaa kwa faida ya kutaka kuhakikisha kwamba wanafanyakazi vizuri.

Lakini la pili niseme tu kuhusiana na masuala ya ushirika na masuala ya Saccos na ukopeshaji, napenda niseme napenda sana kupongeza Wizara ya Elimu kwa kazi zao na uratibu mzuri waliofanya wa wafanyakazi wote walioshiriki katika masuala ya SACCOS, katika SACCOS ambayo ni kubwa sana katika nchi yetu ya Zanzibar ni pamoja na Wizara ya Elimu kwa pamoja wameshirikiana na Afisi yetu imekuwa ikiwaratibu imekuwa ikiwasimamia ……

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa samahani kidogo Waheshimiwa Wajumbe nawaomba sana bado utulivu na sauti na minong'ono hii mara ya pili, ya tatu nitamuomba mjumbe anayeongea atoke nje akazungumze, ya kwanza nimesoma kanuni tuelewane ya pili narudia tena mara ya tatu kila mjumbe nitakayemuona anaongea na sauti zinatoka nitamtoa nje kwanza akazungumze halafu baadae arudi.

Mhe. Waziri wa Uwezehaji, Vijana, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutusimamia na kutukumbusha kanuni, niseme tu katika SACCos ya Wizara ya Elimu hivi sasa hivi wanakopeshana vespa, mabati, vitu vingi sana ambavyo ningeshauri pia Wizara nyengine kama wanaweza waanzishe SACCOS katika maeneo yao ambayo inakuwa ni rahisi sana kuchangia kwa sababu wanaweza kufanya utaratibu ambao ni mzuri wa pesa kukopwa na kurudishwa kwa wakati.

Suala la mimba za utotoni Mheshimwa ni jambo ambalo linarudisha sana maendeleo watoto wa kike ili wamalize masomo yao vizuri wawe akina mama bora, mtoto wa kike akishakatishwa maisha yake akiwa mdogo *future* yake haipo namna ya kumlea yule mtoto inakuwa ni matatizo ndio hao hao baadae wanakuwa watoto wenye matatizo katika jamii. Lakini mara nyingi tunazungumza habari ya mtoto wa kike huyu mtia mimba mbona hatumtaji mara nyingi, kwa hivyo Wizara yangu inajitahidi kutaka kuhakikisha kwamba na huyo anayechangia kufanya mtoto anapata mimba nae tutafute utaratibu mzuri wa kuweza kushughulikia suala hili. Tumefika kupendekeza kuona kwamba ni vyema basi kuwe na kipindi maalum cha kuweza kupima mimba watoto mapema wakiwepo shule na pia kutafuta utaratibu gani, wasichana

wanapokuwa kwenye makundi kila mmoja anajua fulani na fulani anatembea na fulani watakuwa ni mashahidi namba moja kwa kutaka kuangalia kwamba hii mimba aliyemtia ni fulani na maendeleo yaendelee kufuatiliwa ili kuweza kukwepa hili suala la kutekeleza msichana akiwa na mimba wakati kijana aliyemtia mimba yeye anaendelea kudunda na anaendelea kufanya shughuli zake vizuri.

Kuna famili nyengine zenye watoto wa kiume wanafanya mazoezi kwa wasichana wenzao akishaona anazaa anajua mimi hata nikikua siku moja nitazaa naomba watoto wasifanyiwe mazoezi watoto wa kike kwa kujaribu kwamba atazaa siku moja. Wizara ya Elimu na Wanawake zisingependa kabisa kuwepo na vituo vyovyote vile vinavyohitaji kwa mfano Mahakama, suala la Mahakama likiendelea ni kwa maana bado tunaendelea kupinzana na taratibu, lakini maadam lipo jamii inaonyesha kwamba tunazidi kumong'onyoka kwa hivyo tujirudi katika maisha yetu ya kawaida ya Kizanzibari ambayo tulikuwa tunapendana sana. Watoto wetu wana vipaji vingi vizuri sana lakini kutokana na hii hali ya kusumbuliwa leo kaingiliwa leo kafanywa hivi, leo katelekezwa leo kaachwa mtoto anakuwa anahangaika anakwenda kutoa ushahidi wakati wenzake wanasoma kitu ambacho kinarudisha maendeleo nyuma.

Lakini jengine pia naomba nishauri jamii akina baba hebu kumbukeni yale maneno mnayokuwa mkizungumza wakati unapomtaka msichana silali, sipati usingizi, sifanyi nini mpenzi wangu nakupenda nitakutunza, unasema mzuri kama rangi ya chungwa, lakini ukishakaa nae siku mbili unamchoka ukishamchoka yeye unawachoka pamoja na watoto, watoto wanakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa mama hasa kwa wale wanawake ambao wameolewa bila ya maandalizi mazuri wanapata shida. Wizarani kwangu kila siku naletewa watu wa namna hiyo nawaomba tushirikiane hebu nyie mnapokula chakula kweli unameza mojawapo hata akiwa mwakilishi wengine wako hapa hapa ambao wanawakilisha watoto, unakula chakula unameza kabisa wakati unajua una watu sita nyumbani umewaacha ambao hujawasimamia naomba tushirikiane ili watoto waweze kufanya vizuri na Wizara ya Elimu iweze kutoa watoto wazuri watakaoturithi katika vizazi viavyo. Akinababa tuendelee kukumbuka kwamba unapokula *chips*, unapokula kuku, watoto uliowaacha wapelekee basi hata kipolo cha mapembe na sukari wapate kula. Nawatakieni kila la kheri, Mungu awabariki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naye atoe ufafanuzi kwa masuala aliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hotuba yetu hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini kabla ya kufafanua baadhi ya hoja ambazo zimeletwa kwetu na mimi ningelipenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wafanyakazi wenzangu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hasa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ushrikiano mkubwa kabisa anaonipatia katika kufanya kazi zetu, watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu,Wakurugenzi, Maafisa wa Elimu wa Mikoa na Wilaya, Walimu Wakuu, Wasaidizi Walimu Wakuu, Walimu wenzangu, wanafunzi, Masheha na viongozi wote wa Wilaya na Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi kabla ya kuendelea ningependa kueleza maneno ya utangulizi kama yafuatayo.

Sisi viongozi wa Wizara ya Elimu tunaelewa kwamba nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mnayajua mengi ambayo sisi hatuyajui au tumeyasahau, lakini pia na sisi viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu tunayajua mengi ambayo nyinyi hamuyajui au mmeyasahau, kwa hivyo tupo hapa sisi Wizara ya Elimu kuwaelimisha nyinyi yale ambayo hamuyajui, lakini pia tupo hapa kuwakumbusha yale ambayo mmeyasahau, lakini pia na nyinyi mpo hapa kutueleweshe sisi yale ambayo hatuyajui na kutukumbusha yale ambayo tumeyasahau. Kwa hivyo kazi yetu ni moja tu kuelimshana na kukumbushana sote kwa pamoja.

Baada ya kusema hayo sasa nianze kujibu hoja na nianze kwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe katika wasaa huu tutapenda kumjibu suala lake au hoja yake ambayo alitaka kujua, huu ukaguzi wa kushtukia uko vipi sasa katika skuli zetu.

Napenda kusema kwamba, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu ina njia nyingi za Ukaguzi njia moja wapo ni ya ukaguzi wa kushtukiza, na niseme kwamba ukaguzi unafanyika na katika kipindi cha mwaka uliopita wa fedha 2016/2017 jumla ya skuli 178 zilifanyiwa ukaguzi wa aina hii. Kwa hivyo napenda kuwakubusha kwamba ukaguzi upo na unaendelea na aina nyengine za kaguzi tunaendelea kuzifanya, lakini kwa kutumia fursa hii nipende kusisitiza kwamba walimu wakuu na wao pia kuanzia sasa watafanya kazi hii ya ukaguzi tunaita *co-inspector* wataendelea kufanya kazi hiyo, kwa hiyo wakati wote walimu watakuwa chini ya usimamizi.

Lakini pia napenda muelewe kwamba mtizamo wa ukaguzi wa skuli uweleweke kwamba ni mtizamo au ni ukaguzi wa kirafiki, hatutaki wakaguzi

waonekane kama ni polisi miongoni mwa walimu hapana, hawa ni wakaguzi washauri na kazi hizo inaendelea kufanyika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said Jimbo la Chake Chake huyu naye pia alitaka kujua shughuli gani zimepelekea kuengezeka kwa bajeti ya Ofisi ya Mkaguzi kutoka Millioni sitini mpaka kufika milioni mia moja na ishirini na swali hili, hili pia limeulizwa na Mhe. Maryam Thani Juma Mwakilishi wa Jimbo la Gando, lakini pia na Mhe. Salma Bilal Viti Maalum, Mkoa wa Kusini Pemba. Tunasisitiza kwamba saivi Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu, inafanyiwa mabadiliko makubwa na katika mabadiliko hayo ndiyo yaliyopelekea kuengezeka kwa bajeti hiyo, kwa sababu mabadiliko hayo yanahitaji kuengezeka kwa nyezo na ofisi mpya tano za kanda, ambazo zitaanzishwa katika Mikoa yetu sasa mabadiliko hayo, ndio yaliyopelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa ofisi hii na kadhalika.

Lakini pia, nasema kwamba katika kufungua ofisi zetu za kanda tutahitaji wakaguzi, sasa wakaguzi pia wana gharama zao za kuendesha skuli, Mhe. Salma Bilali yeye aliongeza zaidi kwamba mahitaji ya ukaguzi huo ni kupatikana kwa ofisi ambazo zitahitajika ukarabati mkubwa, au zijengwe ofisi mpya za ukaguzi huo na kila ofisi itakuwa na wafanyakazi 20 pia kutahitajika huduma za usafiri. Sasa ukichukua zote hizi utakuta ndizo zilizopandisha bajeti hii ya Ofisi ya Ukaguzi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said, anaendelea tena kuuliza pamoja na Mhe. Mwantatu Mbaraka wa Viti Maalum yeye anasema ukaguzi unaofanyika haumwangalii mwalimu darasani anadhani kwamba ukaguzi ambao tunafanya sasa hivi haumwangalii mwalimu darasani. Sisi wizara tunasema kwamba ukaguzi huu unamwangalia mwalimu darasani na upo, na umefanyika kama tulivyosema awali umefanyika kwa jumla ya skuli 77 zimefanyiwa ukaguzi huo wa ziara ambao ni kumkagua mwalimu darasani, ukaguzi huo hufanywa bila mwalimu kumpa taarifa. Kwa hivyo unakwenda moja kwa moja kwa mwalimu kuangalia mbinu zake za kusomesha, kumwangaliwa zana zake za kusomesha, kuwangaliwa hata uwezo wake wa kumudu somo lake, ziara hizi za ukaguzi tunazifanya.

Mhe. Maryam Thani Juma tena wa Jimbo la Gando yeye alitaka kujua katika kikao cha bajeti iliyopita ilipendekezwa kuanzishwa kwa ukaguzi wa Wilaya, namjibu kuwa mapendekezo hayo yanafanyika ndio huu ambao tunaita ukaguzi wa Kanda. Mhe. Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga yeye alitoa ushauri wa kukiendeleza kitengo cha ukaguzi, kwa hivyo napenda kusema kwamba hatua za kuendeleza Ofisi ya Ukaguzi imefanyika ikiwa ni pamoja na kuengezea hii

bajeti kutoka milioni sitini hadi mia moja na ishirini, hata hivyo tunasema kwamba kuimarika kwa kitengo hichi kutapelekea pia kuimarishwa kwa huduma za usafiri na kuwapatia motisha wakaguzi ili kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Maryam Thani Juma vile vile, wa Jimbo la Gando na Mhe. Rashid Makame Shamis wao walitaka kujua kuhusu suala la kufanya mapitio ya Sera ya Elimu, tunapenda kusema kwamba mfumo wa Elimu kwa mujibu wa sera ya Elimu ya 2006 inayoendelea kutekelezwa ni miaka miwili ya maandalizi kama ilivyofafanua Mhe. Haroun miaka 6 elimu ya msingi, na miaka 4 elimu ya Sekondari kwa wote na watakaofanikiwa kuingia kidatu cha tano na sita watasoma kwa miaka miwili, mfumo huu ulipitishwa baada ya kutafuta maoni kwa wadau mbali mbali kama alivyofafanua Mheshimiwa hapo kwamba karibu wananchi wote walishirikishwa kupitia kamati mbali mbali, kupitia vyombo mbali mbali. Sera hiyo pia ilizingatia mazingira ya dunia katika upatikanaji wa fursa za elimu mfumo huo sio mgeni unatumika katika nchi nyingi za SADC zikiwemo *Mauritius,* lakini pia katika baadhi ya nchi mtoto huanza masomo yake katika umri wa miaka 5 na anaendelea na elimu yake mpaka atakapofikia lakini pia katika nchi za *Malaysia*, *Seychelles* na Ghana pia wanatumia utaratibu kama huu.

Jirani zetu wa Kenya wao wana miaka 8 ya elimu ya msingi, ambapo sisi Zanzibar tumeigawa elimu ya lazima kwa wote ni miaka 12 kama tulivyotanguliza kusema, ndugu zetu Tanzania Bara wao elimu yao unaanza na mfumo huu wa miaka 3 mpaka 5 elimu ya maandalizi na miaka 7 elimu ya msingi, ambapo mtoto wa miaka 6 anaanza darasa la kwanza pia sera yao inatoa fursa kuanza elimu ya msingi akiwa na umri wa miaka 5 tu. Lakini mfumo huu una faida zake na miongoni mwa faida ambazo tunatarajia kuzipata katika mfumo huu, ni pamoja na vijana wetu kumaliza elimu ya juu wakiwa na umri wa kati ya miaka 20 na 21 badala ya kumaliza katika umri mkubwa miaka 28, 30 na kadhalika. Lakini pia inawapatia fursa ya masomo ya nje ya nchi kupitia wafadhili mbali mbali, ambao masharti mengine yanazingatia umri, ukizidi umri fulani huwezi kupata nafasi ya masomo. Sasa umri wa vijana wetu kumaliza masomo unakwenda sambamba na soko la ajira na soko la ufadhili duniani. Kwa hivyo, nadhani tuko katika njia sahihi katika mfumo huu.

Faida nyengine za wanafunzi wetu kuzingatia masomo yao wakiwa na umri ambao haujachanganyika na athari zao za kimakuzi na kimaoni, maumbile na mitizamo. Hata hivyo, wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, imewasilisha warka wa kujadili hoja ya kupitia Sera za Elimu, ni kwamba baada ya kupata malalamiko na maoni ya wananchi mbali mbali, wizara

imeamua kufanya mapitio na taratibu za mapitio zinaendelea na nyinyi wawakilishi wa wananchi tutawapitia kutoa maoni yenu wakati utakapofika.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine hii ambayo imetolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) Mwakilishi wa jimbo la Mpendae. Yeye aliuliza wizara imejipanga vipi hasa katika idadi ya walimu wa michezo waliotayarishwa katika kuhakikisha kwamba azma na heshima ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein katika *Sport fifty-five* inapangiwa. Ni kweli kwamba tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba malengo ya *Sport fifty-five* yanafanikiwa ikiwa ni sehemu muhimu ya kuthamini jitihada za Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na wadau wote waliochangia.

Mpango wa *Sport fifty-five* ni sehemu katika utekelezaji wa mpango wa miaka mitano wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo. *Sport fifty-five* moja ya malengo yake ni kuwapatia taaluma sahihi ya uendeshaji na usimamizi wa michezo walimu wetu wa michezo kutoka wilaya zote. Tayari kabla ya kuanza mpango huu zaidi ya walimu 260 wameshapatiwa mafunzo ya ukufuzi wa michezo wa mpira wa miguu kwa mashirikiano na Baraza la Taifa la Michezo kupitia mradi wa *coaches across continents* zaidi ya walimu 100 wamepatiwa mafunzo ya utawala na usimamizi wa michezo kupitia kamati ya Olimpic Tanzania, pamoja na walimu zaidi ya 60 wamepatiwa mafunzo ya ukufuzi wa riadha kwa msaada wa Chama cha Riadha. Kufanikiwa kwa *Sport fifty-five* kutaongeza nguvu na ufanisi wa wataalamu hao pamoja na kuongeza idadi ya walimu wengine. Kwa ujumla Wizara inaamini sana kamati ya Mhe. Balozi Ramia, inayosimamia *Sport fifty-five,* kwa pamoja tutahakikisha kwamba fedha zilizopatikana na zitakazopatikana kutokana na udhamini wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, zinatumika vyema na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hoja nyengine iliyotolewa na Mhe. Nadir Abdul-latif wa Jimbo la Chaani, hoja yake ni kwamba wizara ifanye juhudi za kutafuta *scholarship* za nje kwa ajili ya kusomesha vijana wetu fani za Mafuta na Gesi ili kuandaa wataalamu wazalendo ushauri huo ni mzuri, na umepokelewa na tayari umeanza kufanyiwa kazi kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Jumla ya vijana 27 wapo vyuoni nchini China na Sudan kwa vyuo vya nje na UDOM kwa vyuo vya ndani. Wanafunzi hao wanasomea Shahada ya Kwanza ya Mafuta na Gesi, juhudi za kutafuta nafasi zaidi zinaendelea kuchukuliwa kwa hivyo ushauri wake tunaendelea kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Mihayo Juma N'hunga wao wanasema kwamba fedha za Serikali zilizotolewa kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu ni nyingi, kwa hivyo juhudi zaidi ziongezwe katika kukusanya marejesho, ili fedha ziweze kukopeshwa kwa wanafunzi wengine, nadhani ni maoni mazuri na tutayafanyia kazi. Kwa hivyo nasema ushauri huo umepokelewa na Bodi imeongeza kasi ya makusanyo na kuweka mikakati mbali mbali ikiwemo kuwatafuta wakopaji, wa kutembelea Ofisi moja kwa moja walizoajiriwa, kutozwa adhabu kwa wanaokwepa au kuchelewa kulipa madeni yao kwa wakati. Kufualitia makopaji walioajiriwa Tanzania Bara kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Utumishi, kwa mwaka 2016/2017 Bodi inatarajia kukusanya zaidi ya shilingi bilioni moja na mwaka 2017/2018 Bodi imejiekea lengo la kukusanya shilingi bilioni 1.5. Kwa hivyo mikakati imewekwa madhubuti na ndio maana idadi ya wanafunzi waliokopeshwa wanaorejesha fedha zao, inaongezeka na sisi wizara inafanya kazi usiku na mchana kuona jambo hili linafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kwa majumuisho yako muda sio rafiki tena nina imani atakapokuja Waziri jioni anaweza akamalizia na hayo yaliyobaki. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa michango yenu lakini pia nawashukuru kwa usikivu wenu na utulivu wenu, katika kuwasilisha hizi hoja kabla ya kuakhairisha kikao kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane katika ukumbi Nam.2. Ahsanteni sana. Kikao nikiakhirisha mpaka saa 11.00 jioni. Nawashukuru sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Kikao Kilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa nimepata ombi la Naibu Waziri ambaye alikuwa hajamaliza muda wake katika kutoa majumuisho lakini nitatoa ile dakika 15 ya Mhe. Waziri halafu tutaendelea, sawa. Haya nakupa dakika 15 za kumalizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ninapenda niendelee kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wawakilishi. Niendelee na hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed

kwamba alitaka kujua zabuni za uandishi wa vitabu Zanzibar. Tuseme kwamba zabuni za uandishi wa vitabu zinatolewa kwa makampuni ya uchapishaji na wala sio muandishi binafsi, labda ndio sababu moja ikawafanya waandishi wa Zanzibar wasipate fursa hii na tunaita *publishing house*.

Hata hivyo katika Kampuni zilizoomba zilikuwa ni kama 14 na miongoni mwa kampuni hizo 14 ni moja tu kutoka Zanzibar, na bahati ikashinda zabuni ya kuandika kitabu cha Somo la Sayansi Jamii. Sasa baada ya kampuni kushinda, wao hutafuta waandishi wa kuwaandikia na kwa bahati kampuni hii pia ikatafuta waandishi wa Zanzibar. Muandishi ni Ali Mwalimu Rashid na Ali Shabani Juma wakapata kazi ya kuandika vitabu hivyo.(*Makofi*).

Baada ya vitabu kuandikwa na hufanyiwa mapitio na walimu wanaohusika na somo hilo na baadae huthibitishwa kwa ajili ya uchapishaji. Hizo ndizo taratibu ambazo huwa tunatumia katika Wizara ya Elimu. Kwa hivyo mimi nipende kutoa wito katika muktadha huu kwamba ni vyema Wazanzibari pia wakaanzisha kampuni za uchapishaji (*publishing house),* ili kuweza kutumia waandishi waliopo kuchapisha vitabu mbali mbali.

Kwa upande mwengine tunashirikiana vizuri na waandishi mbali mbali wa Zanzibar katika shughuli mbali mbali za elimu, ikiwa ni pamoja na kutoa mihadhara, kubadilisha uzoefu na mambo mengine ya namna kama hiyo. Tunashirikiana vizuri na Said Ahmed, Mohamed Suleiman, Shafi Adam Shafi na wengineo pamoja na waandishi wengine chipukizi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala jengine lililotolewa na Mgeni Hassan Juma ilikuwa kama ni ushauritu, yeye alikuwa anadhani kwamba tulikuwa bado hatujaanzisha mitaala ya maandalizi, yeye anaita chekechea lakini sisi tunaita maandalizi. Nimueleweshe tu kwamba mitaala hiyo ipo na inatumika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine imetolewa na Mhe. Ali Khamis Bakari. Yeye alikuwa anazungumzia suala la uzio wa Skuli ya Chwaka -Tumbe. Sisi Wizara tunaelewa kwamba skuli nyingi hazina uzio na kwa kweli ni suala ambalo tunalielewa. Lakini kwa sasa tunahisi kwamba suala la uzio ni mradi mkubwa sana. Kwa hivyo katika vipa umbele vya sasa tunahisi ni afadhali kukamilisha madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kuliko kujenga uzio. Lakini hata hivyo suala hili tunalitafakari kwa ukubwa zaidi. Wizara inapenda sana kuwashirikisha na kuwashajihisha wananchi kupanda miti katika maeneo ya skuli ili kuyahifadhi lakini pia wakati mwengine kuzuia uingiaji wa watu na mambo mengineo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala jengine alilouliza Mhe. Mohammed Said Mohammed, yeye alitaka kujua suala la fedha za *Skill Development Levy (SDL)* kama Wizara inapata au haipati. Namthibitishia kwamba Wizara inapata na imeshaanza kufanya manunuzi ya baadhi ya vifaa na tumepata kwa mfano jumla milioni mia sita na arubaini na moja elfu, laki tisa na sitini na nane elfu mia tatu na tisini na tatu (641,968,393). Hizi zimetumika kwa kununulia meza na viti katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba. Ufafanuzi zaidi angalia jadweli Nam. 12E katika kitabu cha hotuba yetu.

Mhe. Mgeni Hassan Juma pia aliendelea kutahadharisha kuhusu suala la mikataba mibovu inarudisha nyuma azma ya Rais kuwapatia wanafunzi elimu bora. Ni kweli tunakubaliana na sisi Wizara tunahisi maoni haya ni mazuri na tunayachukua na tutajitahidi katika usimamizi wa majengo ili kuweza kupata majengo yaliyo imara zaidi na kwa kweli tupo makini sana, tunafanya kazi, tunafuatilia kwa karibu, tunafuatilia mpaka mienendo ya zabuni zenyewe. Ninamuhakikisha kuanzia sasa majengo yatakuwa imara zaidi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamida Abdalla Issa na Mhe. Rashid Makame Shamsi, hawa walitaka kujua idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Amali Zanzibar. Kwa lugha nyengine alitaka tufanye tathmini ili kujua idadi ya wana vyuo waliokuwepo katika Vyuo vya Amali Zanzibar na akataka kujua kwamba tunachukua hatua gani ili azma ya kuanzishwa Vyuo hivyo viweze kufanikiwa. Niwahakikishie kwamba Wizara tayari imeshaanza kufanya tathmini na baadhi ya hatua zimeshaanza kuchukuliwa zilizopelekea kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliojiunga katika mafunzo hayo. Hata hivyo vituo bado vinahitaji wanafunzi zaidi. Idadi ya wanafunzi imeongezeka lakini si kwa mujibu wa uwezo wa Vyuo vyengine. Kwa hivyo tunataka kufanya juhudi zaidi kwa kuwashajihisha na kuwashawishi wananchi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hapa napenda kutoa wito tena kwa sisi Waheshimiwa Wawakilishi kuwashajihisha wananchi wetu katika majimbo kujiunga na mafunzo ya Amali, hii ni kazi ambayo ni muhimu kuifanya. Sisi kwa upange wetu Wizara tumewaandikia barua Wawakilishi wote, nadhani mmezipata kwa namna ya kuwakilisha na hata kuwadhamini baadhi ya wanafunzi kusoma katika Vyuo vya Amali. Nadhani hilo limeeleweka.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Mhe. Ali Suleiman Ali, yeye alisema Wizara ina mpango gani wa kuwapatia nyenzo wahitimu wa mafunzo ya amali. Tuseme tu kwamba Wizara kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inatoa mikopo nafuu isiyo na riba. Wahitimu wa wanaomaliza mafunzo ya amali kupitia vikundi vyao ambavyo wamevianzisha na kuvisajili. Katika mpango huo mpaka sasa

tumeshawapatia mikopo vikundi 10 vya wahitimu wenye jumla ya wanafunzi 60. Pia vituo vya Mkokotoni, Vitongoji na Mwanakwerekwe vimeanzishwa miradi ya uzalishaji ambayo pia vinasaidiwa kupatiwa nyenzo mbali mbali.

Mhe. Hidaya Ali Makame, yeye alitoa ushauri kwa kweli Wizara izidi kupunguza changamoto zilizopo katika Vituo vya Amali, kwa kutumia bajeti iliyotengwa kwa ukamilifu wake. Ushauri huu tumeupokea na ndio nia ya Wizara kutekeleza mambo kwa ufanisi, ubora na kwa wakati.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla, yeye anataka kujua tu kuhusu mikopo waliyopewa Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni pamoja na Kituo cha Vitongoji Pemba baada ya kumaliza masomo yao walipangiwa kupata mikopo, na pia na kujua mikopo hiyo inaendelea vipi na vikundi vingapi vimefaidika na mikopo hiyo. Nimjibu tu kwamba kuwapatia mikopo wahitimu waliomaliza katika vituo vya mafunzo ya Amali, Mkokotoni, Mwanakwerekwe na Vitongoji Pemba inaendelea vizuri. Mpaka sasa jumla ya shilingi milioni hamsini na mbili, mia tisa na ishirini na saba (52,927) zimeshakopeshwa kwa wahitimu mpaka Aprili hii. Lakini kwa kuwa mkopo ni kupokea na kurudisha, baadhi yao wamesharejesha kiasi cha jumla ya shilingi milioni sita, laki tisa na thalathini na tatu elfu na shilingi hamsini (6,933,000.50). Mpaka mwezi wa Aprili jumla ya vikundi 10 vya wahitimu vyenye jumla ya wahitimu 60 wameshanufaika na mikopo kama nilivyosema juu. Mhe. Naibu Spika, ukaguzi wa mwisho wa vikundi hivi umebaini kwamba shughuli zao wanazozifanya zikiwemo ushoni, huduma za gereji, karakana za ufundi wa elektroniki, ufundi bomba zinaendelea vizuri. Kwa hivyo ina maana fedha zinatumika vizuri.

Mhe. Hamida Abdalla Issa kwa mara nyengine tena, yeye alikuwa anatoa hoja kwamba Wizara itoe muongozo maskulini kwa utoaji wa adhabu mbadala ili kuepusha utashi wa baadhi ya walimu, kwa kuwa kuna maskuli watoto wanapewa adhabu ya kupeleka mifuko ya saruji. Nimuhakikishie kwamba Wizara inasikitika sana kwa vitendo hivyo na inawataka walimu hao waache vitendo hivyo vinavyofanywa. Kwa sasa Wizara imeondosha suala la adhabu mbadala na mfumo wa nidhamu endelevu ndio unaotekelezwa kwa sasa. Tumebadilisha mtindo, sasa tuna nidhamu endelevu badala ya adhabu mbadala. Dhana hii imepatikana kutokana na ushirikiano wa wadau mbali mbali wa elimu wa ndani na nje wakiwemo *Save Children*.

Mhe. Naibu Spika, Wizara imepanga kuwapatia mafunzo ya utoaji nidhamu endelevu walimu wote wa Unguja na Pemba, wakiwemo walimu wa madrasa mpaka wa Vyuo vya Kur-an pia tutawapatia ili na wao pia wajue kutoa adhabu

katika mfumo huu. Pia miongozo kwa ajili ya walimu imeshatayarishwa na kuchapishwa na wakati wowote kuanzi sasa mafunzo yataanza.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo limeulizwa na Wawakilishi wengi, suala la ajira katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Niseme kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mpango Mkuu wa Raslimali Watu *(nominal role)* kwa mwaka 2016/17 ina jumla ya nafasi 456 za ajira kwa wafanyakazi wa kada tofauti, kati yao 250 Unguja na 206 Pemba. Kwa sasa Wizara inasubiri kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini ili iweze kuwaajiri. Katika nukta hii kumetolewa maoni mbali mbali juu ya suala la namna ya kuajiri, wanaojitolea, wanaofanya hivi na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba Waheshimiwa Wawakilishi kuna Sheria inayosimamia suala hili la ajira, kwamba nafasi inapotokea itangazwe katika vyombo vya habari na kila mwenye sifa aombe, anayejitolea na asiyejitolea. Mhe. Naibu Spika, lazima tuweke wazi Kanuni na Sheria zinavyoeleza. Hata hivyo kwa kuwa walimu wanaojitolea wamepata uzoefu mkubwa, tunaamini katika taratibu za ajira zikiwemo usaili wanaweza kufanya vizuri. Kwa maana hiyo wataweza kuajirika endapo utaratibu wa usaili kwa wanaojitolea watafanya vizuri zaidi. Lakini nataka isieleweke kwamba kujitolea ndio sababu au ndiyo sifa ya kupata ajira serikalini, siyo hivyo, si sahihi, mpaka sasa si sahihi. Kwa sababu tunajua kwamba katika maskuli yetu kuna walimu wengi wanaojitolea, hiyo ni sifa ya uzalendo na tunawapongeza kwa kweli. Lakini Sheria na Kanuni za Utumishi zinatueleza hivyo kwamba tutangaze nafasi na kila mmoja mwenye sifa aombe.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la Tatu Mohamed Ussi, yeye alikuwa anataka kujua kuhusu mikopo kutolewa kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi na kupuuza masomo ya sanaa. Nimuhakikishie kwamba serikali imeweka vipa umbele vyake kupitia Tume ya Mipango. Vipaumbele hivi vimelenga zaidi katika masomo ya sayansi. Kwa sababu katika miaka mitano hii inayokuja ndiyo tegemeo kubwa la kujaza nafasi katika nyanja za sayansi. Lakini hata hivyo vipa umbele vyenyewe pia vimegawika katika sehemu tatu nazo ni:-

- Kuna masomo kipa umbele cha kwanza,(katika kundi hilo hilo la sayansi)
- Kuna masomo kipa umbele cha pili,
- Kuna masomo kipa umbele cha tatu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa sanaa nimuhakikishie kwamba yapo baadhi ya masomo bado tunaendelea nayo kuyapa nafasi ya kipa umbele, ni masomo

kama vile *geography*, *history*, *English*, utalii, uchumi, masoko ya hisa, ufuatiliaji na tathmini. Haya nayo pia tunaweza kuyapatia. Lakini hii haina maana kama Vyuo Vikuu vitafungwa, hapana, vitaendelea kutoa huduma zake za kusomesha masomo ya sanaa na kadhalika.(*Makofi*).

Mhe. Zulfa Mmaka Omar yeye alikuwa anasema kuongezwa kwa Ruzuku ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili iweze kuwasaidia wanafunzi wengi wa kike. Niseme kwamba kwa sasa wanawake ndio wanaopata mikopo zaidi kuliko wanaume kwa asilimia 51 na wanaume asilimia 49. Lakini nimuhakikishie kwamba endapo wanawake watakuwa na sifa zinazohusika basi hata asilimia mia tutawapatia. Kwa hivyo ni matarajio ya Wizara kuona hata katika mwaka huu idadi ya wanawake wanaopata masomo ya juu inaongezeka na Bodi ya Mikopo haitosita kutoa mikopo pale wanawake wakapokidhi sifa zinazotakiwa.(*Makofi*).

Lakini pia Mhe. Zulfa Mmaka Omar kazungumzia suala la wadaiwa sugu kwamba wafikishwe Mahakamani, ana siasa kali zaidi kama hivyo. Tuseme tu hadi April 2017 jumla ya wahitimu 4958 walikuwa wamenufaika na mikopo iliyotolewa na uliokuwa Mfuko wa Elimu ya Juu na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Kati ya hao wadaiwa 108 wamemaliza kulipa madeni yao, wadaiwa 14 wamethibitishwa kuwa wamefariki na hivyo kupatiwa msamaha wa kutolipa madeni yao kwa mujibu wa sheria. Wadaiwa 1,387 wanaendelea kulipa madeni yao na wadaiwa 3,449 hawa hawajaanza kurejesha mikopo yao. Bodi hivi sasa inaendelea hatua za kuwaita wadhamini, wakopaji na kuwapa nafasi ya kurejesha mikopo hiyo, baada ya hapo watakaoshindwa watachukuliwa hatua za kisheria kama alivyopendekeza Mhe. Mwakilishi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri malizia unadakika 2 za kumalizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia ningependa kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hii ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na viongozi wake ni walimu na mwalimu siku zote anathamini wazo la mtu yeyote. Kwa hivyo mawazo yenu tutayatafakari, tutayafanyia kazi na tutayachambua.

Naunga mkono hoja ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametujaalia uhai na uzima jioni hii ya leo kuweza kukutana hapa katika Baraza letu Tukufu.

Lakini vile vile nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kufanya majumuisho ambayo yanahusiana na Bajeti na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa Fedha 2017/18.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa hotuba yake aliyoitoa, vile vile pamoja na Wajumbe wake wote, hotuba ambayo iliyotolewa kwa niaba yake na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*).

Vile vile niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu wale ambao wameweza kuchangia moja kwa moja na wale ambao wamechangia kwa maandishi, lakini hasa wale walioweza kuchangia kwa kutupigia makofi ambao walitupa nguvu na faraja kubwa sana, tunakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, napenda sana niwatambue wale wote ambao wamechangia hotuba yetu hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Nitaanza kuwataja wale ambao walichangia kwa njia ya moja kwa moja:

1) Mhe. Abdalla Maulidi Diwani
2) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
3) Mhe. Ali Suleiman Ali
4) Mhe. Suleiman Sarahan Said
5) Mhe. Asha Abdalla Mussa
6) Mhe. Mussa Ali Mussa
7) Mhe. Maryam Thani Juma
8) Mhe. Bahati Khamis Kombo
9) Mhe. Suleiman Makame Ali
10) Mhe. Tatu Mohamed Ussi
11) Mhe. Ahmad Yahya Abdulwakil (Mhe. Ahmad hongera sana kwa kupata uteuzi huu na kwa mchango wako makini, ahsante sana).
12) Mhe. Mohamed Said Mohammed
13) Mhe. Abdalla Ali Kombo
14) Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
15) Mhe. Mussa Foum Mussa
16) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf

17) Mhe. Zulfa Mmaka Omar
18) Mhe. Khadija Omar Kibano
19) Mhe. Masoud Abrahman Masoud
20) Mhe. Ali Khamis Bakari
21) Mhe. Salma Mussa Bilali
22) Mhe. Omar Seif Abeid

Mhe. Naibu Spika, endapo kuna Mheshimiwa yeyote kwa bahati mbaya labda sikumtaja naomba na yeye aniambie ili na yeye niweze au kumtaja aweze kuingia katika *Hansard*.

Vile vile napenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa maandishi :-

1. Mhe. Hamida Abdalla Issa
2. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi (mwalimu huyu)
4. Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mihayo Juma N'hunga)
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa
6. Mhe. Panya Ali Abdalla
7. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
8. Mhe. Shaibu Said Ali
9. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
10. Mhe. Said Omar Said
11. Mhe. Juma Ali Khatib - (Waziri Asiyekuwa na Waziri Maalum)
12. Mhe. Nassor Salim Ali
13. Mhe. Asha Abdalla Mussa
14. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
15. Mhe. Ame Haji Ali
16. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
17. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
18. Mhe. Zaina Abdalla Salum
19. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
20. Mhe. Ali Khamis Bakari
21. Mhe. Naibu Waziri (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum SMZ
22. Mhe. Naibu Waziri (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
23. Mhe. Mgeni Hassan Juma
24. Mhe. Shehe Hamad Mattar

25. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
26. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - ambaye pia alichangia kwa maandishi *(Makofi)*

Wengine napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao na wao walichangia na kusaidia kutoa ufafanuzi kwa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa hapa:-

1. Mhe. Waziri Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
2. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
3. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
4. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
5. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Yeye vile vile ni mwalimu Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri

Wote nawashukuru kwa michango yao ambayo wameweza kuitoa ambayo imesaidia kutoa ufafanuzi kwa hoja zilitolewa na Waheshimiwa Wawakilishi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze kujibu hoja zile ambazo kutokana na muda nitaweze kuzijibu lakini zote ambazo zitakia basi Wajumbe wajue kwamba jawabu zote zipo na nia na madhumuni yetu ni kuweze kutoa ufafanuzi kwa kila hoja ambayo Mhe. Mwakilishi ameichangia.

Lakini kabla sijasema hayo yote napenda sana kusema maneno yafuatayo na maneno haya napenda zaidi ayasikie sana Mhe. Mwakilishi wetu wa Jimbo la Jang'ombe ambaye kwa jana alikuwa mchangiaji namba moja Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mheshimiwa huyu ni Mheshimiwa mweledi sana sote tunamfahamu, bingwa na hodari wa kupenda kujifunza mambo mengi. Ninapenda kusema yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa katika mchango wake alisema kwamba Mawaziri wa Dkt. Ali Mohamed Shein hawako makini na utendaji wa kazi zao. Hili jambo si sahihi na haliko hivyo. Mawaziri wote ambao Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein amewachangua wana dhamira ya dhati, uzalendo, uwezo mkubwa na wamelelewa katika misingi iliyotokana na historia ya TANU na ASP. (*Makofi*).

Vile vile Mawaziri hawa hadi kufikia leo hii wamelelewa vizuri sana na wazee ambao wamelelewa katika misingi hiyo iliyotokana na uzalendo wa dhati

kabisa wa kupigania nchi hii ya kimapinduzi na kulinda heshima ya watu wa nchi ya Zanzibar.(*Makofi*).

Napenda sana kumthibitishia kwamba Mawaziri sote ambao tumechanguliwa na ambao tunakaa katika benchi za mistari zaidi miwili ya mbele ni kwamba sote tuna dhamira na nia kubwa ya kutumikia raia wa Zanzibar na tuko hapa kwa lengo la kutumikia raia wenzetu na vile vile kumsaidia sana Mhe. Mpendwa Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kufuata Katiba, Sheria, Kanuni na miongozo yote ya kiserikali bila ya kusahau Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mamlaka aliyokuwa nayo Kikatiba na Kisheria ana uwezo na Mamlaka ya kutumia vyombo vyote kutumurika sisi wasaidizi wake na kuangalia utendaji kazi wetu. Napenda kumthibitishia kwamba tuko hapa kumsaidia Mhe. Rais pamoja na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar wazalendo na tumeapa na tumeshika Misahafu kutokana na imani ya Dini zetu kuwatumikia wananchi muda wote, wakati wowote. Kutokana na hili napenda niwaambie wananchi wenzangu wa Zanzibar kwamba sisi viongozi ambao Mhe. Rais ametuchagua kumsaidia, tuko kwa ajili ya kuwatumika wao wakati wowote na saa yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee sasa na kuchambua hoja mbali mbali ambazo Wahehsimiwa Wajumbe wamezizungumza.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na Mhe. Asha Abdalla Mussa walichangia sana kuhusiana na majengo ya skuli ambayo yamechangiwa na nguvu za wananchi lakini bahati mbaya sana hayajamaliza kujengwa. Na hii nadhani Waheshimiwa wengi sana wamegusia katika masuala haya na endeapo kama nitakuwa sijamtaja tena, basi athamini kwamba mchango wake vile vile tumeupokea na jawabu ambayo nitaitoa hapa ndiyo itakuwa ni jawabu kwa Waheshimiwa wote ambao wamechangia suala hili.

Katika mwaka huu wa fedha wizara yetu imeweza kukamilisha madarasa 73, afisi 11 na ghala 6 katika skuli 14 na vituo vya walimu 3. Madarasa hayo yamekamilishwa kwa bajeti ya SMZ ya Shs. 350,000,000 na tunatambua kwamba yapo madarasa 285 ambayo yamefikia hatua ya kuezekwa katika skuli mbali mbali na maeneo mbali mbali ndani ya Zanzibar. Nia na madhumuni ya Serikali yetu tufuku kwa mwaka huu wa fedha ni kukamilisha majengo hayo kwa kutumia bajeti ya bilioni 4.6. Kwa hivyo naomba sana Waheshimiwa

Wawakilishi hili suala tayari Serikali inalifahamu sana na tunajua kwamba hiki ni kilio kikubwa sana, kwa sababu sisi sote ni walimu, tunafahamu ugumu wa mwalimu kufundisha darasa likiwa na wanafunzi wengi. Kwa hivyo tunaamini kwamba kwa nguvu na nia thabiti ya Mhe. Rais na taasisi zake ambazo amezichagua basi suala hili nalo litaweza kufanikiwa katika mwaka huu wa fedha na madarasa haya yote basi yataweza kuingiziwa madeski. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif, Mhe. Ali Khamis Bakari pamoja na Mhe. Maryam Thani wao vile walitaka walishauri kwamba hizi fedha ambazo zimechanga kwa ajili ya kununulia madeski zisikae benki na badala yake zikanunuliwe madeski. Mhe. Naibu Spika, tumesikia Waheshimiwa na katika kamati na mimi nilikuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Madeski, suala tayari tushalijadili. Lakini kimoja ni kwamba kweli tumechangia fedha na kuna fedha nyengine kama ambavyo siku ile tulikuwepo baadhi yetu katika ile harambee, si fedha zote ambazo tumeweza kuzipata mikononi.

Mhe. Naibu Spika, fedha nyingi bado ni ahadi ambazo tumeahidiwa na watu mbali mbali, lakini baada ya Ramadhani kati ya mwezi wa Julai tunamini kwamba zitakuwa fedha nyingi zishaanza kupatikanwa. Kwa hivyo tutaweza kununua madeski ambayo yataweza kuingizwa katika skuli zote za Zanzibar. Hivyo Waheshimiwa hichi kilio nacho nadhani karibu kitafika mwisho wake na kama ambavyo Mhe. Rais wetu alisema kwamba hadi ikifika Disemba mwaka huu basi kilio hiki kiwe tayari kimeshamalizika. Mhe. Naibu Spika, tumuamini sana Mhe. Rais kwa hili lakini mutuamini na sisi wasaidizi wake kwamba tunasimamia hizi ahadi.(*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani alikuwa anasema kwamba Skuli yake Kizimbani itajengwa lini au ni stori za kesho kesho. Mheshimiwa napenda nikuhakikishie kwamba kwamba ilivyo UWAWAZA tuko uwazi kabisa na ukweli. Skuli hii pamoja na zile skuli nyengine zote kwa pamoja za ghorofa basi zitaanza kujengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018. Zabuni zote zimekamilika na tunagemea kwamba karibuni tu tutapata idhini kutoka kwa benki ili tuweze kufanya utaratibu wa kuanza na ujenzi. Kwa hivyo Inshallah tumuombe Mwenyezi Mungu kwamba kuanzia mwezi wa saba huko inawezekana ujenzi ukaanza, tutoe mashirikiano Waheshimiwa katika maeneo yetu ambayo ujenzi huu wa skuli utakuwa umepita.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Waheshimiwa walitaka kujua kwamba kwa nini skuli hizi mpya za karibuni tu ikiwepo Skuli ya Mtule zinakarabatiwa kiasi kwamba kuna majengo ya zamani ambayo hayajafanyiwa ukarabati. Ni kweli tunafahamu kwamba hilo tatizo lipo lakini kutokana na mapaa yaliyofanywa

vibaya yamepelekea kuvuja. Kwa hivyo wizara kwa kushirikiana na wahisani wete wakiwemo *Milele Zanzibar Foundation* na Ubalozi wa *Sweden* umeanza kufanyia ukarabati baadi ya majengo ya skuli za zamani. Ile Wizara inafanya kwa sababu hatuwezi kuona kwamba watoto wanavujiwa tukaweza kuwaachia, lakini si Skuli ya Mtule peke yake hata zile nyengine nazo basi hatua kwa hatua tutaweza kuzitengeneza ili vijana wetu waweze kuwa katika mazingira mazuri. Lakini hata zile ambazo za zamani basi kwa kushirikiana na wafadhili wetu tutaweza kuzifanikisha. Lakini vile vile tayari Serikali imetenga Shs.7,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa skuli ambazo tutaanza kwa Skuli ya Lumumba, Ben Bella pamoja na Skuli ya Haile Selasie. Kwa kweli hiyo ni hatua kubwa sana ambayo Serikali yetu tukufu imeweza kuichukua.

Vile vile Waheshimiwa walitaka kujua kwa nini wizara inakadiria bajeti kwa kuzingatia misaada na wafadhili bila ya kujali kwamba uwezo ulivyo wa ukusanyaji. Ni kweli kwamba Serikali inashirikiana na mataifa na mashirika ya kimataifa ambayo yamekuwa yakisaidia sana sekta ya elimu. Wahisani hawa wameahidi kuisaidia nchi zinazoendelea hata kufikia malengo ya *millennium* iwapo mataifa haya yatatenga si chini asilimia ishirini (20%) ya matumizi yote ya Serikali kwa sekta hii ya elimu. Kwa mfano Wizara yetu ya Elimu imeandaa Mpango Mkuu wa Elimu wa miaka mitano na wapo wahisani wengi ambao tayari wameshaanza kujitokeza kuchangia utekelezaji wake. Hivyo pamoja na fedha za Serikali bado tunaendea kupokea misaada kutoka kwa wenzetu misaada ambayo haitakuwa na masharti ya aina yoyote magumu ya kaweza kuathiri maendeleo ya Zanzibar. Kwa hili ni jambo ambalo haliwezi kuepukika sana katika nchi zinazoendelea.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa walitaka kujua kwa nini ujenzi wa Skuli ya Kibuteni umesita, lakini hata Mhe. Waziri Mstaafu wa Wizara ya Elimu akiwa ni Mwakilishi wa Jimbo hilo lakini vile vile na yeye alikuwa na kilio hicho. Ninapenda niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba ni kweli huu ujenzi ulisita ama niseme umechukua muda mrefu, lakini hivi sasa tayari wizara imechukua juhudi ya kusitisha mkataba na yule mkandarasi ambaye alikuwa anajenga ujenzi ule ambaye *United Builders* na baada ya kusitisha mkataba huo, wizara imepeleka maombi kwa benki ambayo ilikuwa inadhamini ujenzi ule, baada ya hapo tumetangaza zabuni tena upya na zabuni hii tayari imeshakamilika kila kitu na tunategemea baada ya muda si mrefu tutaweza kutiliama saini na mzabuni huyu.(*Makofi*).

Kwa hivyo baada ya hapo ni kwamba ujenzi ule nao utaendelea na tunaamini Inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu basi tukija mwakani katika bajeti hakuna tena Kibuteni haijamalizwa, bali itakuwa kwamba Kibuteni wanafunzi

kidogo ama wanafunzi ni wengi, tunaomba sana hili Waheshimiwa mtuamini kwa hilo.

Mhe. Nadir alitaka kufahamu skuli ambazo hazijaezekwa, hazina sakafu, madeski, uzio, vyoo vibovu na mengi mengineyo. Lakini nadhani tayari hili pia nilishalijibu katika suala zima la ujenzi wa skuli pamoja na madeski. Suala la kujitolea limeshazungumzwa na Mhe. Naibu Waziri amefafanua sana, vile vile tumeshauriwa kwamba Wizara kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Wanawake na Watoto kuandaa utaratibu wa kuwachunguza wanafunzi ili kubaini matatizo mapema, tumepokea hilo na tutalifanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo yeye alitupongeza sana na vile vile alipongeza jitihada za wizara katika kusimamia suala zima na michezo na amekuwa tayari kutuunga mkono juu ya hili kwa vile wizara yake pamoja na wananchi wake wa Jimbo la Amani, basi watatusaidia sana katika kusimamia maendeleo ya michezo ndani ya maskuli, tunashukuru sana Mhe. Waziri wa Habari pamoja na sekta yake yote.(*Makofi*).

Mhe. Makame Said Juma yeye alitaka kufahamu na uhaba wa madarasa. Hili nadhani tayari nimeshalitolea ufafanuzi lakini vile vile suala la uhaba wa walimu tayari Mhe. Naibu Waziri amelifafanua.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa alitaka kujua mgogoro uli katika Skuli ya Kiislamu Micheweni umefikia wapi na kama hati miliki imeshapatikana. Napenda nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba mgogoro uliokuwepo katika Skuli ya Micheweni, wazee wanaodai kumiliki eneo hilo wamekubali kuliachia eneo hilo endapo watapewa eneo jengine, na Mamlaka ya Wilaya ya Micheweni tayari imelichukua hilo na inawatafutia hilo eneo na baada ya hapo kwamba kwa yale mashirikiano mazuri na Wizara ya Ardhi basi tayari hati miliki tutaweza kuipata.

Mhe. Shadya aliomba nafasi ya matroni zijazwe hasa Pemba na hili si Pemba tu hata vile vile na Unguja tutalifanyia kazi suala hili. Kwa hivyo zipo nafasi ambazo ziko wazi basi zitajazwa ili mambo yaende vizuri zaidi.

Mhe. Suleiman Makame Ali alitaka kujua kwa nini fungu la fedha kwa Afisa Mdhamini Pemba limepungua. Mheshimiwa ni kwamba fedha hizi zimepungua kwa sababu fungu la mishahara ya walimu wa sekondari na msingi limehamishiwa katika programu husika ya msingi pamoja na sekondari. Hiyo ndio sababu iliyopelekea fedha zile kuweza kupungua, kwa sababu fedha

nyingi ni kundi la mishahara. Kwa hivyo ikitoka mishahara ina maana fedha zinakuwa ni kidogo sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif alitaka kufahamu na alisema kwamba elimu inayotolewa nchini itolewe kwa kuzingatia muelekeo wa dunia. Hili ndio lengo kubwa la wizara yetu na kupitia Sera ya Elimu ya 2006 ambayo tayari tunakwenda kuifanyia mapitio pamoja na mfumo wa elimu kwa kuzingatia malengo endelevu na dunia (STG4), linazingatia suala hilo ikiwa pia pamoja na uendelezaji wa walimu, mitaala, tathmini ya wanafunzi, ufundi wa teknolojia, mafunzo ya amali pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano katika elimu. Kwa hivyo Mheshimiwa ni kwamba ndio njia ambayo na sisi tunaelekea huko huko.

Mhe. Ali Suleiman Ali alitaka kufahamu vitabu vya sekondari vinasemekana vya Tanzania Bara vimeonekana vina dosari, vipi tuko salama? Mheshimiwa sisi tuko salama kwa sababu vitabu vinavyosemekana vina dosari ni vitabu vya msingi na elimu ya msingi si Muungano. Kwa maana sisi Zanzibar tuna vitabu vyetu ambayo viko salama Alhamdulillah na vijana wetu wanavitumia vizuri na kama endapo kutatokezea tatizo lolote basi tunaomba sana mtushauri na mtuambie ili hatua za haraka ziweze kufanywa kwa ajili ya kurekebisha.

Mhe. Maryam Thani suala la mfumo wa elimu alisema kwamba ni tofauti mfumo wa elimu unaotumika Zanzibar na Afrika ya Mashariki. Mhe. Naibu Waziri tayari suala hili alilijibu vizuri sana.

Suala la Vyuo vya Ualimu ambapo pia Mhe.Abdalla Ali Kombo (*captain)* hayupo, alikuwa na masikitiko sana kwa kuondoshwa Chuo cha Ualimu cha Nkurumah. Chuo cha Walimu Nkurumah hakipo, lakini kipo, hakipo jina tu la Nkurumah, lakini tayari pale pale kuna *SUZA* lakini papo hapo kuna Chuo cha Kiislamu Mazizini na Chuo cha Kiislamu cha Kiuyu Pemba.Vyuo hivi vyote vinafanya kazi ile ile ya kutoa elimu kwa walimu wetu. Kwa hivyo Chuo cha Nkurumah kimeondoka jina la Nkurumah lakini yale ambayo yakifanyika Nkurumah bado yapo na yanaendelea.

Sambamba na hili Taasisi ya Elimu Zanzibar ambapo mwaka jana tuliizungumza hapa na vile vile tulipitisha Sheria yake katika Baraza hili hili letu tukufu, kwamba imeandaa tayari mtaala mpya wa walimu wa maandalizi na msingi katika ngazi ya cheti ambayo itaanza kutolewa katika mwaka huu wa masomo yatavyoanza, basi mtaaala huo mpya pia utandelea kutumika. Sambamba hili *SUZA* pia inatoa Stashahada pamoja na Shahada ya Ualimu na

walimu hao hao ndio ambao wanatumika katika maskuli mbali mbali na mazao haya yapo mengi na mimi mmoja wapo nikiwa mazao hayo ya *SUZA*.

Mhe. Nadir vile vile aliishauri Wizara kuwafundisha walimu wake kutumia kompyuta. Kwa kweli sasa hivi walimu tayari ni weledi sana wa kutumia kumpyuta na dunia ya leo sidhani kama kuna mwalimu ambaye hajui kutumia kompyuta hayupo. Kwa hivyo hili suala ni zuri lakini tayari hili suala Wizara tayari imeshalifanyia kazi na walimu wetu tayari wamepatiwa mafunzo haya, walimu 218 kati ya walimu 300 waliweza kupata mafunzo hayo katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Lakini vile vile katika ukurasa 36 na 55 wa bajeti yangu, suala hili vile vile tumelizungumza katika ile Programu Ndogo ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano. Mheshimiwa ukifungua hapa vile vile utaweza kuona zile jitihada ambazo ameweza kuzifanya.

Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Mhe. Nadir walizungumzia kuhusiana na wizi uliotokezea Kwarara. Suala la wizi wa Kwarara tunalifahamu Mhe. Mwakilishi kwa sababu na wewe ni Mwakilishi wa jimbo lile, hata juzi tulililiteta hili suala kwa pamoja na ukaniambia kwamba basi wewe unatangulia mimi nitafuata baada ya kwako wewe. Vifaa vilivyoibiwa pale Kwarara ni kamera mbili, *monitor* moja, *speaker* moja kubwa aina Subofa na kamera ndogo mbili za *CCTV* ambazo zilikuwa katika matayarisho ya kufungwa. Vyote vilikuwa na thamani karibu Shs.26,640,000.

Mhe. Naibu Spika, hatua tulizozichukua sisi wizara ni kuripoti tukio hilo katika Kituo cha Polisi na tayari uchunguzi unaendelea kufanyika katika Kituo cha Polisi cha Fuoni ndio ambao wanasimamia. Kama tutakuwa tuna wasi wasi basi naomba sana tupite Kituo cha Fuoni na tuuulize kuhusiana na tukio hili ambalo limetokezea. Lakini kimoja ambacho bado kinaendelea ni kwamba jengo la kituo hiki bado hatujakabidhiwa rasmi sisi Wizara na nadhani pia Mhe. Naibu Waziri katika maswali na majibu aliwahi kulitolea ufafanuzi suala hili.

Mhe. Naibu Spika, jengo hilo bado hatujakabidhiwa rasmi na mkandarasi ambaye ni *ZECO* na hasara ambayo imepatikana kwa kweli ni kwamba ujenzi kwa kuwa bado unaendelea chini ya dhamana ya mkandarasi, na bila ya pingamizi yoyote mkandarasi alikubali kulipa shilingi 24,640,000 ambazo ni sawa na asilimia 92.5. Mhe. Naibu Spika,alikubali kulipa kwa sababu alikuwa anaamini kwamba wizi umetokezea ndani ya mikono yake, wajenzi wake wapo na hakuna pahala ambapo pamevunjwa kweli. Kwa hivyo ina maana hili jukumu yeye aliweza kulibeba. Lakini sisi Wizara basi maana tuliambiwa

kwamba tuweke walinzi wale wa silaha ndio nia yetu, lakini kwa sasa hivi kwa sababu bado mkandarasi yupo tutakuwa tunamuingilia katika kazi zake, lakini lolote litakalotokea kwa sasa hivi ina maana itakuwa ni jukumu lake yeye mkandarasi kuweza kulibeba na atalisimamia. Kwa hivyo chochote kitakachotokezea tutakuwa tuko sambamba na yeye kuhakikisha kwamba kinarudi na vifaa vyetu vinabaki kuwa katika hali ya usalama.

Mhe. Shaibu Said Ali aliomba kwamba Wizara izingatie zaidi programu ya maandalizi na msingi. Kwa kweli Mheshimiwa ndio lengo letu kubwa hilo sana katika kusimamia na ndio maana sasa hivi imekuwa ni lazima elimu ya maandalizi kutolewa kwa vijana wetu. Na ndio maana mfumo wetu umekuwa 2, 6. Kwa maana ya kwamba lazima kila mtoto apitie elimu ya maandalizi. Hiyo sio hiyari bali kwa sasa ni elimu ya lazima.

Mhe. Rashid Makame Shamsi pamoja na Mhe. Suleiman Sarahan Said walitaka kufahamu maeneo ya ugatuzi katika Sekta ya Elimu hasa ni yepi. Ni yepi ambayo yamegatuliwa yaliokwenda Tawala za Mikoa. Maeneo ambayo yamegatuliwa kwa skuli za maandalizi na msingi ni masuala yote ambayo yanahusiana na malipo ya umeme, maji, matengenezo madogo madogo, uandikishaji wanafunzi, malipo ya posho na nauli kwa walimu, maposho kwa Maafisa Elimu Wilaya na Mikoa, kufanya malipo ya fedha za uji kwa skuli za maandalizi zile za serikali yote yatasimamiwa na yatakwenda katika ugatuzi. Kwa maana haya yote yamegatuliwa. Lakini yako masuala mengine ambayo Wizara itaendelea kuyasimamia ikiwemo uendeshaji, usajili, mitaala bado wizara itasimamia, sera na utafiti, mitihani, lakini vile vile na masuala yote ya ujenzi wa maskuli basi wizara itaendelea kusimamia. Kwa hivyo hayo mambo mengine yamegatuliwa na mengine bado yamebaki katika Wizara na ndio maana tukiangalia katika lile fungu kuna watu wamehoji kwa nini fungu limepungua. Fungu limepungua kutokana na baadhi ya fungu limegatuliwa vile vile nalo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Asha Abdalla Mussa vile vile alitaka kujua sababu zinazotokea uhaba wa walimu katika Skuli ya Kilombero. Lakini na hili nalo tayari nadhani tumeshalizungumza, lakini katika skuli yake vile vile ya Mgonjoni pale nadhani pia imebahatika kupata walimu wapya katika ile skuli kutokana na ile ahadi ya Mhe. Rais ambayo aliiweka kwamba lazima wale viojana walioko pale wataajiriwa. Lakini na haya mengine sambamba na kwengine basi uajiri utakapofanyika vile vile walimu wengine nao wataongezwa katika maskuli. Vile vile wizara yetu inafanya tathmin ya kuona maeneo gani ambayo pengine yana walimu kidogo sana na yepi yana walimu

wengi ili kuweza kupunguza lile fungu la walimu ambao wamezidi katika maeneo mengine ili kuweza kusaidia katika baadhi ya maeneo.

Vile vile alitaka kufahamu kwa nini walimu wa madarasa ya msingi wanapangiwa kufundisha madarasa ya maandalizi. Mheshimiwa ni kwamba katika kuimarisha utolewaji wa elimu ya maandalizi wizara kwa kushirikiana na Madrasa Ali Shaib Programu imewapatia elimu mwalimu wa msingi. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kuweza kupata mbinu za kuwafundisha watoto wadogo wa madarasa hayo. Mheshimiwa hawashushwi hadhi wala hawashushwi kiwango. Kama mwalimu ana *certificate*, kama ana *diploma* ataendelea kutambuliwa kwamba ni mwalimu wa *diploma* na maslahi yake yatazingatia kiwango chake cha elimu na sio darasa ambalo anafundisha. Lakini kuwashusha wale walimu yote ni katika kujenga ile elimu ya maandalizi ili iwe ni elimu nzuri zaidi yenye kiwango kikubwa sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said na yeye vile vile aliuliza suala ambalo linafanana na hili pamoja na Mhe. Yussuf Hassan Iddi wa jimbo la Fuoni, wote wamezungumzia katika masuala mazima ya elimu ya maandalizi nadhani tayari tumeweza kuwajibu.

Mhe. Said Omar Said wa Wingwi amesema kwamba baadhi ya skuli hazina sekondari, kwa hivyo huwafanya watoto waweze kwenda katika masafa ya mbali. Mheshimiwa ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuhakikisha upatikanai wa elimu bora kwa wananchi imehakikisha kila panapokuwa na haja na uwezo wa raslimali kama vifaa vya kufundishia, walimu wenye sifa na uwezo, wizara hujenga skuli za sekondari. Katika kuwaondolea usumbufu wanafunzi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakamilisha majengo yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kuwafungulia skuli wanafunzi karibu na maeneo wanayoishi pamoja na kuwapatia raslimali hizo na miundombinu ambayo inahitajika. Hata hivyo Mheshimiwa kwa kuwa na yeye ametupa kilio chake basi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itakuja itaangalia kuona idadi ya wanafunzi wa sekondari ambao wako hapo ili tuweze kuwawekea sawa na wao wasipate usumbufu wa aina yoyote.

Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mwenyekiti wa Baraza alisema kwamba kuna skuli nyingi sana zimejengwa za wilaya dakhalia lakini hakuna na sehemu za kupikia na kulia chakula kwa wanafunzi hao. Ina maana hii ni kusema kwamba anakiri kuwa baadhi ya dakhalia zipo na ndio maana akasema hakuna sehemu za kupikia chakula. Lakini hata kwa zile ambazo hakuna, kwa hivyo katika utoaji na upatikanaji wa elimu bora dakhalia kuwepo ni jambo la msingi sana na inasaidia kupatikana elimu kwa utulivu, kusoma kwa salama na vile vile bila ya

usumbufu kwa sababu mwanafunzi anakuwa yupo katika mazingira ambayo ni karibu na skuli. Hata hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inazisimamia na kusaidia dakhalia zilizopo ili wanafunzi waweze kujifunza vizuri sana, na tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumepata usaidizi wa kutoka kwa ndugu zetu mbali mbali ambao wanasaidia katika dakhalia hizi, kwa mfano kama Utaani, *CCK*, Kengeja, Ufundi, Mohamed Juma Pindua, *Fidel Castro*, skuli zote hizi ambazo zina dakhalia basi zinapata misaada mingi tu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na hivi juzi juzi tu tarehe 30 Aprili, tulipata msaada mwengine kutoka kwa mfanyabiashara mmoja ambaye alitusaidia sana masuala ya chakula na mambo madogo madogo, ambapo skuli zote hizi ziliweza kufaidika. Serikali vile vile inaangalia namna ambavyo itaweza kujenga dakhalia nyengine ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wake waliopo.

Mhe. Omar Seif Abeid aliuliza kwa nini tunataka kujenga ukumbi badala ya kujengwa uzio. Mheshimiwa ni kwamba uzio ni muhimu sana lakini kwa Skuli ya Konde maandalizi ukumbi una umuhimu mkubwa sana. Kwa sasa skuli hiyo ina vyumba vya madarasa viwili tu na kama tunavyoelewa kwamba mahitaji ya madarasa ya maandalizi ya Konde ni makubwa. Kwa hivyo ukumbi utatumika kwa madarasa ya michezo ya ndani, chakula pamoja na shughuli nyengine za kitaaluma. Tunashauri sana jamii zinahitaji kuhamasishwa zaidi kutunza raslimali zilizopo katika maeneo yao yakiwemo ya skuli. Wizara yangu ina mfano halisi wa kujenga uzio katika Skuli ya Kiuyu Maandalizi lakini jamii iliuvunja wote kwa sababu sijui kama hawakujali au ndio wameghafilika. Kwa hivyo tunaomba sana kwamba kwa zile sehemu ambazo tayari uzio umejengwa basi tushirikiane kulinda raslimali ambazo zimo ndani ya maeneo yetu ya skuli.

Suala hili vile vile limeulizwa na baadhi ya Waheshimiwa wengi suala la uzio. Wizara inatamani kujenga uzio kwa kila skuli, lakini tukiangalia kipaumbele kikubwa ni nini. Mhe. Naibu Spika, tukijenga uzio kuna madarasa ambayo yanahitaji kuezekwa, kipi mwanzo, uzio au madarasa. Waheshimiwa naomba nikuachieni hilo swali japo mtanijibu kwa maandishi na mimi. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Omar Seid Abeid alisisitia suala zima la kujengwa nyumba za walimu katika Kisiwa cha Kokota. Ni kweli Mheshimiwa Kokota kuna mahitaji hayo ya kujengwa nyumba lakini tuna visiwa vingi pamoja na skuli zilizopo maeneo ya kando kando ambayo yote yanahitaji nyumba hizo. Wizara imeweza kuwasaidia walimu hao magodoro na kuwatengea chumba kidogo kimoja cha kulala. Wizara yangu tayari imeanza kazi za ujenzi katika visiwa kidogo kidogo kulingana na uwezo wetu wa kifedha katika kisiwa cha Fundo ambayo iko

zamani. Lakini pia tumefanya ukarabati mkubwa na kupeleka magodoro ya kutosha. Katika jitihada hizi vile vile katika baadhi ya visiwa vyengine basi kadri hali ya uwezo itakavyoruhusu tutaweza kujenga hizo nyumba lakini hatua kwa hatua kadri hali itakavyoruhusu. Lakini Waheshimiwa Wawakilishi kwamba kwa yule ambaye Mfuko wake wa Jimbo ukiruhusu basi si vibaya vile vile akatusaidia katika suala zima la ujenzi wa hizi nyumba.

Mhe. Nabu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na Mhe. Suleiman Sarahan walisema suala zima la kuweko ama kukaa nje kwa wanafunzi katika maeneo ya skuli na vituo vya daladala. Mheshimiwa ni ukweli usiopingika kuwa katika baadhi ya maeneo ya skuli huonekana wanafunzi wakiwa nje ya maeneo ya skuli. Hii inasababishwa na mambo mbali mbali likiwemo suala zima la kuchelewa kwa wanafunzi kufika kwa wakati skuli. Kwa hivyo baadhi ya wanafunzi huwa wanakimbia masomo yao hata kama wanafika skuli mapema. Hii yote inapelekea wanafunzi kuwa katika mazingira ya nje na hasa ukija katika *Jamhuri Garden* wanafunzi wengi utawakuta wanasambaa katika maeneo yale ya karibu, kwa hivyo hujui wanafunzi hasa wa skuli gani lakini unakuta pale wanafunzi wengi. Wizara inatoa wito sana wa kuwataka wazee kutoa mashirikiano ya karibu sana na skuli wanazosoma watoto wao na tufuatilie mienendo ili tuweze kubaini ni mwanafunzi gani yupo skuli, muda gani na mwanafunzi mda gani hayupo skuli, vyenginevyo watoto wetu watakuwa wanapotea, wataharibika bila ya kufahamu tukiamini tu kwamba wako katika maeneo ya skuli.

Mhe Masoud Abrahman Masoud ameuliza wizara ina mpango gani na inashirikiana vipi katika kukitumia Kituo cha Mafunzo cha Michezo cha Dole. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ipo karibu sana na kituo cha mafunzo ya michezo kinachomilikiwa na Kamati ya *Olympic* Tanzania kwa mashirikiano ya Jumuiya ya Maendeleo ya Michezo ya Dole na miongoni mwa wanamichezo waliosajiliwa kituoni hapo ni wanafunzi wetu kutoka katika skuli zilizozunguka kituo hicho. Skuli hizo ni pamoja na Kizimbani, Dole, Langoni, Mwenge, Kianga, Machui pamoja na skuli nyengine za karibu. *(Makofi)*

Shughuli za michezo kama vile mafunzo na mashindano zinafanyika vyema na zinawashirikisha walimu wa michezo na wanafunzi kutoka katika skuli hizo ambazo nimezitaja. Aidha wanafunzi na walimu wanapata fursa mbali mbali zikiwemo za ushiriki wa mashindano ya *Sumsung Youth Games* yenye mnasaba wa kuibua na kukuza vipaji vya mpira wa miguu na kuendeleza utamaduni wa nchi yetu ndani na nje ya nchi, na tayari kupitia kituo hiki zaidi ya vijana wanne wamepata nafasi ya kushiriki katika Timu ya Taifa ya Vijana ya Zanzibar. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa kwamba wizara yangu

itaendelea kutoa kila aina ya mashirikiano ili tuweze kuwapata akina Mbwana Samatta wengi zaidi.

Mhe Naibu Spika, suala jengine ambalo Mhe. Rashid Makame Shamsi mwalimu huyu, alitaka kujua na alitushauri namna ya kujenga viwanja vya michezo katika eneo la *SUZA* ili kozi ile ya *PEU* iweze kuendeshwa katika maeneo ya karibu na *SUZA*. Suala la *SUZA* kuwa na viwanja vyake kwa ufanisi wa kozi ya Stashahada ya michezo ni moja ya kipaumbele cha *SUZA*. Kwa hivi sasa tayari chuo kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa China wamekubali kujenga viwanja mbali mbali vya michezo vya kisasa vikiwemo vya mipira ya miguu, mpira wa kikapu na mpira wa pete. Mhe. Naibu Spka, tayari wameshatembelea sehemu mbali mbali za *SUZA* kwa ukaguzi wa awali na sisi tunasubiri waje wafanye uchambuzi yakinifu na *SUZA* ina maeneo makubwa na jambo hili linawezekana sana kufanyika tuwe na subra Mheshimiwa hili *In shaa Allah* nalo litaweza kufanikiwa.(*Makofi*).

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na Mhe. Ali Suleiman Ali walitaka kujua utaratibu gani unatumika wa kuwezesha *SUZA* kujiendesha baada ya kuunganishwa na taasisi nyengine tatu. Lakini vile vile walihoji kwa nini ile bajeti ya *SUZA* iko *ten billions* na isiwe *twelve billions.* Nadhani Mhe. Naibu Waziri pia alilijibu suala hili, lakini kabla ya kuunganishwa na taasisi nyengine *SUZA* serikali ilikuwa ikitoa ruzuku kwa ajili ya mishahara tu, fedha za kujiendesha zilitokana na ada ambazo wanatoa wanafunzi. Baada ya kuunganishwa na taasisi tatu bado utaratibu utaendelea kama ambavyo ulikuwa unaendelea kwa kutoa ruzuku ya mishahara. Hii shilingi bilioni kumi ni kwa ajili ya hiyo mishahara, kwa sababu hapo awali *SUZA* tukiangalia katika ile bajeti ya mwaka jana utakuta ilikuwa ina kama 6.2, lakini mwaka huu imekuwa na *ten billions*. Kwa hivyo hii yote ni ile ruzuku ambayo imeongezeka kwa ajili ya mishahara ya wale wafanyakazi wengine ambao wameongezeka ndani ya *SUZA* kutoka katika taasisi nyengine. Lakini yale masuala mengine ya uendeshaji basi yote hutokana na malipo ambayo wanafunzi wanalipia.

Mhe. Naibu Spika, lakini serikali ikiona kuna haja, kuna upungufu basi itaweza kuongeza ruzuku ya mishahara endapo itatokezea jambo hili. Ila kwa sasa ile bajeti ambayo imewekwa inatosheleza kwa ajili ya mishahara ikiwemo pia na ongezeko jipya la mishahara ya wafanyakazi wa *SUZA*.

Vile vile Mhe. Shehe Hamad Mattar alitoa ushauri kwamba *SUZA* kuelekeza katika utafiti wa sehemu kubwa kwa lengo la kuongeza mapato. Mheshimiwa ni kwamba utafiti kwanza ni kazi moja ambayo Chuo Kikuu inakuwa inafanya. Lakini ushauri wake tumeupokea na utaweza kufanyiwa kazi zaidi. Lakini

tayari *SUZA* inafanya tafiti mbali mbali na wako baadhi ya wahadhiri wengi wanakuwa wanakwenda hata nje ya nchi kwenda kuwasilisha zile *projects* ambazo wanazisimamia kutokana na tafiti ambazo wanazifanya.

Mhe. Mtumwa Peya vile vile alisema kwamba *SUZA* walihitaji *twelve billions*, nadhani tayari nimeshamjibu Mheshimiwa na naamini kwamba ameridhika sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri umebakiza dakika tatu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana. Mhe. Naibu Spika, nikushukuru maana dakika tatu najua siwezi tena kumaliza.

Waheshimiwa kama ambavyo niemeeleza awali ni kwamba michango yote ambayo mmeitoa kwa ajili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumeipokea, yote majibu yake tunayo nadhani nyote ni mashahidi mnaona, lakini wakati ukuta, Mheshimiwa Mzee wa ukuta yupo. Hatuwezi kumaliza kuzunguza yote ambayo yamechangiwa hapa, lakini tuseme kwamba michango yote tumepokea na yote itaingia katika *hansard* ili kila mmoja aone kwamba mchango wake hatujaupoteza.(*Makofi*).

Kuna Mhe. Salma Mussa Bilal na wengine wengi hapa Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, michango yao yote ipo na yote itapelekwa iingizwe katika *hansard* ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi lakini vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango yao mizuri na ya kujenga. Pongezi ambazo wametupa Waheshimiwa tumezipokea, Waswahili wanasema: "Mgema akisifiwa tembo hulitia maji", lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haiko huko. Sisi tunasema kwamba sifa ambazo mmetupatia ina maana hii ni kutupa hamasa na mori na ari ya kusema kwamba tufanye kazi zaidi ambavyo tunafanya. Hili tunawahakikishia kwamba tutafanya kazi zaidi, kwa nguvu zaidi, kwa kasi zaidi, kwa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuzingatia kauli yetu elimu bora kwanza iweze kufanikiwa sana. Tunakushukuruni sana kwa michango ambayo mmetupatia. *(Makofi)i*

Mhe. Naibu Spika, lakini Mheshimiwa wa Jimbo la Ole ukuta ni muhimu sana na ndio maana hata nyumba siku hizi ukijenga nyumba yako hata kama ndogo

ya kiwango gani, muhimu kuiwekea ukuta, bila ya hivyo usalama unakuwa ni mdogo. Kwa hivyo tunakushukuru sana kwa kulisema hilo.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri toa hoja.

Baada ya hayo Waheshimiwa tunakuombeni sana tupitishe bajeti yetu hii ili maendeleo ya elimu Zanzibar yaweze kufanikiwa sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imeshatolewa wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wasiokubali, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitia vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

Fungu K01	**-**	**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**	
Kifungu K0101		Idara ya Mipango Sera na Utafiti	143,093,000
		Jumla Kuu	**143,093,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PK0101 Elimu ya Maandalizi na Msingi

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia maslahi ya walimu wa maandalizi na nikasema kwamba elimu inaanzia kule msingi wa elimu ya awali kwenye maandalizi.

Nikasema maslahi ya waalimu wa maandalizi nilishauri kwamba iongezwe pesa ambayo wanapata sasa hivi na kazi kubwa walionayo ni ndogo. Kwa hivyo naona sijapata majibu yoyote Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo tulizungumza awali kwamba baadhi ya majibu mengine hatukuweza kuyasema kutokana na uchache wa muda. Lakini katika Elimu ya Maandalizi na Msingi maposho ya masuala mengine yote kama ambazo Mhe. Waziri wa Sheria, Katiba na Utumishi wa Umma alieleza ni kwamba wanayafanyiakazi na watakapokuwa tayari basi na wao vile vile wataweza kupatiwa.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri lakini leo hapa ndio tunapisha hii bajeti, na kama nilivyosema kwamba bajeti hii sasa hivi ikipita kule nyuma kuna baadhi ya walimu maslahi yameshakuwa mazuri. Lakini hawa walimu wa maandalizi tukisema ndio kwanza tunajiandaa ni lini ambao kwamba na wao watajisikia angalau maana si mshahara lakini lile posho angalau kuongezwa.

Mimi naona Mhe. Mwenyekiti, angalau nipate majibu mazuri ili niweze kuachilia hichi kifungu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti**,** namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake na ni sahihi na nilitoa kauli hiyo kweli kwamba kila ambapo pana matatizo tuletewe na sisi tutayashughulikia kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo kusiwe na mashaka hayo.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Sijamsikia hivyo, mimi Mhe. Waziri maana anasema kidogo...

Mhe. Mwenyekiti: Aaah! hujasikia Mheshimiwa ameshakujibu, amesema pale ambapo kila patakapotekea matatizo watayashughulikia kutokana na sheria zilizokuwepo. Ndilo jibu ambalo ametoa.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Mwenyekiti, matatizo ndiyo yapo hayo, pesa ni elfu ishirini hayo ni matatizo ambayo si madogo. Kwa hivyo tunahitaji kwanza tuambiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa hili tatizo umeshalizungumza na serikali ipo imeshalisikia ndio watakapolishughulikia watalishughulikia madhali umeshalizungumza sawa, tuendelee.

Mhe. Suleiman Makam Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme sina buti labda itakuwa ni "kiyebo yebo" tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipochangia nilizungumza kwamba walimu walioko maskulini kwenye skuli za msingi ndio waliopangwa hao hao kusomesha maandalizi ambao kwamba muda ule huwa hautoshi kwa vile vipindi wanavyopangiwa. Nilitaka kujua hapa kwa sababu sikusikia kwamba kuna hatua gani zitachukuliwa ili kuwaongeza walimu au kuwaajiri wale walimu wa kusomesha *specially* kusomesha maandalizi, nilitaka kujua hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika utaratibu wa usomeshaji maskulini mwalimu anaweza akatolewa ngazi yoyote akapelekwa ngazi yoyote kusomesha *provided* anazo sifa za kufanya hivyo na hivyo ndio wizara inavyofanya. Kwa sasa ni kwamba tunawateremsha chini baadhi ya walimu wa msingi kwenda kusomesha maandalizi huku wakipatiwa mafunzo madogo madogo.

Lakini hata hivyo, karibuni tutaajiri walimu wa msingi wakiwemo pia na maandalizi.(*Makofi*).

Mhe. Suleimba Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hilo ni jibu zuri na nimeridhika vya kutosha na nadhani Baraza zima hili limeridhika. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PK0101	Elimu ya Maandalizi na Msingi	70,724,571,000
Kifungu PK0102	Elimu ya Sekondari	63,496,813,000
Kifungu PK0103	Elimu ya Juu	

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilimwambia Mhe. Waziri anipe utaratibu au maelekezo kuhusu kile Chuo cha Kufundishia Ndege na Urubani sijui na Uhandisi. Kwa hivyo sikupata maelekezo, hivyo nilikuwa naomba ufafanuzi kidogo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Chuo ambacho anachosema kinafundisha masomo ya

Urubani wa Ndege ambacho kinatolewa na Taasisi ya Karume kimesajiliwa kwa sababu kile Chuo ni cha zamani, kozi imeanza ni mpya lakini kozi hii imeshajiliwa chini na *NACTE.* Ahsante sana.

Mhe. Suleimba Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, sawa kimesajiliwa lakini nilikuwa naomba niongezee maelekezo kwamba je, *certificate* zake zitakuwa zinajulikana au pamoja na kwamba kimesajiliwa wapi kimesajiliwa Zanzibar au kimesajiliwa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoja ya msingi imeshajibiwa amesema kimesajiliwa chini ya *NACTE* na *NACTE* maana yake kinatambulika, ndio maana yake.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, hapa tunavyo Vyuo vinakuwa vinasajiliwa lakini matokeo yake kwa sababu tunasimamiwa na Jamhuri ya Jamhuri ya Muungano, wale watu wa vibali wa Jamhuri wa Muungano wanaweza wakasemaa kwamba hichi sisi hatukitambui. Sasa hichi kinatambuliwa na mawasiliano ambayo nikisema miundo mbinu ya Bara katika Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, tunavyosema *NACTE* maana yake ni Taasisi ambayo inasimamiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo bila ya shaka inatambuliwa kwa sababu ipo chini ya sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo kama ana mashaka zaidi itakuwa ni mashaka ya kibinadamu lakini kiilivyo ni kwamba inatambulika Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zote zinafuatwa na zinazingatiwa, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kabisa sina ya kuzuia fungu leo nimeridhika sana, lakini nilikuwa nataka ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilipeperusha baadhi ya vitabu vya bwana wetu Abeid Aman Karume na nikaeleza jinsi ya upotoshwaji wa historia katika mitandao lakini vile vile nikaelezea Kigoda cha Karume. Kwa sababu Chuo Kikuu *UD* kuna Kigoda cha Mwalimu Nyerere. Lakini kwenye Chuo chetu Kikuu kuna Kigoda cha Mfalme Qaboos tu hakuna hichi Kigoda cha Abeid Aman Karume.

Nilitaka nipate tu ufafanuzi serikali ina mpango gani na kwa sababu hiyo wakati wa Uwaziri wa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, Profesa Ali Mzee Ali alichangia na akamwamba Waziri yuko njiani kufanya Kigoda kile. Nilikuwa nataka kupata ufafanuzi wamefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hili ni pendekezo analolitoa Mheshimiwa na kwa kweli ni pendekezo zuri na sisi viongozi ambao tupo sasa hivi tutaanza kulifanyia kazi na pengine tukija mwakani utatuuliza suala jengine zaidi. Lakini kutunza historia ya viongozi ni jambo muhimu sana katika jamii yoyote. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Naibu Waziri na maana yangu ni kuwaenzi kwa vitendo tusiwaenzi kwa maneno. Naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu PK0103	Elimu ya Juu	23,413,375,000
Kifungu PK0104	Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali	17,151,057,000
Kifungu PK0105	Ubora wa Elimu	

Mhe. Mwenyekiti: Maryan Thani Juma baadae atafuata Mhe. Ali Khamis Bakari atafuata Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika kifungu hichi nimehoji fedha ambazo ni shilingi milioni mia moja na ishirini kwenye ukaguzi wa elimu ambazo nimeuliza kwamba ni shughuli gani fedha hizi zilizopangiwa hadi kufikia ongezeka la asilimia mia moja. Mhe. Waziri nataka majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hili suala wakati tunajibu katika majumuisho Mhe. Naibu Waziri alilijibu, inawezekana Mheshimiwa hakulisikia ila kwa faida ni kwamba kifungu hichi kimeongezeka cha uchaguzi kutokana na kwamba tunaanzisha ule ukaguzi wa Kanda. mambo kama haya wengi walivyochangia mwaka jana waliseme walishauri kwamba uchaguzi wa Ukanda na tayari wizara imefanya hicho kitu cha uchaguzi wa Kanda ili kuweza kuweza kufanikisha hilo lifanyike, ndio maana zile pesa zimeweza kuongezeka. Lakini sambamba na hili kuna sheria ya ukaguzi ambayo ipo mbioni kumalizika.

Kwa hivyo, ili sheria ile ufanye kazi yake vizuri kuna mambo lazima yataongezeka. Kwa hivyo lazima bajeti yake iongezeke ili kufanikisha ufanyaji wa kazi mzuri wa ukaguzi wa elimu. Ahsante sana.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na tuendelee.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia niuliza masuala ya walimu pamoja na kwamba Mhe. Waziri alishatujibu katika kipindi hichi kama kuna walimu wataajiriwa sijui nimesahau kidogo Pemba na Unguja. Lakini nilizungumzia kule Kaskazini "A" Unguja kama kuna walimu 83 Mkoa mmoja tu hakuna. Sasa je, hapa nilitaka kujua katika kipindi hichi cha bajeti ambacho utaajiri.

Je, ni walimu wangapi ambao utawasaidia katika Mkoa ule.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, idadi ya walimu hasa wangapi wataajiriwa nadhani katika bajeti yetu tumezungumza walimu wangapi wataajiriwa. Lakini kuajiriwa kwa walimu hao vile vile bado inategemea na upatikanaji wa fedha kwa serikali. Kwa Mkoa wa Kaskazini si peke yake ambako kumelalamikiwa uhaba wa walimu ni kwamba kote zoezi la uajiri litakapofanyika, kila sehemu wataajiriwa walimu.

Lakini hivi juzi tumetoa tangazo la ajira kwa walimu ili kuweza angalau kuziba zile nafasi za walimu ambao wamestaafu na waliofariki na ikiwemo Kaskazini na Kaskazini "A" pia imo. Hasa kama Mheshimiwa labda lile tangazo hajalisiki basi vile vile ningemuomba sana hata kwenye mitandao ya kijamii kuna watu wameliweka tangazo ambalo Tume ya Utumishi Serikalini imeliweka. Kwa hivyo kutokana na kujaza nafasi zile ni kwamba kusaidia ule uhaba wa walimu wa Kaskazini lakini na Mikoa mengine yote ambayo ina uhaba wa walimu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Tuendelee Mheshimwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti, makini. Lile suala langu tayari nimepata jibu baada ya suala alilouliza Mjumbe aliyepita. Naomba tuendelee. (*Makofi*).

Kifungu PK0105	Ubora wa Elimu	6,074,270,000
Kifungu PK0106	Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu	16,430,090.000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Makame Ali na atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa tena nafasi hii ikiwa ni mara ya pili kwa kutaka ufafanuzi na kujua pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani pamoja na Wazanzibari kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye HK01060201 Kupanga na kusimamia kazi za wizara kwa mfuko maalum kusaidia huduma za elimu.

Hapa nilizungumzia kuhusu suala la upatikanaji wa huduma za maji maskulini pamoja na vyoo. Nilitaka hili Mhe. Waziri anipe ufafanuzi lakini pia vile vile kwenye kuratibu shughuli za wizara Pemba nilizungumzia kuhusu mzozo wa Skuli ya Ndagoni ambao kwamba katika majibu nilisikia Mhe. Bihindi Hamad Khamis tu ndiye aliyejibiwa, kuhusu Skuli ya Ndagoni sikupata majibu.

Kwa hivyo nilitaka kujua kwamba Mhe. Waziri tunakwenda kwenye bajeti ya pili hii. Je, mzozo ule wa Skuli ya Ndagoni wale wananchi waliotoa lile eneo kwa moyo thabiti, kwa nia njema imefikia hatua gani ili kuwapatiwa ile fidia yao ambayo kwamba Mhe. Waziri tulikuwa tunagongana gongana hapa katika muuliza masuala na akaunda kamati. Naomba majibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mheshimiwa kuhusiana na suala lake la maji, vyoo nadhani tulipokuwa tukizungumza kuna Mwakilishi aliuliza suala zima kuhusu maeneo ambayo yamegatuliwa na miongoni mwa mambo ambayo yamegatuliwa basi lilikuwemo suala zima la matengenezo kama haya ya maji miundombinu hii midogo midogo ni kwamba ule ugatuzi kwa zile Halmashauri ambazo zitapelekewa zinaweza kufanya kazi hii.

Kwa maana suala hili nalo litahamia katika ugatuzi, na suala la Ndagoni kwamba sisi wizara tumeunda Tume Maalum ya kuchunguza suala hili na hii ilitokana kwamba zile nyaraka ambazo zilipatikana mwazo zilikuwa zina utata kwa yule ambaye alisema kwamba ni hati yake, aliyesema hati yake lakini nyaraka alizoleta ni za shamba jengine. Kwa hivyo baada ya kuona mzozo ule tukaona mzozo ule tukaona bora tuunde timu maalum ya kuweza kuchunguza lile suala la ripoti yake itakapokamilika basi tutaileta. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali hilo kwamba kamati iliundwa na nilikubali hilo. Lakini na wale walioundiwa kamati walithibitisha, wale walioundiwa kamati kule walioambiwa kwamba lile

eneo ni la wao wengine sio wale waliotoe lile eneo na wao pia waliufyata walikimbia maana walijificha wakarudi nyuma nyuma ikawa wanapeleka sema wewe, sema wewe.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majibu aliyonijibu Mhe. Waziri kwamba ameunda kamati na inavyotakikana ni majibu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee lakini ni kwamba nasubiri majibu yangu na sitolisahau hilo mpaka nitoke humu kwenye Baraza litalisimamia Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. leo sina nia kabisa ya kuchukua mshahara wa Waziri lakini nilikuwa naomba ufafanuzi tu, wakati nikichangia nilitaja baadhi ya waandishi wa vitabu, wataalamu wetu na nilitoa idadi ya vitabu 47 ambavyo hivyo kwa muda tu wamevitunga hapa Zanzibar, lakini vyengine vinatumika Bara vyengine vinatumika Kenya hapa havitumiki.

Nikamuuliza, Mhe. Waziri kuna nini, tangu enzi za Waziri wa Kwanza Waziri makini Mhe. Haroun Ali Suleiman mpaka kufikia Waziri huyu aliyekuweko sasa mpaka sasa hawajaitwa wala kukaa pamoja na watu wale. Mimi nilikuwa nataka nipate tu ufafanuzi wa wataalamu wetu ambao tumewafundisha kwa gharama kubwa halafu tunaviacha hatuvitumii. Nilikuwa nataka kupata ufafanuzi tu.

Ni lini wanaweza wakakaa nao pamoja wakanijumuisha na mimi niweze kuona hali halisi yao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nashukuru sana kwa ushauri na mchango ambao Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) ameutoa, ni kwamba maana yake niliona mwanzo kama anachanganya masuala mawili. Mwanzo suala la vitabu kutumika, lakini pili swala la wale waandishi.

Suala la waandishi ni kwamba kwa sababu kama nilivyowataja wapo wengi na wengine kama hatuwajui vile vile tutashirikiana na yeye ili aweze kututambulisha walipo tuweze kuwapata wote.

Baadhi yao tumeweza kuwaita lakini tutawaita wengi wengi ili tuweze kupata maoni yao, na mambo mbali mbali hasa ambayo yanahusiana na masuala ya utunzi wa vitabu.

Lakini suala la vitabu vile vile navyo ambalo uligusia gusia ni kwamba vitabu vile vinatumiwa na Sekondari hasa katika maeneo ya fasihi basi vitabu vinatumika vya waandishi wa Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman ulikuwa hujasimama wakati wengine wanasimama, sisi tuna *register* mtu akisimama. Mheshimiwa zungumza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufafanuzi zaidi wa Waziri kwa sababu nilimwambia kwamba skuli zangu za mjini ambazo za Chake Chake, Madungu, Kongwe, Michakaeni, Chanjaani hali zake ni mbaya na haziwezi kuendelea sasa hivi kutokana na hali za vyoo, hawana *total* hawana vyoo wala maji.

Lakini hapa Mheshimiwa alizungumza habari ya ugatuzi, nilikuwa nataka nijue kwamba hii ni hali ya dharura kwa muda huu keshagatuka yeye, ameshampisha Waziri wa Serikali za Mitaa au bado naendelea na yeye mpaka atakapogatuka.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mchango wako uliochangia ulielekea huko au unauliza tu kwa sababu Mheshimiwa kajibu, eeh!

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nilichangia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mheshimiwa Suleiman Sarahan Said ni kwamba ugatuzi utaanza katika mwaka mpya wa fedha kama tulivyozungumza 2017/2018, na ambao utamalizika mwezi wa Juni.

Sasa kutokana na dharura kwa sababu hiyo anayosema ni kwamba kutokana na athari ya mvua kuna baadhi ya miundo mbinu mengine imeharibika, hilo tunalifahamu.

Lakini kutokana na bajeti ya hapa bado tunaendelea nayo kumalizia, nayo basi tutafanya ukarabati baadhi ya maeneo hasa ya muhimu ikiwemo vyoo na miundo mbinu mengine ya maji ili kuweza kufanya ukarabati ili watoto wetu waweze kusoma katika mazingira yaliyokuwa mazuri na bora kabisa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu Pk0103 Elimu ya Juu	6,074,270,000
Jumla ya Programu Kuu	16,430,090,000
Jumla Kuu	**197,290,176,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kutupitishia Bajeti yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Amali bila ya mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio haya. Ahsante*: (Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kabisa kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake na timu yake nzima. Kwanza kabisa kwa kupitisha Bajeti yao nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini chengine Mhe. Wajumbe niwapongeze Mawaziri wote pamoja na Manaibu Waziri ambao wametoa ufafanuzi na niwapongeze sasa Waheshimiwa Wajumbe *backbenchers* kwa michango yao mizuri kabisa na naomba tuendelee hivi hivi tukiwa tunapitisha bajeti, tukiwa tumetulia kabisa leo katika siku ambao tumetulia kupitisha bajeti ni siku ya leo. Niwapongeze sana na hiyo

haimaanishi kwamba buti msipige endeleeni kupiga buti ili kwa kutaka kujua nini kinaendelea katika Mawizara yetu. *(Makofi)*

Lakini pamoja na kushauri ambayo ndio kazi yetu kubwa Waheshimiwa Wajumbe wa Wawakilishi.

Sasa niseme hayo nazidi kumpongeza Waziri nafikiri katika Wizara ambayo imepata *minimum* mabuti ni wizara hii, hongera sana Mheshimiwa. Sasa hili hii linadhihirisha kwamba wanawake tunaweza. (*Makofi*)

Nashukuru sana na basi baada ya hayo machache niahirishe kikao hadi tukijaaliwa kesho asubuhi saa tatu.

(Saa 12:28 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 26/05/2017 saa 3:00 asubuhi)